

MASWALI NA MAJIBU



Na tuendeleo kusimama kwa muda mfupi tu tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi.

Mungu Baba mwenye fadhili, tunakushukuru asubuhi hii toka kilindi cha moyo wetu, kwa sababu wewe waweza na unapenda kujibu maombi yetu. Nasi twaomba kuwa utapokea shukrani zetu kwa yale umekwisha tutendea sisi. Tunangoja kwa hamu kuu msaada Wako asubuhi hii, na tuondokapo langoni mwa jengo hili, na tuende nje hapa watu tofauti kuliko tulivyokuwa tulipoingia. Na Roho Mtakatifu atuumbe asubuhi hii, tabia zetu, na atufanye raia wa Ufalme Wako kwa kuwa twaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina. (Mwaweza kuketi.)

² Nasikitika kwa kuchelewa kidogo, lakini nilikuwa na mambo machache ya kufanywa, na watu wengi wagonjwa na mahojiano kabla sijaingia jengoni.

³ Na kwa hivyo, tuna furaha kuwa hapa asubuhi hii na kuwaona ninyi nyote watu wazuri. Nami nataka kuwashukuru watu hao—wale waliotuletea hivyo vitu vizuri, zawadi kwa mke wangu na kwa—na—ndugu yule aliyenitumia bunduki yake ya kulungu. Bwana ambariki. Yeye—kasema yeye anazeeka na hangetaka kuitumia tena, naye alitaka mimi niichukue; kwa hivyo ni—ninashukuru hakika kwa hayo—kwa hayo. Mradi tu mimi hai, Ndugu, mradi tu naweza kujisaidia mwenyewe, nitakuwa nayo. Sitaiweka kamwe mkononi mwangu isipokuwa niwaze juu yako na nikuombe.

⁴ Sasa, tuna...Kuna mambo mengi ya kufanya leo, niliwaza labda hali niko hapa ningechukua maswali kadha na kuchunguza yale yaliyokuwa juu ya moyo wa kanisa—watu mbalimbali. Bila shaka nilifanya hivyo! Nimepata maswali yanayotosha kunikawisha hadi ule Utawala wa Miaka Elfu utakapozana! Sikujua yangelipatikana mengi hivyo. Ni—nina mia ndani humu, na kuna mia au zaidi yaliyoletwa asubuhi hii. Kwa hivyo sitaweza kamwe kuyajibu, nadhani, sawasawa, kwa sababu... Nayo—nayo ni maswali mazuri, mazuri sana.

⁵ Sasa, baadhi yake hayangesomwa hadharani, kwa hivyo mwajua, nimewauliza wao...Kama ni yale siwezi kuyaeleza kwa njia nyingineyo...Ni shida za kinyumbani na... Mwafahamu. Nami—nami nimeuliza nikutane nao—mume na mke kwa mahojiano ya kibinafsi, ili niweze kuongea nao faraghani kuhusu mambo haya. Si mambo mabaya; ni mambo ambayo yapasa yasuluhishwe kati ya familia, ni tabia za mwanadamu na mataifa ambazo tuna...wakati tunaishi na kadhalika, yanayozusha mambo haya, na ni shida zinazohusu

jamii ya kibinadamu; nayo sharti yajibibe. Na kwa hivyo, nitafanya kila niwezalo kuyajibu kwa njia bora sana.

⁶ Wakati mwingine katika kujibu maswali, inachukua wakati mwingi; nami sitaki nikose hata moja. Nitapata kila moja yayo kwa makini niwezavyo. Sasa, yako niliyaingiza kikapuni hapa, kuyajibu, na—na kuandika andiko kama yanipasa niwe nalo, na—na kuyarudisha. Ndipo nilikuwa macho jana yote, na sehemu kubwa ya usiku uliopita, na tangu mapambazuko asubuhi hii. Nami nilipata karibu mara mbili za haya hapa yaliyoletwa asubuhi hii. Kwa hivyo, nadhani vile tutafanya, Bwana akipenda, nitayajibu hadi—kadiri niwezavyo hadi karibu saa sita mchana, ndipo tutaondoka, kisha mrudi tena jioni hii na—na nitajaribu kumaliza mengi niwezavyo usiku huu, na kuona kama naweza kupata kuyamaliza. Na labda sitawachosha kwa muda mrefu sana katika muda mmoja wa kuyajibu. Nami nadhani itawapa nafasi ya kuondoka na kupumzika, na kuburudika kidogo, kulala kidogo na cho chote kile, na mrudi mkiweza. Msipoweza, naam, Ndugu Fred Sothmann, nadhani, ayanasa haya. Je, yanaswa? Vema, sawa. Naam, wako chumbani wakiyanasa, na—na kanda hii huenda ika—kama ni sawa—huenda ukapata kanda; itawekwa na kuitwa *Maswali na Majibu* kwa sababu kuna maswali magumu sana ndani humu na kitu fulani. . . Mengi yayo yanahusu mafundisho ya kanisa.

⁷ Sasa, ningependa watu wajue kwamba wakati mwingine katika kujibu maswali haya, ni vigumu. Inahitaji neema nyingi kusimama hapa, kama mnajua upendo nilio nao kwenu watu. Singeudhihirisha. Hata siudhihirishi kwa watoto wangu; hata siudhihirishi kwa upendo wangu—wangu mwingi sana kwa mke wangu nipaswavyo kufanya, kwa sababu mi—mimi nina moyo mwepesi, nami huendelea kufanya, kufuata safu mmoja. Kuna kitu kimoja pekee ambacho ningedhihirisha upendo wangu wote kwake; hicho ni mwenyezi Mungu. Nami—nampenda Yeye mbele ya yote. Watu wengine nawapenda, lakini si—sitaki kupata—sitaki kuchafua upendo huo nilio nao Kwake; na huo uwe wa kwanza. Kwa hivyo basi, ninapojibu maswali yenu, nayajibu kwa upendo moyoni mwangu kwenu; lakini kuna moja moja lililo mbele yangu daima: hilo ni Yesu Kristo (ona?), jinsi Yeye angelijibu.

⁸ Wakati mwingine huenda ikanipasa kujibu. . . Huenda likawaumiza, huenda likawakwaruza, nami—nami sikusudii iwe hivyo. Ninayajibu tu na kusudi moja, kama nilivyosema, Kristo mbele yangu. Nami yanipasa, kukumbuka kuwa ni Yeye ambaye nina. . . sina budi kumtolea hesabu. . . Kwa hivyo upendo wangu wa kwanza ni Kwake; wa pili ni kwenu watu, na kwa hivyo mimi—kanisa Lake ambalo Yeye amenunua kwa Damu Yake Mwenyewe. Na Yeye hakika awapenda kuliko alivyojipenda Mwenyewe, kwa sababu Yeye alijitolea Mwenyewe kwa ajili yenu. Ninyi ni nunuzi ya Damu Yake, nami, na—naishughulikia

kwa uangalifu na kwa unyofu sana kadiri ni juavyo. Lakini basi, katika kutenda hivyo wakati mwingine mnadhani, “Hayo yalikuwa matamshi ya kiburi sana (Niko karibu. . .); ni makali na hayakolei.” Nafanya hivyo nikifikiria habari Zake (ona) kujaribu kufanya—kusudi wengine—kila mtu aone tu kuwa haina budi kuwa hivi. Si kwa—kwa kuumiza au si zaidi ya kuhakikisha tu kuwa watu wanalifahamu, nami natumai kila, mtu analipokea katika njia hiyo. Na sasa, ndani hapa tunapata kujua nini kilicho katika nia zetu.

⁹ Na nionapo ninyi nyote mmekusanyika asubuhi hii na kila kitu kimerundikana hapa, nami nadhani tuna makutano yaliyojaa sana katika—katika kanisa lingine. Kanisa shirika limechukua re—redio au simu ya—ya namna fulani inayosikizwa. Hilo ni. . . Kanisa hili limejaa sana asubuhi hii, nafahamu. Ndugu. . . Au ndugu mwingine ana ka—kanisa lililojaa sana ambalo linapata haya moja kwa moja kwa simu toka hapa hadi kwa kanisa hilo. Ili haitawapasa kukanyagana miguu na kadhalika ukutani.

¹⁰ Sasa usiku huu, Bwana akipenda, tuta—tutaanza mapema usiku huu. Ningependa kumwuliza mchungaji na ha—halmashauri kama wange. . . Hebu tuanze mapema kidogo usiku huu kwasababu watu, baadhi yao wako hapa, nao wana safari ndefu ya motokaa. Nami nataka kuanza ikiwezekana saa moja mapema usiku huu, kama tungeweza, na kuyamaliza hayo. Kwa hivyo mara tu mpatapo chakula cha mchana saa 12:00 au wakati wo wote, naam, ningeanza. Ona? Tuseme, ninyi kawaida huanza saa 1:30 sivyo? na iwe—Hebu mimi niwe jukwaani ifikapo saa 1:00. Ona? Na ifikapo saa 2:00 au saa 2:30, au kitu kama hicho, ingewapa ninyi nafasi ya ku—kuenda manyumbani mwenu na mwe tayari kwa kazi ya kesho, kama kuna kesho.

¹¹ Sasa, Bwana awe nanyi na awabariki sana, nami nitaingia mara tu ibada hii itakapokwisha na kuyachukua maswali mengine na kujaribu kuyajibu. Naandika juu yayo, na—maandishi madogo na kadhalika, ambayo na—naweza. . . Husahau Maandiko. Ndipo ninapokuwa chumbani nikisoma kirefu, basi nina (napenda kutaja tena mahali fulani, na ninapo hapa) na—yameandikwa tu kwenye kijikaratasi. Na kwa hivyo kama iko katika—katika kamusi ya maarifa yote yanipasa nitafute, au usemi wa neno, au jina, nimeyaandika mbele zangu. Hainipasi kuleta vitabu chungu nzima na kadhalika; ninayo hapa.

¹² Sasa, kama swali haliwaridhishi vema, basi, labda nimekosea. Ona? Hu—hu—huenda nimekosea, kwa sababu mambo haya ni kadiri ninavyofahamu. Nami nataka m—mhudumu ambaye huenda ana kusanyiko lake, au kusanyiko la kanisa fulani ambao wangesikiza maswali haya. . . Sitaki hili. . . Kama inahusiana vyo vyote na mafundisho yenu na kusanyiko la—la—lako, nataka kusanyiko hilo wafahamu

dhahiri kuwa haya ni—mafundisho yetu tu hapa maskanini. Sijaribu kuyasukumiza juu ya makundi mengine ya watu. Nami—ninataka kuwa mkristo moyoni mwa—mwangu, kuwa nafundisha yale ninayoamini. Nasimama kwa dhamiri yangu. Kama nikipatana kwa hilo, mimi ni msaliti kwa Kristo na mnafiki kwenu; na i—inanipasa kudumu mwaminifu kwa yale naamini kuwa ni kweli. Lakini kila mtu ana haki kufanya vivyo hivyo. Mungu ndiye Hakimu wetu sote.

¹³ Sasa, kabla tu hatujaanza, nilidhani ningemtaja mwanahistoria mzuri, Paul Boyd. Wengi wenu mnajua; yeye huhudhuria maskani haya. Amerudi hivi punde toka Yerusalemu na kuhudhuria Maonyesho ya Ulimwenguni. Yeye zaidi sana ni mwalimu wa unabii, naye ni mwanahistoria, mojawapo wa walio bora sana. Yeye ni Ndugu Mmennonite—alikuwa—na amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na kwa hivyo amekuwa rafiki msiri wangu. Naye kila mara alichunguza na kuandika orodha ya kila kitu nilichosema kuhusu unabii, kuchunguza aone kama ilitimia.

¹⁴ Na sasa, yeye ameniandikia hapa (kwa kuwa yuko humu Marekani tena sasa), na yako kwenye ubao wa matangazo, nadhani, asubuhi hii. Ameandika karatasi ambayo aliweka katika mojawapo wa makaratasi au chochote kile, kuhusu unabii wa kusisimua. Naye ataja kitu cha tano, nadhani, ni cha tano ambacho niliona miaka thelathini na mitatu iliyopita kuhusu mafanikio ya—ama, maandeleo ya sayansi. Na ye yote wenu anayekumbuka mmeyaandika. Ninayo katika vitabu vyangu. Na kila kitu ambacho Bwana aliniambia—huniambia mimi, nakiandika, yaani kile cha muhimu ambacho—au mambo ambayo naweza kuwaambia watu.

¹⁵ Nami niliwaiza asubuhi hii, kabla sijaanza... Haya si mahubiri, lakini sisi tuko hapa kuketi pamoja kupata kujua sisi kwa sisi yale yaliyo mioyoni mwetu. Na tuyachambue mambo haya sasa kama tulivyozifuatilia zile nyakati za kanisa na kadhalika. Nadhani ni vizuri kutulia kwa mkutano mmoja au miwili, na kuchunguza na kuona yaliyo ndani ya mioyo ya watu, na ndipo kuendelea tokea pale. Mwaona? Kisha tuyarudie tena na—katika mfululizo wa ibada. Bwana akipenda, nataka kufanya hivyo hapa maskanini kabla ya muda si mrefu, mfululizo wa ibada nyingi; mwajua lile ninalokusudia, za—za masomo mbalimbali; na nizidi kusonga mbele hata atakapokuja kunichukua au niende kumlaki Yeye, mojawapo. Ona?

¹⁶ Paul Boyd aliandika hapa kuhusu hayo mambo saba niliyoyaona katika mwaka wa 1933, ambayo yangetimia. Naye huyachunguza kwa makini, ustadi, awezavyo, kwa sababu yeye ni mwanahistoria. Naye huyachunguza, yale hasa usemayo. Naye aliona mambo hayo yaliyotabiriwa miaka mingi iliyopita: Jinsi huyo Mussolini... na yale yangetendeka kwake, na Hitler, na yale yangetendeka kwake; na jinsi Ukomunisti ungechukua

Ufashisti na haya yote; na jinsi ile Ngome ya Siegfried ingejengwa. Na jinsi Waamerika wengeshindiwa pale (nao hawangelikubali hata yapata tu miaka miwili iliyopita, nao wana picha za Ujerumani za kule kuzingirwa; nao walivawa sana. Nusura . . . Walipoteza karibu jeshi lao lote papo hapo); na mambo hayo yote yaliyofanywa.

¹⁷ Na sasa, pia inasemekana, “Na itakuwa, ya kwamba kabla haujaja wakati wa mwisho, motokaa zitachukua umbo la yai, kuwa zaidi kama yai, nami niliona jamaa ya Kiamerika ikiendesha kwenye njia kuu katika motokaa ambayo. . . Walikuwa wameketi wakitazamana, na walikuwa na meza, nao walikuwa, ilionekana kama, wakicheza mchezo wa mirabaraba au kucheza karata. Nao hawakuwa na usukani wo wote katika motoka ile. Na Iliendeshwa na nguvu fulani pasipo usukani. Wangapi wakumbuka nilipotabiri hayo (ona?), ambao walikuwepo?”

¹⁸ Sasa, kwenye Maonyesho ya Ulimwengu tayari wanauza motokaa hiyo. Hapa kuna. . . Inauzwa sasa; kampuni fulani kubwa imenunua hizo kwa wingi. Na motokaa hii, iko hapa. Paul Boyd alikumbuka unabii huo, alitazama katika kitabu chake yale niliyokuwa nimesema, na akapiga picha ndani mle. Ndiyo hiyo, katika umbo la yai hasa, ikiwa na viti viwili vilivyokaa *hivyo*, na viti viwili vimekaa *hivi*, na meza imewekwa katikati ya kuchezea karata na mengineyo juu yake, vivyo hivyo.

¹⁹ Neno la Bwana ni sahini kamili kabisa. Hayo yalikuwa mwaka wa 1933. Hiyo ingekuwa . . . Hebu tuone, hiyo ingekuwa mingapi? Miaka thelathini na miwili iliyopita, sivyo? Huu ni ‘64.’ Naam, thelathini . . . Naam, miaka thelathini na mmoja iliyopita. Miaka thelathini na mmoja iliyopita Bwana aliniambia hayo, na ndiyo haya hapa na kuna kampuni hapa ambayo imekwisha ziagiza; na na kampuni za malori na mengineyo zinafanya malori yaundwe vivyo hivyo. Wanaweza kuyasimamia moja kwa moja toka kwa makao makuu hivyo, haihitajiwi hata kuwa na dereva ndani yake. Na ziko hapa zimekwisha tengenezwa, na motokaa ziko hivyo. Sasa, yako kwenye ubao wa matangazo kule nyuma, nanyi mnaweza kusoma unabii na mwone tu jinsi Mungu wetu alivyo sahihi, jinsi Neno Lake . . . Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitatanguka.”

²⁰ Tazama tu, miaka thelathini na mitatu iliyopita. Mwajua jinsi—jinsi katika mwaka wa 1931, au wo wote ule, muundo wa motokaa ulivyokuwa; ingeonekana kama mabaki ya kale. Ulisema, “Ingefanana na yai—kuwa kama yai.” Hakika, nadhani, hakuna ye yote humu, anayeishi leo au kati yetu aliyenisikia nikisema hayo. Ni. . . mmesikia nikiyasema katika nyakati zote, lakini. . . naam, hapa kuna mwanamke anayeketi hapa. Naam, Bi. Wilson, hapo ni wakati yeye aliponywa, akifa kwa kifua kikuu (mwanamke yule, mumewe na bintiye walikuja kuniita mimi nimwombe) angalitokwa na damu hata pembe—

pembeni mlijaa fo—foronya na kadhalika vilivyolowa damu. Na madaktari walisema, “Hakuna njia ya kumfanya apate kuishi,” na hata . . . Yeye alikuwa akijaribu kuniambia jambo fulani kabla hajafa, na damu hiyo ingevuja kote juu ya mablanketi na mashiti alipokuwa pale, alipojaribu kukohoa. Nami nilimwondosha kitandani mle, na kumpeleka katika mto baridi pale, na maji ya barafu, na kumbatiza kwa jina la Yesu Kristo. Na hiyo imekuwa miaka thelathini na mitatu, na yeye yuaketi hapa leo, angali anaishi, wakati wengi wa watoto wanene na wenye afya wameaga dunia. Naam. “Neema ya ajabu, ni tamu vipi inapotamkwa, iliyoookoa fukara kama mie!” Hiyo yaonyesha tu jinsi inavyotimilika kikamilifu wakati ni BWANA ASEMA HIVI.

21 [Mwanamke fulani aongea na Ndugu Branham katika kusanyiko—Mh.] Naam, sawa, Dada. Naam, bwana! Wanawake . . . Nilisema wanawake wangekuwa wazinifu sana katika . . . Sasa, mwajua miaka thelathini na mitatu iliyopita jinsi walivyovalia. Kasema wangekuwa wazinifu sana, hata wangetembea barabarani na—hadi—kama kwamba wamevalia nguo zao za ndani pekee. Nami nilisema, “Kisha itakuwa kwamba watakuwa waliojiaibisha sana, hadi watavaa kitu fulani kama jani la mtini.” Niliona hayo, nao wanacho, nao wanakivalia. U—uzinifu wa wanawake ungekuwa wa hali mbaya mno na ya kuaibisha . . . Hatuwezi kushuka chini zaidi tena sasa; huwezi kuwa mbaya zaidi. Mwanamke amefikia mwisho! Ona, hawatakuwa kamwe uchi wa mnyama. La, wao . . .

22 Nimewahubiria watu, wanawake kwa makumi elfu ambao hawakuvalia nguo yo yote (ona?), wavulana, na wasichana, na wote hao, lakini hawajui kuwa wako uchi. Ona? Hawajui hilo. Na jinsi wanawake wafanyavyo siku hizi . . .

23 Nilikuwa naongea usiku mmoja na marafiki wangu kadha tulipokuwa juu kule mlimani, na kijana mwanamke . . . Nilikuwa nimemwomba mtoto wake mchanga hivi punde; alikuwa na kifafa; na mtoto yule amepona. Na jamaa ndogo maskini, nyuma kule yenye shamba ndogo la tumbako lililozunguka nyumba—na yapata vyumba viwili vitatu ndani yake—na watoto saba au wanane . . . Mwanamke yule anafanya kazi (ole wangu!)—mwenye shoka kubwa kule, akikata kuni na mengineyo, na—na kulima shamba, na kuweka vitu kwenye mikebe. Nami nilimtaazama maskini mwanamke yule—nguo ile ile ambayo amekuwa akivaa kwa mwaka mmoja au miwili, na imeraruka na kila kitu . . . Nami nilikuwa najaribu kupata baadhi ya nguo za Meda kumpelekea juma moja baadaye.

24 Na—na tuliona tukisimama pale, mimi pamoja na ndugu kadha, mama yule akimlisha mtoto wake. Yeye alitoa tu matiti yake toka kwa—toka kwa—toka kwa nguo yake na kuanza kumpa mtoto; na lilikuwa la kugutua kidogo; hivyo ndivyo mama yangu alivyoniilisha! Ndivyo hasa.

25 Nina heshima kubwa kwa mwanamke kama huyo kuliko nilivyo nayo kwa baadhi ya wanawake hawa wanaovalia sidiria wapate kujitupa nje. Hata hawaonekani kama ni wanadamu. Wana kusudi la kufanya hivyo; huo ni uzinifu, wasiomcha Mungu. Mwanamke anayevaa mavazi mengi na kujaribu kujifanya aonekane kama kitu fulani yeye asicho... Mimi... Naam, wanawake hawa—hawako hivyo hasa; ni baadhi ya upuzi fulani wa Hollywood. Na roho wa Shetani anajaribu kuwaingia wanawake wajaribu kuvutia wanaume kwa jinsia. Mwanamke alipewa matiti apate kumlisha mtoto wake mchanga. Ndivyo hasa. Mwanamke yule hajastaarabika, lakini ana njia safi. Nina heshima zaidi kwa hayo, kwa mwanamke huyo hivyo, kwa sababu yeye... hivyo ndivyo mama yake alivyomkuza; hivyo ndivyo... Hawa—hawa—hawajali kamwe. Mtoto hulishwa kama picha ile ya bikira Mariamu ambayo mngeiona. Na kama watu wangeweka tu mawazo yao hivyo, ingalikuwa tofauti.

26 Lakini unapoondoka kwenda nje na labda uvae bluasi au cho chote kile, na ndipo ujiongezee mwenyewe sidiria na vinginevyo, ambavyo huonekana vibaya sana na kumfanya mwanamume... Je, watambua kuwa huyo ni roho wa Shetani juu yako? Jamani, naam! Kwa hivyo hutaki kufanya hivyo, dada. Msifanye hivyo; hayo ni mapambo ya Hollywood na mtego wa Shetani! Unapofanya mwanamume awaze jambo fulani baya kukuhusu; na unapofanya hivyo, ndipo una hatia ya kuzini na mwanamume huyo, kwa sababu ulijionyesha mwenyewe hivyo kwake. Huwezi kujizuia jinsi ulivyoumbwa, lakini enda na ukae tu jinsi Mungu alivyokuumba. Ona? Usijaribu kujifanya mwenyewe kitu kingine. Kaa tu kama mwanadamu. Hilo latisha? Vema labda hilo lajibu maswali fulani ya mtu fulani pia.

27 Baba yetu tunakushukuru Wewe leo kwa ajili ya Yesu Kristo na kwa ajili ya unyofu wa Neno. Ninapoonza Wewe dhahiri ukifanya maneno hayo yatimie, lanifanya niwe na bidii kukaa na Kweli na kila neno la Kweli. Kwa hivyo naomba, Baba, kuwa utatubariki sisi asubuhi hii, hawa watu wapendwa. Na nikujua kuwa kanda hii inaenda mahali pengi watakakosikia hata matamshi yale nimenena sasa... Si—hayakuwaziwa mbeleni; Wewe waujua moyo wangu. Ilikuwa tu kwenye nia yangu, nami naamini Wewe ulinitaka niyaseme. Nami niliyasema, na yamekwisha sasa. Na—na hivyo ndivyo ninavyosadiki hasa na yale ninayoamini ungeniruhusu niseme.

28 Na kila mwanamke anayesikia hayo kote nchini na kote taifani na ulimwenguni; hebu aone aibu na aone kile kilichotendeka, na ajivike kama mwanamke wa heshima basi, asiwe na hatia ya uzinzi. Ulimuumba mrembo, kiumbe cha kupendeza sana, sehemu ya mwanamume, kuwa hivyo apate ku—ku—kumvutia, wao wawili waweze kuwa mmoja, kwa sababu yeye alitoka kwa mwanamume. Naomba, Mungu, kuwa

mwanamke atatambua kuwa urembo wake na jinsi alivyo, unamhusu tu mumewe. Tujalie, Baba.

²⁹ Twaomba kuwa Wewe utatusaidia sasa tunapojaribu kueleza maswali haya. Hatufai kwa mambo kama haya, lakini hebu Roho Wako mkuu aje, Bwana, ambaye ni utoshelevu wetu; na ajibu maswali katika mioyo mingi. Twakuomba Wewe kwa ajili ya yale umetupea sisi: *Zile Nyakati za Kanisa* na *Zile Muhuri*, na...Ee, jinsi Wewe umetushughulikia sisi katika mambo makuu mno ambayo yamekuwa makuu kwetu, Bwana, kwa sababu twaona wakati wa mwisho wakaribia.

³⁰ Sasa, ku—nilidhania ingalifaa au yafaa kwa ajili ya Ufalme Wako kama ningeliwachunguza watu. Wakati mwingi chini ya upambanuzi na kwa kuona vitu vingi mbalimbali, na huwezi kushughulikia kimoja; kwa hivyo nikiwaza—ningeacha tu wao waandike yale wao waliwaza mioyoni mwao. Na ndipo ningalijua nia zao kwa kipande cha karatasi ambacho wamekiandika, na ndipo Wewe utupee jibu sahihi. Sisi sote tunangoja, Bwana. Njoo tulipo sisi, Bwana, na tembea juu na chini ya marefu ya kanisa, shughulikia kila mmoja kulingana na mapenzi Yako. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

[Ndugu Branham aongea na ndugu fulani kuhusu kunaswa kwa kanda—Mh.]

³¹ Sasa, kama ninavyosema sasa tena, tunapoanza, kwa—hao wahudumu au watu katika sehemu mbalimbali za nchi, au watakaosikia kanda, mna—mna (kama kanda hii ni sawa)—haya ni maswali mioyoni mwa watu wa maskani haya, ambapo hatuna dhehebu lo lote, ushirika tu sisi kwa sisi. Nami naamini kuwa itakuwa—kunyosha mawazo yetu, kuwa tutajua la kufanya na kujua jinsi ya kuishi vyema baada ya maswali yetu kujibiwa. Najua, kwa kuyasoma tu, yalikuwa baraka kwangu.

³² Sasa, nimeyaweke hapa katika kifurushi, nami nitachunga na itakapofika saa sita dakika tano kasoro, nitamwacha mwondo. Halafu, turudi tena jioni hii saa kumi na mbili na nusu.

Swali la kwanza nililo nalo, naamini ni maswali matano yakifuatana, yamepigwa chapa kwenye karatasi ya manjano.

236. Nini maana ya haya? Mathayo 24:19, “Ole wao wenye mimba na waamwishao siku hizo!”

Ajabu ni kwamba, bila kujua hilo, nilitaka kusema hili kuhusu mwanamke, na liko hapa wakati huu, swali la kwanza.

³³ Sasa, Mathayo 24:19. Yesu alikuwa ameulizwa maswali matatu. Katika haya maswali ilikuwa kwamba: Je, ni lini ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe? Nayo ni nini dalili ya mwisho wa ulimwengu? Na—na maswali matatu mbalimbali Yeye aliyoyouliwa. Naye ayajibu katika njia tatu mbalimbali, ajibu kila swali. Je, ni lini ambapo halitasalia jiwe

juu ya jiwe? Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako? Na dalili ya mwisho wa dunia ni nini? Na Yeye ayajibu katika njia mbalimbali tatu. Yeye awaambia ni lini ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe, ni nini dalili ya kuja Kwake; halafu, mwisho wa dunia. Na wakati mwingi, upochunguza kwa makini, sasa, jinsi Yeye anajibu (ona?), utayafarakanisha na kuyatupa yote katika wakati mmoja; kisha utafarakanika.

³⁴ Sasa si kuwadharau ndugu zetu—ndugu zetu wa Adventi wanaoyachukua haya yote kuwa ya wakati ujao. Kuingilia somo hilo la siku ya sabato kwamba: “Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya sabato,” kasema (ona?), wangukuwa bado wakiadhimisha Sabato. Sio kuitupilia mbali kwa ndugu wale, hiyo haingekuwa tabia ya Kikristo kufanya hivyo, lakini ili tu kuinyosha. Ona?

³⁵ Ulimwengu wote wa Kristo ungewezaje kukusanyika ndani ya ukuta, na kuta zile hazifunguliwi na kufungwa kama zilivyokuwa wakati ule. Ona? Ingalifaa nini, kama ilikuwa wakati wa baridi au wakati wa hari kwa watu walioishi katika eneo la tropiki. Ona? Ilikuwa tu kwa Israeli pekee. Huo ndio wakati ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe. . . *ole wao wenye mimba, na waamwishao siku hizo*, kwa sababu mama aliye na mimba (ona?), ingekuwa vigumu kwake kukimbia, na kwa wale waamwishao watoto wao wachanga kuwabeba, kwa sababu iliwapasa kuondoka Yerusalemu nje ya mji na kupanda—kupanda ile milima ya Judea.

³⁶ Na sasa, ningekaa tu asubuhi yote kwa hilo jambo moja pale, ili kulifanya dhahiri; lakini nitajaribu kugusia tu sehemu muhimu niwezayo, hata watu waelewe, na ndipo niendeleo na swali linalofuatia.

³⁷ Sasa, Yesu alikuwa amewaambia kuwa wange. . . “Mwonapo Yerusalemu imezingirwa na majeshi, ndipo aliye shambani, asirudi nyuma mjini kuichukua nguo yake, kuchukua cho chote toka nyumbani mwake; asirudi tena mjini kwa vyo vyote vile, lakini akimbilie Judea, maana kutakuwako na wakati wa dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu.” Na hayo yote yalitimia katika siku zile yule jemadari wa Kirumi, Tito, alipouzingira Yerusalemu, akauteketeza mji ule, na kulikuwako tu na—na akawaua watu hata damu ikatiririka toka malangoni na kutiririka nje—nje barabarani. Yeye aliuzingira. Sijui ulikuwa mwaka gani, ambapo yeye alichukua majeshi yake na akapanda na kupiga hema karibu na huo mji. Na hata watu, wanawake, walichemsha watoto wao na kuwala, walikula maganda ya miti, nyasi toka mchangani. Hayo yalikuwa kwa ajili ya kulikataa Neno. Hayo ndiyo yaliyosababisha hayo. Ndiposa. . .

³⁸ Sasa, wale waliolipokea Neno, kama Josephus, yule mwanahistoria mkuu aandikavyo. . . Yeye aliwaita wala watu,

kasema walikuwa wakila mwili wa Mtu aliyeitwa Yesu wa Nazareti, ambaye Pilato alimsulubisha; nao walikuja usiku na kuuiba mwili Wake, na watu hawa waliutoa na kuukata vipande vipande na kuula. (Walikuwa wakipokea Ushirika, mwaona. Hawakuja.) Huo ulikuwa tu uvumi ulioenea, kama walivyo nao juu yetu na Wakristo wengineo. Mwaona? Wao husema mambo, lakini. . .

³⁹ Sasa, watu wale waliokuwa. . . Sababu, “Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi,” Judea ilijaa barafu. Ona, Krismasi? Basi, Yesu alizaliwaje mle juu kwenye milima iliyojaa barafu? “Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya Sabato” (ona?), kwa sababu siku ya Sabato malango yalifungwa, nao wangeshikwa katika mtego wao. Kama Tito angefika pale siku ya—ya—ya Ijumaa aduhuri, walijizingira ndani mle kwa ajili ya Sabato, kwa sababu malango yalikuwa yamefungwa. Malango yalifungwa siku ya Sabato na hayakufunguliwa. Hakukuwa na kuingia wala kuondoka mjini siku ya Sabato.

⁴⁰ Na sasa, mwaona kile kilichotendeka? Ndipo Yeye alisema, “Ole wao wenye mimba na waamwishao siku hizo,” (ona?) kwa sababu kutoroka na kukimbia. . . Na kulingana na historia, hakukuwa na hata mmoja wao aliyemwamini Yesu na kuliamani Neno ila wale waliokuwa wakitazamia hayo yatendeke. Nao waliepuka, na wakaenda toka Yesusalemu hadi Uyahudi, na—na wakatoroka wasije wakauawa, na hakuna hata mmoja wao. . . Kwa sababu walionywa na Mchungaji wao na walikuwa wakitazamia saa hiyo ije. Waliposikia Tito anakuja, wakakimbia, wakatoroka wasije wakauawa, wakaondoka mjini.

Sasa, swali la pili linafuata.

237. Mathayo 24:24: “Watatokea manabii wa uongo—na—makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu.” Tutawatambuaje?

⁴¹ “Watatokea. . .” Katika hilo sasa unaingia katika kipindi kingine. Ona? “. . . watatokea makristo wa uongo na manabii wa uongo.” Kristo wa uongo ni mtiwa mafuta wa uongo, kwa sababu Kristo ni Mtiwa Mafuta. Wangapi wajua kuwa *Kristo* maana yake ni “mtiwa mafuta”? Watatokea watiwa mafuta wa uongo, nao watajiita manabii. Lakini mtawatambuaje? Kwa Neno; hivyo ndivyo mtakavyowajua, kwa Neno, kama wako sahihi. Tutawatambuaje? Itakuwa kwa Neno. Kama wao wana. . . Kama wao wanasema kuwa wana Neno, hali wanakana Neno, basi hawafai kitu kamwe, haijalishi wanafanyaje. Huenda wakaponya wagonjwa; huenda wakafungua macho ya vipofu; na kukana Neno, usiwakaribie. Haijalishi ni nini, kaa na Neno haijalishi (ona?), kwa sababu wakati mwingi nimeona uchawi na mambo mbalimbali yakitendeka chini—chini ya uponyaji.

42 Hapa yuaketi Ndugu Sidney Jackson, Dada Jackson asubuhi toka Afrika ya Kusini. Yeye angesimama hapa na kueleza somo hilo na awaambie mambo fulani kulihusu huko chini. Naam, hakika, watu huja kwa sanamu na kuponywa. Ona, kwa sababu gani?

43 Kama tu vile Dk. Hegre alivyonishambulia wakati mmoja, niliposema kuwa shetani hawezi kuponya. Na ilisemwa, “Mtu anyesimama mbele ya watu wengi kama wewe ufanyavyo, na theologia fukara kama hiyo,” kasema, “ukisema Shetani hawezi kuponya.” Kasema, “Tuna mwanamke jirani papa hapa ambaye hubeba lesu; na watu huja na kumzunguka na inawapasa kutia pesa katika hiyo lesu; ndipo yeye atazisugua na kung’oa nywele zake kichwani mwake na damu toka mishipani mwao na—na kuiweka juu ya nywele na kuzitupa nyuma yake; na inapombidi kutazama nyuma, ugonjwa unawarudia watu. Na,” Kasema, “asilimia thelathini yao hupona. Halafu unasema shetani hawezi kuponya?”

44 Nami niliwaza, “Jamani!” Nilimrudishia barua, nami nilisema, “Bwana:” Nilisema, “Ni ajabu kwangu kuwa mwalimu anayesimamia chuo cha Kilutheri angeweka theologia yake juu ya ujuzi badala ya Neno la Mungu.” Ona? “Neno la Mungu lasema Shetani hawezi kumfukuza Shetani. Hilo latosha; Yesu alisema hivyo.” Kama Shetani. . . Kasema, “Ndipo huenda ukashangaa jinsi watu hawa wanavyoponywa kupitia kwa hayo, huyo mchawi, ni kwa sababu watu hao wenyewe hudhani wanamwendea Mungu kupitia kwa mchawi huyo. Na uponyaji unategemea imani, si jinsi ulivyo mwenye haki, jinsi ulivyo mwema, jinsi ushikavyo amri, au lo lote lile, inategemea imani pekee. “Yote yawezekana kwao waaminio!” Ona? Haitegemie jinsi ulivyo mwema. Nimeona makahaba wakija jukwaani na kuponywa papo hapo na mwanamke mtakatifu anakufa jukwaani na kuukosa. Hakika, inategemea imani—*Kama waweza kuamini—si kutegemea haki yako.*”

45 Tazama hapa Ufaransa ambapo wao huenda kwa kaburi la mwanamke huyo, wanaingia humo kwa viti vya kusukumia wagonjwa na wanaondoka wakitembea, bali si kitu cho chote ila ushirikina tu, haidhuru, ni kuabudu mtu aliyekufa. Ona? Na wanaponywa haidhuru, kwa sababu wao hudhani wanamwendea Mungu. Sasa, si kwa kudharau Wakatoliki, nadharau utaratibu wa Kikatoliki, kama tu ninavyofanya utaratibu wa Kipentekoste, (ona?), mambo haya yote.

46 Sasa, wahudumu, najua hili litapenya ndani, lakini ninajibu maswali; nami nataka—nataka mwelewe hilo (ona?). Ni—ni—niwaambieni ninyi Kweli toka moyoni mwangu; Kristo akiwa mbele yangu kadiri nijuavyo. Ona? Ni taratibu hizo zote, na taratibu hizo zimewafungisha watu pamoja kama. . . Watu huenda kujiunga na Methodisti, Batisti, Presbiteria, Pentekoste, Katoliki; nao wanadhani wanamkaribia Mungu bali wanapitia

tu kwa taratibu fulani. Mungu huikubalia wakati mwingine na kuondoa magonjwa ya—yao kupitia kwa sanamu. Naam, kule kwa wale Wahottentoti wa Afrika wanapata uponyaji kwa sanamu na kadhalika (ona?), lakini wao hudhani wanamkaribia Mungu.

47 Wadhani mtawa wa kike Mkatoliki huenda na kujiunga na chama cha watawa wa kike wa Katoliki kwa sababu yeye anataka kuwa mwanamke mbaya? Anajiunga na chama hicho cha watawa kwa sababu yeye anataka kuwa mwanamke mwema. Mwanamume ye yote hajiungi na kanisa Katoliki apate kuwa mwanamume mbaya; yeye aenda pale na kujiunga awe mtu mzuri. Hu. . . “Vema, ni nini?” Wala wale Wahindi wa India, au wale Wahindu hawajiungi na Uhindu wawe wabaya.

48 Nilipoingia katika hekalu la—la Jaini ambapo nilihojiwa pale na kasisi huyo—kama papa aliyeketi juu ya mto mkubwa, miguu yake imepitanishwa, akishika vidole vya miguu yake—na kwa mtazamo fulani ambao yeye aliandikia mfano wa Maandiko ya Zaburi 23 kwa macho yake juu ya kipande cha chuma ambacho hakizidi—kisichozidi robo inchi. Sasa, na haiwezekani kamwe kwa mawazo ya kibinadamu kuandika hayo, naye aliyachora pale kwa macho yake ya kawaida; naye alikuwa mtu wa umri wa miaka arobaini au zaidi. Ona?

49 Naam hakika, ninyi—ninyi mnakaa hapa, mnasikia tu kuhusu Methodisti, Batisti, Presbiteria; yawapasa mwende kule nje kwa umishenari wakati mmoja. Mpate mambo ya kufungua macho yenu! Ona?

50 Sasa, unadhani kuwa hao dada wote wanaoketi pale; wao hawawezi hata—hawawezi kupika; hawawezi kula; inawalazimu kuomba kila kitu wapatacho. Hawa—wanajitengezea vifagio vidogo mikononi mwao kufagia mchwa na vinginevyo barabarani, kwa sababu wanaamini kuwa nafsi za waliokufa huja na kuwaingia wanyama; huenda wanawakanyaga jamaa zao. Hangalikanyaga mchwa, kuuwa inzi, ama cho chote kile; hawawezi kuchemsha kisu kuua viini kukifanyia kidole upasuaji. Humwacha mtu yule afe, wasije wakaua viini vya magonjwa; huenda ikawa ni—ni baadhi ya jamaa zao waliorudi. Ona? Unaendelea kuwa bora, na bora, na bora; mwishowe, unakuwa mwanadamu, mwanadamu bora zaidi, na kuendelea hivyo, hata unakuwa Mungu. Kuendelea tu, na kuendelea, na kuendelea, ikizunguka, ikiwa bora na bora zaidi.

51 Sasa, hawafanyi hivyo kuwa watu wabaya. Wanafanya hivyo kwa unyofu wa moyo, lakini mwaona, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu.” Kuna jambo moja pekee, enyi watu, ninalotaka kuwaambia kama—kama darasa asubuhi hii juu ya maswali haya, ni Neno, Neno la Mungu. Mpate kuamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye lile Neno, nalo Neno limefanyika

mwili sasa kwetu, likitimiza hasa yale Yeye alisema Yeye angeyafanya katika wakati huu. Vema.

Sasa, hivyo ndivyo mtakavyowajua, si kwa kanisa lao, si kwa kanuni zao za imani, si kwa ishara zao, si kwa madhehebu yao, si kwa uponyaji wo wote, si kwa lo lote, ila kwa Neno, Ona?

238. Mathayo 24:26 (linalofuata) inanena kuhusu “nyumbani” na “jangwani.” Nini maana ya hili?

⁵² Lamaanisha kutatokea makristo wa uongo na watiwa mafuta wa uongo, na kadhalika. Na nini maana ya *wapinga*? *Wapinga* ni “kuwa dhidi.” Itakuwa ni viumbe wawa hawa wakiwa dhidi ya Neno. Nao watakuwa jangwani, nyumbani, nao walisema, “Msiwafuate; musiwakaribie.” Ona?

Sasa, swali la nne:

239. Mathayo 24:28 (Mtu yule anaendelea moja kwa moja. Hawakuandika majina yao; naam waliyaandika. Samahani. Sitataja majina haya, kwa sababu si muhimu. Ona?) Mathayo 24:28: “kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakusanyika tai.” Mzoga ni nini na tai ni nini?

⁵³ Sasa, hilo ni swali nzuri, halina ubaya wo wote! Mzoga ni nini? Mzoga ni kile anachokula tai. Sasa, tai huhesabiwa katika Biblia, nabii. Nabii ni tai. Mungu—Mungu hujiita Mwenyewe tai, nasi tu “wana tai” basi, wa—waamini. Mwaona? Na mzoga waulao ni nini? Ni Neno. Po pote lilipo Neno, tabia halisi ya ndege itajidhihirisha yenyewe. Ona? Tai, anayekula nyama mbichi, hana budi kupata nyama iliyuawa wakati uo huo. Yeye si kipanga (ona?), yeye ni tai. Huwezi kumlisha vyakula vya kidhehebu; hana budi kupata chakula cha tai; hicho ndicho chakula cha wakati uliopo hasa, si yale Musa alifanya, si yale mtu fulani mwingine amefanya, si yale Sankey, Finney, Knox, Calvin, bali sasa hivi, Nyama iliyuawa kwa ajili ya siku hii. Na hiyo ni sehemu ya Kristo iliyokufa kufanya Neno hili lithibitishwe. Hilo ndilo wanalokula. Mnafahamu? Ona, Ona?

⁵⁴ Si yale Nuhu alifanya, yale Musa alifanya, wao ni vielelezo; twaona na kusoma yale wao walifanya, bali yale Yeye aliahidi kufanya sasa. Yeye alikuwa Neno nyuma kule; hilo lilikuwa ndilo Mzoga wa siku hiyo. Siku ya—ya Wesley lilikuwa mzoga kwa ajili ya siku hiyo; siku ya Luther lilikuwa mzoga kwa ajili ya siku hiyo; lakini hawarudi hayo. Hicho kimekwisha ambukizwa. Kile kilichosalia sharti kiteketezwe, hata cha Ushirika; usikiachie kizazi kinachofuata. Biblia ilisema mnapopokea Ushirika, kile kilichosalia, msikiache hata asubuhi; kiteketezeni. Kwa hivyo tutarejea kwa hayo? La, bwana! Tuna chakula kipya leo; hicho ni Neno lililoahidiwa kwa saa hii kudhihirishwa katika saa hii. Hapo ndipo tai walipo—mzoga ulipo. Tunaweza kukaa kwa muda mrefu kwa hilo, lakini nina hakika mnafahamu lile ninakusudia.

Vema, swali la tano:

240. Je, Bibi-arusi atakusanyika mahali pamoja kwa ajili ya kunyakuliwa, na je, itakuwa Magharibi?

⁵⁵ La, si lazima iwe kule. Naam, Bibi-arusi atakusanyika mahali pamoja. Hilo ni kweli, lakini sivyo mpaka kwenye ule ufufuo. Ona? “Sisi tulio hai, tuliosalia hata wakati wa kuja Kwake Bwana... Efeso-2 Wathesalonike sura ya naamini ni hapo, “Sisi tulio hai, tuliosalia hata wakati wa kuja Kwake Bwana hatutawatangulia (au hatutawazuia) wale waliokwisha kulala mauti (ulimwenguni kote); parapanda ya Mungu italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tulio hai, tutanyakuliwa pamoja nao ili tumlaki Bwana hewani.” Kwa hivyo, Bibi-arusi atakuwa pamoja aendapo kumlaki Bwana. Ona? Atakuwa pamoja, lakini halina maana kuwa sisi—lazima wawe mahali pamoja hivi; kwa sababu Bibi-arusi analala katika mavumbi ya nchi kote ulimwenguni, toka ncha ya kaskazini hata kwenye tropiki, na toka—toka mashariki hata magharibi, toka kaskazini hata kusini.

⁵⁶ Yesu alisema, “Mwana wa Adamu ajapo,” naam alisema, “ingekuwa kama nuru iangazavyo toka mashariki hata magharibi.” Jambo lote, kutakuwako na ufufuo, kunyakuliwa, na kuondoka. Na kabla hajanyakuliwa kumlaki Yeye . . .

⁵⁷ Tazama hekima ya Bwana. Sasa, na tuseme, kwa mfano, katika kuongea hili . . . Ninasema hili kwa mawazo ya neema na imani katika Neno, ambapo nasema “sisi.” Najitupa mwenyewe ndani pamoja nanyi nyote nami—na pamoja na mwili wote wa Kristo, ulimwenguni kote. Nina—naamini hilo. Nisemapo “sisi” basi, nakusudia, kwa neema ni—ninaliamini. Kwa imani naamini katika neema Yake, kuwa tutakuwa miongoni mwa wale watu watakaonyakuliwa.

⁵⁸ Sasa, jambo la kwanza litakalotendeka tutakapofufuliwa . . . wale walio hai watabaki tu . . . kufufuka kutaanza kwanza, kufufuka kwa wale wanaolala. Kutakuwa na wakati wa kuamka, na wale waliolala mavumbini sasa, sio wale waliolala katika dhambi, kwa sababu wataendelea kulala. Hawatafufuliwa kwa muda wa miaka mingine elfu. Lakini wale waliolala mavumbini watafufuka kwanza, nao wata—hii miili iharibikayo itavaa ile isiyoharibika katika neema ya kunyakuliwa ya Bwana. Kisha sisi sote tutakusanyika pamoja. Na wanapoanza kukusanyika pamoja, ndipo sisi tulio hai na tuliosalia tutageuzwa. Hii miili inayokufa haitaona mauti, ila tu kwa ghafula, itakuwa kama upepo uvumao juu yetu, nanyi mtageuzwa. Mmehadilishwa kama Ibrahimu alivyofanyiwa, toka kwa mzee kuwa kijana, toka kwa mkongwe na kuwa msichana. Huku kugeuzwa kwa ghafula ni nini? Na baada ya kitambo kidogo una—unasafiri kama wazo, na unaweza kuona basi wale waliokwisha kufufuka. Ee, ni wakati wa jinsi gani! Kisha tutakusanyika pamoja nao halafu tunyakuliwe pamoja nao kumlaki Bwana hewani.

⁵⁹ Si lazima, kama mjomba wako amezikwa Kentucky ya kusini, kama yeye apaswa kufufuliwa Indiana, au amezikwa Indiana na yapaswa apelekwe Kentucky ya kusini. Haijalishi yeye yuko wapi. . . Hao waliokufia baharini. Wale walioangamizwa katika ule uwanja wa tamasha na wakaliwa na simba, wale waliotupwa katika tanuru na hakuna hata mfupa utakaosalia au vumbi, bado watafufuka! Au walikuwa Roma, au uwanja wa tamasha kule Roma, au kama walikuwa katika pori za tropiki za Kusini, au katika eneo la barafu la Kaskazini, watafufuka katika wafu na kubadilishwa na kunyakuliwa; kisha walio hai watabadilishwa katika kufumba na kufumbua macho kisha tutanyakuliwa pamoja.

⁶⁰ Watazame wamishenari waliokufa kule katika huduma barani Afrika. Watazame hao waliokufia kule ng'ambo katika—katika—katika maeneo ya barafu kule Kaskazini. Watazame hao waliokufia katika viwanja vya tamasha, kote ulimwenguni, katika Congo, na kote ulimwenguni. Wamekufia kila mahali, China, Japan, kote ulimwenguni; na kuja kwa Bwana kutakuwa duniani kote, kunyakuliwa huku kutakuwa duniani kote.

⁶¹ Tazama kule kugeuzwa. “Wawili watakuwa kitandani; nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja,” wakati ule ule, “Wawili watakuwa shambani; nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja,” mmoja upande wa dunia wenye giza na mmoja upande wenye nuru wa dunia. Ona? Kutakuwa kunyakuliwa kutakaotukia duniani kote. Naam, kanisa litakuwa lote pamoja, lakini ni baadaye baada ya kuanza kwa ufufuo na kunyakuliwa.

⁶² Sasa, kama huioni kwa njia hiyo, naam, hiyo ni sawa sasa. Sineni hasa ninaposema hayo; tunanasa haya. Mwaona? Na huenda kuna wahudumu wengine ambao hawakubaliani nayo. Hilo ni sawa.

241. Mpendwa Ndugu Branham, swali langu ni juu ya ubatizo. Mtu anaokoka lini? Nilikuwa nimesikia ni mtu anapoamini. Wengine husema unapompokea Roho Mtakatifu umeokoka, hata ingawa hujabatizwa katika maji, kama vile alivyokuwa Kornelio kwenye Matendo 10:47. Wengine husema Paulo aliokolewa akiwa njiani kwenda Dameski, lakini katika Matendo 22:16, yasema kuwa alikuwa bado angali na dhambi zake siku tatu baadaye. Je, mtu aweza kubatizwa katika Roho Mtakatifu kama Kornelio alivyokuwa, na hali angali ana dhambi zake, kwa kuwa yeye hajapata ubatizo wa maji bado, juu ya—au haiwezekani mtu kwenda Mbinguni hadi amepata ubatizo wa maji, hata ingawa yeye ana Roho Mtakatifu?

⁶³ Sasa; rafiki yangu mpendwa. . . Sasa, ndugu huyu aliweka jina lake; simjui, lakini yeye aliandika jina lake. Lakini si—sitawataja majina, kwa sababu si muhimu; kwa sababu watu

wengine watawaendea na kusema, “Vema, si—sikubaliani na wewe kwa hili na lile.” Ona? sitataja majina. Mengi ya haya yameandikwa majina yao, lakini mimi—kwa ajili yangu. Ona? Nayarudisha tena ndani humu, ili niyaweke. Kwa hivyo ni mwandiko wa samawati; mengine yamepigwa chapa na njia mbalimbali.

⁶⁴ Sasa, swali hapa kwanza lilikuwa: “unaokoka lini?” Na linalofuata—linalofuata ni, “Je, dhambi yaweza kuondolewa nje ya ubatizo wa maji, kwa kuwa Kornelio alikuwa amempokea Roho Mtakatifu—yeye na nyumba yake na alikuwa bado hajabatizwa katika maji.” Na Paulo hakuwa—baada ya yeye kupata ujuzi wake kwa—akienda zake Dameski, yeye, pia, alikuwa bado yungali na dhambi zake hadi yeye alipobatizwa; kwa sababu ilisema (nimesoma Maandiko haya yote tena nipate kuwa na hakika). . . Na kwa hivyo ilikuwa. . . Yeye alisema, “Simama, enenda zako ukabatizwe, ukiliita Jina la Bwana—ukabatizwe, dhambi zako zipate kusamehewa (zifutwe), na—na ukiliita Jina la Bwana.”

⁶⁵ Ndiposa, “Je ubatizo wa Roho Mtakatifu. . . mtu anaweza kubatizwa Naye na bado wana dhambi zao na hawaja—na hawajabatizwa katika maji.”

⁶⁶ “Je, kuingia kwa mtu Mbinguni kunayakinishwa anapobatizwa, ijapokuwa wana Roho Mtakatifu; bali yapasa wabatizwe katika maji, kabla kuingia kwao Mbinguni hakujayakinishwa?” Sasa, naamini. . . Sasa, si—simjui ndugu huyu, na hilo ni zuri sana na ni swali lenye busara. Na yapasa lishughulikiwe kirefu, kwa sababu inatupasa tujue mambo haya. Ona?

⁶⁷ Sasa, naamini kuwa ndugu huenda ananiambia au ananifanya niseme (au labda yeye analiamini, sijui) na—ni kitu ambacho nadhani ni—ni kinyume kidogo cha ile Kweli, imani ya kweli ya Neno. Ni. . . Hili laonekana kama ndugu huyu anasema. . . Sasa, ambalo ni vema, Ndugu; huenda wewe umeketi hapa; na ni sawa. Ni—ninadhani hilo ni zuri. . . Nina furaha sana uliliweka ndani humu. Sasa, ona? Lakini siamini katika kubatizwa ndani ya maji iii uzaliwe mara ya pili (ona?), kwa sababu unapofanya hivyo, hilo lafuta ile Damu. Ona? Unabatizwa majini kuonyesha kuwa kuzaliwa upya kumekwisha tendeka. Ona? Huyu ni wa nje—mfano wa kuzaliwa upya. Jambo lote lategemea kabisa kuchaguliwa tangu awali. Ona? Lakini hatujui nani aliye na nani asiye, tunahubiri Injili. Kwa imani tunahubiri tu.

⁶⁸ Lakini juu ya kuzaliwa upya sasa, hapo ndipo natofautiana na ndugu wa umoja. Nanyi ndugu wa umoja mnaosikiza kanda hii kama ingeingia afisini mwenu, au nyumbani mwenu, au kati yenu watu mlio watu wa umoja, msikose kunifahamu, sasa, kuwa ni—ni—kwa sababu tu hatukubaliani.

69 Mimi na mke wangu hukosa kukubaliana, hakika hukosa kukubaliana. Namwambia nampenda, naye asema haamini nampenda. Kwa hivyo basi—kwa hivyo basi hakika sisi hukosa kukubaliana, lakini nakwambia, tunaendelea vema.

70 Sasa tazama Labda simwonyeshi dalili za kutosha ambazo zingekuwa. . .Niko nje nikihubiri, ndipo niingie nyumbani na kuchukua ndwano niende kuvua samaki. Ona? Lakini humo ndani moyoni mwangu nampenda; yanipasa tu nikae mbali naye, hivyo tu.

71 Sasa, tazama katika hili. . .Sasa, tusipokubaliana, ni sawa; lakini mwaona, maji hayaondoi dhambi; ni jibu la dhamiri safi.

72 Sasa, naamini ilimpasa Paulo abatizwe pale, kwa sababu imeamriwa na ni muhimu katika Biblia kuwa tumebatizwa. Kwa sababu narudia hili basi; yule mwizi alipokuwa ameangikwa msalabani. . .Naye alikufa bila kubatizwa kwa vyo vyote vile, bali alipata ahadi kuwa Yesu angekuwa pamoja naye Paradiso siku hiyo—Paradiso, si katika nchi ya waliopotea, kwa sababu huu ulikuwa wakati wa kwanza nafasi ilitolewa kwake.

73 Nami naamini hali ile ile ilikuwa kwa ile mioyo kwenye nyumba ya Kornelio walipopokea Neno la Mungu kwa furaha. Na Roho Mtakatifu ni Neno hilo likiwa hai, na lilikuwa limehuishwa kwao. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu alianza kunena kwa lugha nyingine na kutoa unabii. Ilikuwa ni katika mioyo mipokevu ya watu ambayo Neno liliangukia, walipoona yote ya kimbinguni.

74 Hilo ndilo linishangazalo mimi siku hizi katika hii saa tunayoishi. Baada ya kundi hilo la Warumi kuwa—na Wayunani, kama walivyokuwa, baada ya kuona tu dhihirisho la ono likithibitishwa, Roho Mtakatifu aliwatia hofu sana hata Petro alipokuwa akinena maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia. Ona?

75 Kama tu. . .Ona, Kornelio alisema, “Nenda kamwite. . .” Yeye alikuwa *centurion* (akida) na hilo latoka kwa “*century*” ambayo ni mia. Yeye alikuwa akisimamia watu mia. Yeye alikuwa akida wa Kirumi; naye—yeye alikuwa ameona ono alipokuwa akiomba, na Malaika akamjia. Yeye alikuwa mtu mzuri. Yeye alisema, “Nenda zako kule Yafa. Mtu mmoja Simoni, mtengenezaji wa ngozi, na kunaye mtu anayeitwa Simoni Petro. Yeye ako kule juu. . . utamkuta pale, naye atakuja kuwaambia Neno.”

76 Vema, yeye alidhani ono lile lilikuwa halisi sana. “Haiwezekani nilikuwa nimelala; nilikuwa namtazama Malaika moja kwa—kwa moja.” Kwa hivyo yeye aliwatuma kule baadhi ya askari wake waaminifu sana.

77 Na alipokuwa kule, Mungu alikuwa akimtayarisha mtume upande ule mwingine. Kisha akasema, “Sasa, amka.” Yeye kasema. . .Kwa kuwa yeye alikuwa juu darini akimngoja yule—

Bi. Simoni aanda chakula cha kutwa. Na alipokuwa juu pale . . . Yeye alikuwa anaona njaa, labda kwa kutembea, yule mtume alikuwa vile, kupitia kwa—jangwani Na—naye alikuwa amelala pale juu ya nyumba kabla chakula cha kutwa, juu darini, kama ilivyokuwa desturi. Bado wanafanya vivyo hivyo, wanalala juu darini, nao hupandia kwa ngazi na wakati mwingine vipandio na vinginevyo, kushuka toka juu darini—waliketi pale wakati wa jua kupungua.

⁷⁸ Lakini mtume yule alilala, basi alipokuwa akilala, yeye akalala sana na kuingia katika njozi; na ndipo yeye aliona shuka ikishuka huku imejaa vitu vichafu na kadhalika, naye alisikia Sauti ikisema, “Ondoka, uchinje ule.”

Yeye alisema, “Hasha, Bwana, sijakula kamwe kitu kilicho kichafu.”

⁷⁹ Sasa, ona, ndilo hilo ono. Sasa, tazama! Hilo yapasa lifasiriwe. Sasa, hilo laonekana kama Petro anaenda kuwinda na alikuwa yuaenda kupata aina fulani ya mnyama ambaye hangemla kamwe hapo kabla na ajaribu kumla. Yeye alisema, “Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu.”

⁸⁰ Yeye alisema, “Vilivyotakaswa na Mungu usiviite—kichafu nilichotakasa.” Kasema, “Amka, kuna watu wanaokungoja mlangoni. Nenda, usitilie cho chote shaka.” Wakati ule ule wao walikuwa wakibisha mlango. [Ndugu Branham abisha jukwaani—Mh.]

⁸¹ Sasa, waona? Basi alipomkuta mtu huyu hapa, hawa askari waaminifu, kulingana tu na ono lile . . . Na hapa wanarudi na mtu yule yule ambaye Mungu alikuwa amesema katika ono—mtu asiyejulikana, mvuvi mdogo tu asiyejulikana. Lakini kati ya hilo kundi ndogo, ilikuwa muhimu sana kwamba yeye alikutana na huyu mvuvi. Huyu juu hapa akiingia nyumbani sasa, mahali pale pale ambapo yeye aliona ono. Kornelio aliwakusanya watu wote pamoja na kusema, “Naam, iko tu kama nilivyoiona.” Na ndipo Petro akasimama akaanza kunena jinsi wangempokea Roho Mtakatifu, na alipokuwa akinena . . . ! Walikuwa wameona kila kitu kikiwa kikamilifu kabisa katika taratibu ya ono moja. Kundi la watu waliokuwa Mataifa, walioona ono moja likidhihirishwa, nao walisikia Neno la Kweli jinsi wangepokea Uzima; na Roho Mtakatifu aliwashukia hata kabla hawajapata kubatizwa.

⁸² Hilo lapaswa lifanyeje kwa maskani haya asubuhi hii? Wagonjwa, wanaougua, vipofu, viziwi, bubu, wa—wenye dhambi, kila kitu . . . Hebu fikiria, kati ya makumi elfu ya mambo, hata moja halijakosa kutimia kwa yodi moja wakati wo wote kamwe! Naam, haina budi kuwasha mioyo yetu!

⁸³ Naam, sasa, yeye basi, alipokuwa akinena maneno haya, Roho Mtakatifu aliwashukia. Ndipo Petro alisema, “Je, twaweza

kukataza maji, kwa kuwa hawa wamepokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi juu pale. Naamini dhambi zao zilikuwa zimekwisha samehewa, kwa maana Roho Mtakatifu hangeingia ndani; na Yeye hangeingia ndani isipokuwa tu kuwe chombo kilichochaguliwa tangu awali.” Yeye alijua kuwa wangepuata. Alijua. . .

⁸⁴ Naamini Paulo, kusudi la kubatizwa tena ni, yeye alikuwa amewatesa Wakristo. Naam. Naye—Mungu alijua, kwa sababu Yeye alisema, “Nimemchagua,” Yeye alimwambia Anania, yule nabii. Yeye alipotambua Sauli alikuwa chini pale chumbani, uso mweusi na macho meusi, na alikuwa a—ameomba sana na amejaa vumbi mwilini kote, na alikuwa amepofushwa na ile Nguzo ya Moto iliyomtokea barabarani; naye alisema, “Nimemchagua awe chombo kiteule kwa Mataifa.” Mungu alijua kuwa Anania angeweza kumbatiza katika Jina la Yesu Kristo katika ule Mto Dameski siku tatu baadaye. Lakini naamini dhambi zake zilikuwa zimekwisha ondolewa, lakini yeye alipaswa afanye hili kuonyesha ulimwengu. Nami naamini kuwa hiyo ndiyo sababu inatubidi tubatizwe katika Jina la Yesu Kristo. Naamini uzao uliochaguliwa tangu awali utalionna, na hao tu ndio watakaoliona.

⁸⁵ Sasa, ndugu wa imani ya utatu, siwatupii ninyi hili, ndugu zangu wapendwa, ninajibu tu maswali. Natoa tu mawazo yangu dhahiri juu yake. Kanda hii huenda wakati mmoja ikafika Afrika. Naamini kuwa tuko katika vivuli vya kuja Kwake. Sisi sote twaamini hilo.

Nina marafiki wapendwa, kina Du Plessis na Schoemans, na wengine wote, Yeager, na hao ndugu wema katika—katika Afrika kusini. Lakini kila wakati kuna mtu fulani anayejitokeza waziwazi tu katika maisha ya mtu. Na miongoni mwa watu wote ambao—nami nawapenda wao vema tu kama nimpendavyo ndugu huyu, nampenda sana, lakini Ndugu Jackson na mke wake alijitokeza nje maishani mwangu. Singelifahamu; yeye—yeye alijitokeza nje. Sasa, kuna Justice Duplessis, rafiki mpendwa, na ee, wengi sana wa hao ndugu wapendwa, wapendwa Wa-Afrikana na kina dada.

⁸⁶ Vema, mbona Ndugu Jackson na mke wake walijitokeza kwangu? Kwa sababu yeye alikuwa mwindaji? Hasha! Kwa sababu nina marafiki wengi wazuri wawindaji chini kule. Lakini mbona yeye alijitokeza? Ni sababu gani? Laiti ungelijua tu siri iliyoongoza hili lote. Lakini siwaambii watu siri zote ninazojua. Vema, kwa nini ilikuwa wakati ule ule ambayo Bwana alisema, “Wasiliana na Sidney Jackson katika Africa Kusini,” ndipo Bwana akamwambia Sidney aje hapa? Baada ya juma moja akabatizwa, yeye pamoja na mke wake, katika Jina la Yesu Kristo, papa hapa katika uvuli wa wakati. Ona, alichaguliwa tangu awali kwa kusudi hilo. Ona?

⁸⁷ Sasa, naamini kuwa ana—una—unaokoka kwa kumkubali Yesu Kristo. Na ubatizo ni ishara ya nje kuonyesha kuwa kitu fulani ndani kimetendeka, kwa sababu maji hayana nguvu, ni dalili tu. Nami naamini kuwa unaokolewa unapo . . .

⁸⁸ Sasa, kunao watu wengi (hebu ninyoshe hili kwa ajili ya ndugu) . . . Kunao watu wengi ambao—husema wameokoka; wengi wamebatizwa katika Jina la Yesu; wengi hunena kwa lugha, na wana kila namna ya ishara za Roho Mtakatifu, na bado hata hawajaokoka. Naam. “Wengi watanijia siku hiyo na kusema, ‘Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako?’—mhubiri—na kwa Jina Lako kutoa pepo, kufanya miujiza mingi.” Ndipo atawaambia, “Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu; sikuwajua ninyi kamwe.” Ona? Kwa hivyo mambo hayo yote, bali ni—ni—ni Mungu; yako mkononi Mwake. Lakini nionapo hayo . . .

⁸⁹ Unasema, “Vema, basi, mbona waita watu wabatizwe tena?” Ni kwa sababu nafuata mfano wa mwanzoni. Hatuwezi kupoteza hiyo ramani.

⁹⁰ Sasa, tunamchukua mtume Paulo yeye alipokutana na wanafunzi kadha ambao walikuwa watu wa ajabu. Naamini walikuwa wameokolewa, na hali wao hawakuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, ijapokuwa wao walikuwa wamebatizwa (Matendo 19). Paulo akipitia nchi za juu za Efeso; akakutana na wanafunzi kadha. Naye akawauliza, “Je, mlimpokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Nao wakamwambia, “Hatujui habari za Roho Mtakatifu, kwamba kuna Roho Mtakatifu.”

Yeye akasema, “Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?”

Wao walisema, “Tumebatizwa. Yohana alitubatiza sisi, mtu yule yule aliyembatiza Yesu.” Huo ni ubatizo mzuri sana.

⁹¹ Mtazame huyu mtume mkali hata hivyo. Yeye alisema, “Lakini Yohana alibatiza tu ubatizo wa toba,” si kwa ajili ya ondoleo la dhambi, kwa sababu ile Dhabihu haikuwa imeuawa, kubatiza kwayo . . . Nao waliposikia haya, walibatizwa tena kwa Jina Lake Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu kawashukia.

⁹² Sasa, hili lilifanyaje? Lilionyesha kuwa watu hawa waliochaguliwa Uzima, mara tu walipoona Kweli ya Maandiko, walienenda katika Kweli ile na kupokea thawabu ya mwamini; Roho Mtakatifu aliwashukia, nao wakanena kwa lugha, na kutoa unabii, wakimwadhimisha Mungu. Mwalifahamu sasa? Ona? Walifanya hilo baada ya wao kuwa na furaha kuu, shangwe, na kumtukua Mungu.

⁹³ Katika Biblia wao walikuwa na mhubiri Mbaptisti juu pale; yeye pia alikuwa amebatizwa. Lakini yeye alikuwa, na yeye alikuwa alithibitisha na—alithibitisha kwa Biblia kuwa Yesu alikuwa Kristo. Na watu hao walikuwa na furaha kuu, na—nao

walikuwa na furaha tele juu ya hiyo; nao bado hawakuwa na Roho Mtakatifu! Iliwabidi wabatizwe tena. Na Paulo alisema katika Wagalatia 1:8, “Malaika akitoka Mbinguni akawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na aiaaniwe.” Sijali ingekuwaje.

⁹⁴ Kwa hivyo, tukijua mambo hayo . . . Labda hamyajui, ndugu zangu; lakini tukijua mambo haya, basi nalazimika na nina wajibu kwa Mungu kutekeleza mpango huu wa ule msingi wa kwanza, kwa sababu hakuna mtu mwingine awezaye kuweka msingi mwingine kuliko ule uliokwisha kuwekwa; huo ni mitume na manabii. Manabii waliyatabiri, nao mitume wakayatimiza; na tunahitajika kuendelea kuuendeleza hata hilo jengo litakapomalizika.

⁹⁵ Sasa, naamini basi, kuwa mtu anaokolewa anapomwamini Bwana Yesu Kristo kwa moyo wake wote, na katika moyo wake, si katika dhamira yake ya nje sasa . . .

⁹⁶ Ona, wewe u—wewe ni mtu mara mbili—watu watatu katika mmoja, nafsi, mwili, na roho. Sasa, naamini hisi zako za nje, nafsi—nafsi yako toka kwa—si nafsi yako, lakini dhamiri zako za nje, hisi zako. . . Unapoamka, kwa maneno mengine, una—unasimamiwa na zile hisi tano: kuona, kuonja, kugusa, kunusia, na kusikia. Hizo zilitolewa tu kuwasiliana na makao yako ya dunia hii; nazo ni—hazikutolewa kwako kuwasiliana na makao yako ya kimbinguni. Hakika kuna hisi sita katika mwili wa mwanadamu, kwa sababu yeye ni nambari sita katika Biblia. Yeye aliumbwa siku ya sita, na yeye yu nambari sita—mwanadamu yu hivyo. Naye ana kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia, na imani. Imani yake yaonyesha mwisho wake, anakoelekea.

⁹⁷ Sasa, imani ni hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo usiyoyaona, hauyaonji, hauyagusi, hauyahusi, wala kuyasikia. Lakini kwa imani, yeye ashikapo Neno, huingizwa katika kiwango (ona?) kinachoyafanya halisi sana kwake, hata huwa tu kama yu nayo mkononi mwake. Yeye ajua yatatendeka.

⁹⁸ Sasa, kuna mambo yale yale kwenye swali hili hapa kuhusu ubatizo wa maji. Ona? Mungu alijua kuwa watu hawa watabatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na Paulo, yeye alitoa matamshi kuwa hakuna mtu, hata Malaika toka Mbinguni, apaswaye kufundisha fundisho lingine lo lote isipokuwa yale yeye alikuwa amefundishwa; kwa hivyo, nikija kama mhubiri, kama mhudumu, kama nabii, au ye yote yule, au hata Malaika akishuka, na angefundisha jambo lingine kinyume cha yale mtume huyu alifundisha, na sikuwaamuru watu wabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo, ningalipatwa na Biblia kuwa ni shahidi wa uongo kwa jambo ninalodai kuliamini.

⁹⁹ Kwa hivyo naamini kuwa mfano umekwisha wekwa. Kila mtu katika Biblia alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo. Hakuna

wakati hata mmoja ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ona? Hakuna ye yote aliyepata kunyunyuziwa maji; wao wote walizikwa majini.

¹⁰⁰ Kwa hivyo naamini kuwa hakika una... Kwa swali lako, ndugu mpendwa, naamini kuwa Mungu anapojua moyo wako... Kutakuwa na maelfu pale waliobatizwa kwa Jina la Yesu. Unaingia tu ndani mwenye dhambi aliyekauka na kuondoka aliyelowa. Ona, Ona? Lakini kama mwamini halisi wa kweli, ambaye yakupasa uenende katika imani yote na dhamiri njema kwa Mungu, unapoliona, unabatizwa! Lakini naamini kuwa ni dalili tu ya nje kuonyesha ya kwamba kazi ya ndani ya neema imetendeka.

¹⁰¹ Vivyo hivyo kama vile Mungu alivyojenga safina. Kasema, “Nuhu, ingia ndani, wewe na jamaa yako na nyumba yako.” Nao wakiingia. Sasa, naamini kama hapangukwako na safina pale, Mungu angemruhusu Nuhu aketi juu ya gogo au atembea juu ya maji. Ona? Lakini alimtengenezea safina kusudi aingie, na hivyo ndivyo ilipasa kutenda; hiyo ilikuwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Naamini Mungu humwokoia mtu kwa neema. Katika Jina Yesu Kristo kwa wonyesho wa nje ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu ya kuingia humo, kwa kuwa wote walibatizwa hivyo.

¹⁰² Siwalaumu watu wengine, lakini hilo tu ni... Nadhani hivyo ndivyo ilivyokuwa. Maji hayamwokoi mtu, yaonyesha tu kuwa yeye ameokolewa; ni ishara ya nje. Sasa, hilo huenda lisiwe sahihi, ndugu. Kama sivyo, basi, tatalipata wakati mwingine au... vema.

242. Katika Mwanzo 6:4 baada ya gharika, wanefili wale walitoka wapi?

¹⁰³ Hilo ni zuri, nzuri sana. Hilo ni swali la busara. Wanefili wale walitoka wapi? Adamu hakuwa mnefili tujuavyo sisi, kwa sababu kama ingekuwa vile Biblia ingelisema hivyo. Yeye alikuwa tu mtu wa kawaida. Wao walitoka wapi? Sasa—sasa, huu ni ubishi mkuu, na hili nilipewa tu. Liko kwa karatasi kubwa, nyeusi, na liko—au herufi kubwa nyeusi kwenye karatasi nyeupe.

¹⁰⁴ Sasa, wanefili hawa... Naamini ilikuwa mtu—mtu fulani hapa si muda mrefu uliopita... Huenda alikuwa Josephus. Si—sisemi hayo sasa, ndugu wahudumu, kuwa ilikuwa Josephus. Lakini naona kama huenda ilikuwa yeye, au Dk. Scofield, au baadhi yao, waliosema kuwa wanefili hawa waliokuwa nchini walikuwa roho walioanguka wa Mungu waliosikiza hadithi za—za Shetani, alizosimulia kule—kote Mbinguni... Na ilikuwa Mikaeli... Akijaribu vita na Mikaeli Mbinguni... alifukuzwa... Ambapo hawa wana wa Mungu waliona binti za watu, na ya kuwa hawa wanefili walikuwa nchini wakati huo, ambao hao walijiingiza wenyewe katika miili wa kibinadamu. Ukifanya hivyo unamfanya Shetani mwumbaji. Huwezi kufanya hilo.

¹⁰⁵ Pia kama asemavyo Dk. Smith, wa Seventh Day Adventist kuhusu mbuzi aliyetolewa sadaka. Yeye alisema mbuzi mmoja alikuwa... Waliua mbuzi wawili—kwenye siku ya kutoa sadaka—siku ya Upatanisho, na mbuzi mmoja aliuawa na mwingine akaachiliwa. Kisha yeye alisema mbuzi aliyeuawa aliwakilisha Yesu, mchukua dhambi zetu aliyekufa; lakini mbuzi aliyeachiliwa aliwakilisha Shetani, anayechukua dhambi zetu na kuingia katika milele nazo. Sasa, mwaona, lo lote... Nionavyo mimi... Kama hili litawahi kumfikia ndugu M-Adventist, sisemi lo lote kuhusu huyo mtu mashuhuri, Dk. Smith. Ee, yeye alikuwa Mkristo mwerevu, mwenye busara na mtu mwema, mvungwana, mwamini; lakini kwangu, mwaona, halina busara. Ufanyapo hivyo, unamtolea sadaka Shetani basi. Wote wawili waliwakilisha kifo cha Kristo, kuzikwa, na kufufuka. Yeye pia alikufa kwa ajili ya dhambi zetu na kuondolea mbali dhambi zetu; wote wawili walikuwa Kristo.

¹⁰⁶ Kwa hivyo wanefili hawakuja kamwe kwa kujiingiza wenyewe ndani. Wanefili walikuwa wana wa Kaini, ambao baba yao alikuwa nyoka, aliyeonekana kwa kila hali hasa kama mwanadamu, lakini alikuwa mtu mkuu, mtu mkubwa sana, mkubwa kuliko mwanadamu. Na hapo ndipo wana wale walitokea, kwa sababu walikuwa wana wa Kaini, kwa sababu walikuwa Wakanani katika nchi ya Kanani, ambako walitokea; na huko ndiko Kaini alikoenda. Na hiyo ilikuwa... Ona, hilo pia lathibitisha ule uzao wa nyoka. Ulikuwa ukoo tofauti kabisa wa watu. Huo ulikuwa uzao wa nyoka. Ona?

¹⁰⁷ Sasa, hilo—hilo swali la uzao wa nyoka limo humu ndani, kwa hivyo tuna—tutalifikia, nami nawatakeni kukumbuka hili. Ona? Sasa, hili litaweka msingi huu.

¹⁰⁸ Ona, walikuwa—walikuwa Wakanani, hawa wanefili; nao walikuwa wana wa Kaini, aliyekuwa mwana wa nyoka. Naye nyoka alikuwa mtu mkubwa, jitu la mtu, si mnyama atambaaye kwa vyo vyote vile, mrembo. Yeye alikuwa mjanja kuliko wanyama wote wa makondeni. Naye alikuwa ndiye... .

¹⁰⁹ Ona, mbegu za—za mnyama katika mwanamke hazitazaa kwa vyo vyote vile. Wamejaribu tena na tena; haina uhai kwa shahawa ya mwanamke. Na sasa, hawawezi kulipata. Chukua Sokwe, ni mnyama aliye karibu sana na mwanadamu wawezaye kumpata, au nyani, au baadhi ya hao walio karibu na mwanadamu. Kama Mungu katika mageuzi yake makuu yanayoendelea alianza kuumba samaki; na ndipo Yeye akaumba ndege; kisha Yeye akaumba vitu hivi vingine, wanyama, na vikaendelea kuwa bora, hadi moja ikafikia sokwe na kima, na kuendelea hadi kufikia sokwe, halafu ikafikia mfano wa nyoka, kisha toka kwa nyoka yule hadi kwa mwanadamu.

¹¹⁰ Na mwanadamu amejaribu kuchunguza, sayansi, imejaribu kupata mifupa, jinsi huyu mnyama alivyokuwa aliyemfuatia

mwanadamu. Na mwanadamu ni mnyama. Mwanadamu, upande wa mwili ni mwili wa mnyama; tunajua hilo. Sisi tu wanyama wazaa na kunyonyesha, ambao ni wanyama wenye joto jingi; twajua hilo! Lakini tofauti ni nini? Mnyama hana ile nafsi ya ndani. Lakini mwanadamu anayo. Yeye hajui mema kwa mabaya.

¹¹¹ Mbwa mdogo jike hajui inampasa kuvalia nguo, nami siamini angalivalia suruali kama yeye alikuwa—alifahamu. Wala na nguruwe jike, lakini ni uzao ulioanguka wa mwanadamu. Ona?

¹¹² Sasa, hapo—hapo ndipo inatokea. Hapo ndipo wanefili hao walitokea. Walikuwa wana wa nyoka.

¹¹³ Basi ona, yeye alipoona Hawa katika hali hii, yeye—Shetani alimpata na kumfanya a- . . . Ona, Adamu alikuwa bado hajawahi kugundua. Si—sijui jinsi ya kutumia maneno hayo. Ingekuwa sawa hapa kwenu nyote, lakini mtu fulani hupinga sana. Mwajua, kila mara wanajaribu kupata kitu fulani. Lakini ona, Adamu hakuwa amemjua Hawa kamwe, mke wake. Yeye hakuwa amefikia mahali pale, na Shetani akafika pale mbele yake. Ona? Basi yeye alipopata mimba, ndipo Adamu akamjua. Tutafikia hayo kwa hili swali linalofuata au mojawapo wa maswali haya. Sijui liko wapi; sisi—nililiona tu humu. Sasa, lakini hapo ndipo wanefili walitoka.

243. Mpendwa Ndugu Branham, je, wana na binti zote za waamini wa kweli waliozaliwa mara ya pili wataokoka?

¹¹⁴ La, ndugu; la, hakika hawataokoka. Ona, kama ni—kama nilivyomnukuu David DuPlessis kwa msemo huu, “Mungu hana wajukuu” (ona?), ana wana wa kiume na wa kike tu. Ona, watazaliwa tu hasa kama baba zao na mama walivyozaliwa kwa Roho. Ona? Hilo ndilo limfanyalo mtu mtu mpya, ni kwa sababu yeye amezaliwa tena, amezaliwa upya. Kuzaliwa kwake kwa kwanza humleta duniani kama mtu wa kawaida; kuzaliwa kwake kwa pili humfanya yeye mtu wa kiroho wa Mbinguni. Ona, Humgeuza, nafsi yake, si dhamiri yake, utu wake wa nje, fahamu zake; yeye bado hugusa, hunusa, huonja, na husikia; lakini sehemu zake za ndani, tamaa zake, kile kinachomchochea yeye, zimegeuzwa kwa Mungu. Ona?

¹¹⁵ Sasa, kumbuka, njia pekee ambayo hili lingetendeka ingekuwa hii, kama ilivyokuwa katika wakati wa yule akida wa Kirumi. Paulo aliwaambia Warumi, yeye na Sila, alipotaka kuchomoa upanga wake na kujiva, kwa sababu Mungu alikuwa ametikisa gereza hilo kwa tetemeko la nchi, yeye alisema, “Usijidhuru, kwa maana sisi sote tuko hapa. Amka!” Na alitaka kujua yale angefanya. Yeye alisema, “Ondoka ukabatizwe, ukaliite—Jina la Bwana, nawe na nyumba yako mtaokoka.” Ona? Kwa maneno mengine, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka, pamoja na nyumba yako.”

116 Vipi basi? Kama nyumba yako ikiamini vivyo hivyo unavyoamini. Ona? Omba na uweke watoto wako kwa Mungu na ushikilie kwa Mungu, ukiamini kuwa wao wataokoka.

117 Nimepitia katika matukio hayo na Rebeka wangu. Ona? Liweke tu kwa Mungu. Yeye alipokuwa wa umri wa “tineja,” naye alikuwa akitembea na msichana fulani tulipoenda mara ya kwanza kule, kuenda—akakimbilia nyumba ya msichana fulani kujifunza muziki. . . Na msichana huyu. . . Nilipitia pale siku moja, na hapa msichana huyu alikuwa ameketi kwenye kinanda akisakata rumba. Vema, hilo likanitoshia! Kwa hivyo nilimwambia asikaribie mahali pale. Ona? Ndiposa yeye alisema, “Vema, hapo ndipo mahali pekee ninapoenda kujifunza muziki.” (Mwajua jinsi “matineja” huwa).

118 Nami nilisema. . . Kila mtoto apaswa kupitia kwa hayo. Karibu kila mmoja apitia umri huo. Mliupitia; niliupitia. Nasi yatupasa kuwaza mawazo yao.

119 Kwa hivyo basi, siku chache baadaye mama yake alimkemea kwa jambo fulani, naye akamfanyia ujeuri. Sasa, huyo si Rebeka kwa vyo vyote vile. Akaondoka na kufunga mlango kwa kishindo, na karibu kuangusha vitu toka ukutani, akaenda shuleni.

120 Sasa, ilinipasa, labda, kuchukua mshipi wangu na kumfuata nje kule bustanini, na kumrudisha na kumcharaza mijeledi. Ona? Lakini niliwaza, “Ngoja kidogo, yanipasa kuwaza mawazo ya umri wa miaka kumi na minane.” Ona? “Sasa,” nilisema, “Mama, najua hilo. . .” Yeye alianza kulia, Meda. Nilisema, “Najua umefanya yote uwezayo kufanya; nimefanya yote niwezayo kufanya. Sasa, kama imetushinda sisi, yatupasa kuchukua hatua nyingine.”

121 Kama mwanamke mpendwa alivyoandika siku nyingine (liko kati ya mojawapo wa maswali haya hapa), kasema, “Ndugu Branham, wewe si Masihi, sivyo?”

Nilisema, “La, mama.”

Yeye alisema, “Twakuamini wewe kuwa mchungaji wetu, lakini wewe kila mara unatuelekeza kwa Mchungaji mkuu.”

Nilisema, “Naam: ndivyo hivyo.” Ona?

122 Nilisema, “Vema, tazama, Mpenzi, sasa, yakupasa unisikie mimi. Ni vigumu kwako kufanya hivyo; mimi ni mumeo. Lakini watu huja kwa motokaa kutoka nchini kote na majirani pia kwa ajili ya maneno machache ya wosia. Sasa kama una- . . . Niliongea naye hivi majuzi, naye akaniondokea tu akaenda.”

123 Sasa, Rebeka hakupata kunifanyia mimi hivyo. Ona? Na mama yake aliposema kitu fulani kulihusu, yeye alifunga mlango kwa kishindo na kusema, “Unanitarajia mimi kuketi hapa na kuwa ua la ukutani maishani mwangu mwote?” Kisha buum!

Akafunga mlango kwa kishindo na kutoka nje. Huyu alikuwa shetani.

124 Nakumbuka, miaka miwili ya kwanza ya maisha yake alilia. Tuliingia mkahawani kula; ningemtembea barabarani huku Meda anakula, na ndipo yeye angemtembea nikila. Alilia tu na kulia. Na siku moja kule Canada, alilia usiku wote, nami singepumzika na kadhalika; mimi nikisimama pale. . . Sasa. Na Kitu fulani kiliniambia, “Ni Shetani akiingilia huduma yako.”

125 Nilisema “Nipe mtoto huyo.” Nilisema, “Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, ondoa mikono yako kwake.” Yeye alikoma kulia papo hapo na hakulia tena kwamwe. Ndiye mtoto mtulivu zaidi niliye naye. Tangu saa iyo hiyo kulikwisha. Yakupasa uwe nayo. . . Yakupasa uwe nayo ndani yako haidhuru, kabla kulifanya!

Basi yeye alipo—basi hilo—yeye alianza hayo. Nami nilimzunguzia Meda karibu saa moja. Nilisema, “Meda, mwache.”

“Mimi? Huyu ni mtoto wangu.”

126 Nilisema, “Si ni wangu nami pia?” Vema. Nilisema, “Kama yeye alikuwa yuafa asubuhi hii, ingekupasa kumkabidhi kwa Mungu kwa ajili ya kituo chake cha milele. Mbona tusimkabidhi kwa Mungu sasa kwa ajili ya safari yake duniani?”

Naye alisema, “Vema, huyo ni mtoto wangu!”

Nilisema, “Ni wangu pia.”

Nilisema, “Sasa, waweza kuondoa. . .”

“Mimi nisimwambie lo lote?”

127 Nilisema, “Sikusema hayo kamwe. Tutaacha kumkaripia, tumpe wosia tu. Yeye ataka rafiki, nawe ndiwe unayepaswa kuwa rafiki yake, mimi na wewe. Sisi ni wazazi wake.”

128 Watoto hawa siku hizi wanahitaji rafiki. Kama wangukuwa na mama na baba ambao wangukaa nyumbani na kuwalea, badala ya nje hapa kwenye vyumba vya pombe wakikimbia usiku wote na mambo kama hayo, hatungekuwa—hatungekuwa na kichaa cha vijana. Ona?

129 Waliacha Biblia; wote walienda kanisani na kufanya mchezo wa karata na mengineyo na. . . Ona? Mnajaribu kuyalainisha kama uwanja wa Shetani kule Hollywood. Hungeweza kuleta Hollywood kanisani, yapasa ku—namaanisha kuleta kanisa katika Hollywood, yawapasa mlete Hollywood uwanjani mwenu. Ona? Si kwenda uwanjani mwao, waache hao waje hapa. Tuna kitu fulani ambacho hao hawajui lo lote kukihusu.

130 Kwa hivyo tulipiga magoti na kulikabidhi kwa Mungu. Nilisema, “Najua yeye ana umri wa miaka kumi na minane—atakuwa katika siku chache, naye—na msichana wa umri huo atawaza kuhusu marafiki wa kiume, na tumemfungia

ndani.” Nilisema, “Si—sikutaka kamwe kuona akiolewa. Nataka kumweka afisini hapa, afanye kazi. Nataka kumwona yeye amejazwa na Roho na—na—na aishi hivyo.”

Naye . . . Vema, sisi sote tulitaka hivyo. Yeye kasema, “Vema, hatuwezi kufanya hilo.” Kasema, “Yeye hatalisikiza.”

¹³¹ Nilisema, “Ngoja kidogo! Tumemlea vizuri tuwezavyo, sasa mweke mikononi mwa Mungu—mkabidhi yeye.” Nami nilisema, “Ndipo yeye afanyapo lo lote sema, ‘Rebeka, mpendwa, mama hakutaki ufanye hilo, lakini mimi ni rafiki yako; nitakaa nawe.’ Ona? Acha yeye ajue unampenda, Yeye atapata mtu fulani wa kumpenda, na huenda ni mwanamke mbaya.” Ona? Nilisema, “Wewe kuwa ndiye huyo mwanamke ampendaye.” Nilisema, “Mpenzi, hilo laonekana la kijinga, lakini watu hutoka kila mahali, na kuketi kwa mahojiano ya kibinafsi, na kadhalika.” Nilisema, “Mimi ni wa kawaida sana; sisi tumezoeana sana sisi kwa sisi, kwa sababu sisi ni mume na mke, lakini tusiache hilo litendeke. Yakupasa ukumbuke, hili ni katika Jina la Bwana!”

Kwa hivyo yeye alisema, “Vema.”

Tulipiga magoti na kulikabidhi Mungu. Kasema tumeliachilia hilo.

Adhuhuri hiyo yeye akaingia; naye kasema, “Vema, nadhani bado unasema siendi kule!”

¹³² Meda kasema, “La, sijasema lo lote kuhusu hilo.” Kasema, “Wajua mama hakutaki ufanye hivyo; na unajua lilikuwa karibu kumwua baba yako alipokusikia juu pale ukipiga huo muziki wa rumba, wo wote ule, na msichana huyo.” Kasema, “Sasa, yeye hakukutaka ufanye hivyo, nasi hatukutaki ufanye hivyo, Beka, lakini tuliyaachia hayo Bwana. Nataka wewe ujue tunakupenda. Cho chote ufanyacho, bado twakupenda.”

Yeye akapaza sauti, kasema, “Nitaenda haidhuru!”

Kasema, “Vema, mpendwa.” Kwa hivyo kaendelea. Kasema, “Vema, chakula cha jioni kitakuwa tayari urudipo.” Yeye hakuenda kamwe! La, hajaenda kamwe tangu wakati huo. Ona?

¹³³ Si muda mrefu baada ya hayo yeye alikutana na George; George ni Mkristo. Hilo—hilo likatosha.

¹³⁴ Yeye alikuwa anajaribu kumwambia Bi. Wood kuhusu hayo hivi majuzi. Yeye alisema, “Ee, nilikuwa jeuri mno.” Kasema, “Baba na mama waliniachia Bwana.” Kasema, “Jeuri mno.” Lakini huo—huo ulikuwa ujeuri mwingi kwetu; hatutaki kupata ujeuri zaidi. Ona? Hebu iendeele hivyo. Vema.

244. Ndugu Branham, wawazaje kuhusu . . . (Ee, enhee! Nakumbuka nilisoma hili. Sikuwa . . . Nilikuwa nililiweka hata baadaye, lakini nadhani yafaa nilisome. Mwandiko wa mwanamke fulani. Bila shaka anatoka Kentucky, kwa sababu yeye ana—tikiti ya Kosmo Portland Cement hapa).
Ndugu Branham, waonaje kuhusu dada wetu kanisani

kuvalia nguo fupi sana? Je, si hiyo inaharibu ushuhuda wetu na kuonyesha mfano mbaya kwa vijana wetu kanisani mwetu? Inaonekana k—a—...kuona vijana—kuona mwanamke mzima amevalia nguo fupi sana hata zinaonyesha magoti yake anapotembea.

¹³⁵ Ye yote uliye, Dada au Ndugu, ye yote uliye, nakubaliana na wewe mia kwa mia. Ni aibu, lakini niambie nitafanyeje kulihusu! Nalihubiri tu kwa nguvu nijuavyo jinsi ya kulihubiri; wanafanya vivyo hivyo. Kwa hivyo ni hukumu kwao, kwa sababu neno lilihubiriwa. Naam, hakika napinga nguo ndogo za kale zinazokaza na kuonyesha mwili uonekanavyo kama... Mara kwa mara huwakemea watoto wangu, Rebeka na Sara. Sijali ni wadogo jinsi gani, ni...hilo...Nawakemea wakati wote. Nadhani hata wao huvaa nguo zao...Meda humpeleka Rebeka kando kila siku kuhusu hilo. Ona? Huvalia hata... Watoto hakika, unaweza kutazamia hayo kwa watoto, na yakupasa uwasahihishe; lakini ifikiapo mwanamke, kuna kasoro pale. Ona?

¹³⁶ Sidhuru dhamiri sasa, ninajibu tu maswali. Uliniuliza kwa moyo wako; nakujibu kwa moyo wangu. Kama utapata suluhisho, mimi—tafadhali uje uniambie mimi, hakika nitalifanya, kama naweza kufanya lo lote kulihusu.

¹³⁷ Kama mtu fulani alivyosema hivi majuzi, yeye alisema, “Vema, nakwambia, Ndugu Branham,” kasema, “Nikwambie kile Adamu na Hawa...” Kasema, “Ilikuwa hakika; walikuwala tofaa!” Nami niliona waligeuza hilo sasa; walisema walikula nini? Naamini iliitwa *kitu fulani*? [Mtu fulani katika kusanyiko ajibu, “Embe dodo”—Mh.] Embe dodo, naam, ilikuwa ni embe dodo walilokula. Vema, wakati umefika wa kuwapa tena embe dodo kama itaweza kuwafanya wao watambue wako uchi. Ona?

245. Ndugu Branham, nimeupokea Ujumbe wa Mungu wa wakati huu, na pia mtoto wetu wa kiume. Nasi sote wawili tumebatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Mume wangu— mume wangu hajaupokea Ujumbe na anaupinga Ujumbe huu. Naye amemshawishi mtoto wetu na anampeleka kwa kanisa la Kimethodisti. Yeye anitaka niende naye kanisani wakati hatuna ibada hapa maskani. Je, ni sawa kwangu kuenda pamoja naye au ingekuwa heri kuwa nje ya dhehebu hilo?

¹³⁸ Vema sasa, Dada mpendwa... Yeye hakuandika jina lo lote, lakini labda unasikia swali lako; kama hausikizi, utalisikia kwenye kanda. Enda na mumeo, lakini usiwe mshiriki wa—wa yale wanayofanya. Ona, wapaswa kumpenda mumeo, na upendo ndio uwezao. Kolea kabisa, yeye atakuwa na kiu kama kuna cho chote ndani yake.

¹³⁹ Usijiunge na dhehebu lao. Ulisema, “Kukaa na dhehebu hilo.” Usijiunge nalo; enda kwalo. Kama huwezi kupata mkate

wote, pata nusu; kama huwezi kupata nusu, pata tu kipande chake. Ona, Ona? Lakini hiyo ndiyo njia ya kumvutia mumeo, kwa kufanya hivyo. Usiwe mwenye kiburi, ndipo yeye atajua ana kadiri tu wewe ulicho nacho. Ona? Lakini uonyeshapo kitu fulani ulicho nacho ambacho yeye hana, hilo litamfanya yeye awe na kiu ya kuwa kama wewe. Mke aliyetakasika humtakasa mumewe.

¹⁴⁰ Huo ulikuwa tu wosia. Kwa hivyo ni—ningechukua muda mwingi kwa hilo, lakini tunataka tu kumaliza mengi tuwezavyo, kwa sababu naona nina karibu dakika ishirini na mbili basi. Vema.

246. Ndugu Branham, naamini Ujumbe huu unaofundisha kwa moyo wangu wote. Unachangamsha nafsi yangu; ingawaje, mke wangu na mwanangu hawafurahii Neno. Hawataki kujitenga wenyewe na baadhi ya tabia zao za kilimwengu. Ulisema kuwa yatupasa tudai jamaa yetu—tudai jamaa yetu. Naona hilo ni gumu kufanya, kwa sababu hawaishi kwa Neno au katika Neno. Nifanyeje, bwana? Je, niwadai na kuamini, au niombe, “Baba, mapenzi Yako yetendeke, “na niridhike katika hali nijikutayo mwenyewe ndani yake? Ningefurahia uongozi wako, Ndugu Branham.

¹⁴¹ Mungu akubaribi, Ndugu yangu au Dada, ye yote yule. Ni—ningewakabidhi wao kwa Bwana. Ni . . . Ona, kwa sababu, “Wale alionipa Baba yangu watanjia mimi.” Ona? Sasa, jambo pekee kwako kufanya . . .

¹⁴² Ilifanya moyo wangu ufurike kwa furaha majuzi nikienda huku na huko kuona hawa watu wa hoteli za barabarani . . . Nilishuka kwenda kumwona Bw. Becker. Yeye alisema, “Billy, wajuaje? Nalisha makutano yako yote Jumapili”—hali Blue Boar hulisha mia tatu kila Jumapili! Ona? Nami nilienda hapa nje pamoja na mtu huyu hapa juu, hapa, huyu mwungwana hapa juu katika—katika Ranch House, mtu mzuri sana . . .

Nilikutana naye; yeye alisema—nilisema, “Vema, hilo lilikuwa jema kabisa.” Nilisema, “Nafurahia kwamba uliuondoa upuzi huo wote pale—kule kutenda yasiyofaa.”

Yeye alisema, “Naam, bwana, Ndugu Branham.”

Nilisema, “Yeye alinijuaaje?” Ona? Nilisema, “Ulinijuaaje?”

Yeye alisema, “Nakujua.” Kasema, “Nalisha makutano yako yote hapa kila Jumapili kwa . . . Vema,” yeye alisema, “nami nataka kukwambia jambo fulani; ni watu wazuri. Ni watu wazuri!”

¹⁴³ Sasa ona, hilo lilinifanya nijisikie vizuri. Ninyi watoto wangu. Ona? Ninapooni watoto wangu wakitenda mema na kuwa wazuri, hilo lamfanya baba ajisikie vizuri sana. Ona? Kwa hivyo mwafahamu.

144 Naam, sasa, mama, wakati . . . Dada yangu, kama mume wako akutaka uende kwa kanisa Methodisti, enda. Huenda usipate mkate mzima, lakini kama hata wanasema wanaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, unaamini hilo, kwa sababu hata nasi twaamini hivyo pia. Sasa, kama wataenda kando kwa hamaki na mengineyo, a—acha tu waendeleo, lakini ule tu mkate kiasi kile. Ona? Hapo, unaonyesha tu kwa utamu wa maisha yako na kuchukuliana na wengine . . . Na kama hujalipata, Dada mpendwa, omba hata ikujie, kusudi usije ukaiga cho chote, kwa sababu ufanyapo hilo, si halisi. Mume wako aweza kung'amua hilo. Lakini una—wakati tayari umeomba hata ambapo maisha yako yamejaa chumvi ya Mwokozi, itagusa. “Nami nikiinuliwa juu, nitawavuta wote Kwangu.” Ningeenda; jihadhari sana. Usijiunge na kanisa lao hata hivyo! Tafadhali usifanye hivyo; usijiunge na kanisa lao, lakini endelea!

247. Ndugu Branham, hapa kuna swali ambalo limekuwa likiwatatiza baadhi yetu hapa. Mojawalo—kwenye—kwenye (kunradhi)—kwenye kanda zingine unaongea kuhusu kuokolewa kwa Wayahudi peke yao baada ya Bibi-arusi kunyakuliwa. (Na yamechorwa mstari) Tafadhali eleza kamili kuhusu Mataifa ambao hawatashiriki katika kunyakuliwa. Nilidhani ulisema kwamba Mataifa waliosalia walipitia kwenye ile dhiki na kutoa uhai wao kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu. Yeye anaporudi toka kwa Mataifa kuwaendea Wayahudi—Yeye anapowaachilia Mataifa na kuwaendea Wayahudi, ndipo hakuna nafasi yo yote kwa Mataifa kuokolewa, ni Mataifa waliokwisha okolewa peke yao, lakini hawajapokea ile Kweli ya siku zao za mwisho watakaopitia katika ule wakati wa dhiki ndiposa waokolewe mwishoni. Sivyo? Tafadhali eleza, kwa sababu ulisema kuwa kutakuwa na wachache tu watakaonyakuliwa. Itakuwaje kwa watu wanaomwamini Bwana—wanamwamini Bwana sasa nao—na hawaamini vile unavyohubiri Ujumbe huu wa siku za mwisho? Je, wataokolewa? Na dada yule amelilandika jina lake.

145 Sasa, swali nzuri sana. Sasa, kwanza, tatanisho ni, ni yale nimesema kuhusu siku za Mataifa kukamilika wakati ile dhiki—katika ile dhiki iliyo kuu. Sasa, sioni Mataifa katika Biblia . . . Bibi-arusi wa Mataifa, si kanisa la Mataifa sasa, kanisa la Mataifa litapitia katika ule wakati wa dhiki iliyo kuu (ona?), lakini si . . . Ona, yule Bibi-arusi ni hao walio Wateule; Hawapitii kwa lo lote lile ila kule kunyakuliwa. Wao watageuzwa tu na kuondolewa ulimwenguni. Ona? Sasa, nitaeleza hayo katika swali lingine mbele hapa, nikilileta toka kwa Luther na kuendelea; na mtaona basi yamaanisha nini; ni kukomaa kwa ule mwili. Ona?

146 Sasa tazama. Sasa, Wayahudi waliosalia ndilo watakaohubiriwa na wale manabii wawili, Eliya na Musa.

147 Sasa, hili ni wazo langu, ndugu wahudumu, katika njia yangu mwenyewe nionayo Roho Mtakatifu amenifunulia.

148 Sasa, jambo linalofuata ni Uyahudi—au Bibi-arusi mtaifa aliyeteuliwa kutwaliwa pamoja na Bibi-arusi wa Mataifa aliyeteuliwa ambaye amekuwako katika nyakati zote—kunyakuliwa hata katika uwepo wa Kristo Mbinguni. Wafu wanafufuliwa; wale ambao wako hai na waliosalia wanabadilishwa, nao watanyakuliwa pamoja nao hewani kumlaki Bwana. Ndipo, kwa sababu. . .

149 Baada ya sherehe za Arusi Utukufuni, Yesu—baada ya hao kunyakuliwa hewani, Yesu atarudi duniani na kujitambulisha Mwenyewe kwa watu Wake, katika mfano kama Yusufu alivyojitambulisha mwenyewe kwa ndugu zake. Na mke wake, hakuna Mtaifa aliyekuwako, hakukuwa mtu ila Yusufu pekee, yeye alipojitambulisha mwenyewe kwa ndugu zake. Nyote mwafahamu hilo sasa?

150 Yeye alituma. . .Hata mke wake alikuwa katika jumba la enzi, mfano kuwa Bibi-arusi atakuwa katika jumba la enzi Utukufuni wakati huo. Ndipo Yesu ajijulisha Mwenyewe kwa Wayahudi (ona?) baada ya sherehe za Arusi, ile miaka tatu na nusu, na—na taabu yake Yakobo, hiyo miaka tatu na nusu, ule mwisho wa juma la sabini la Danieli. Masihi atakatiliwa mbali katikati ya. . .Na Yeye alifanya unabii kwa miaka tatu na nusu na akakatiliwa mbali. Ndipo kuna miaka tatu na nusu iliyosalia kwa manabii, Musa na Eliya, kisha mwishoni mwa siku yao ya sabini kama ilivyokusudiwa kwa watu wale, kama Danieli alivyosema; ndipo mwishoni mwa hizo sabini, Yesu atajijulisha Mwenyewe kwao. Yeye na yule Mtawala ambaye apaswa kuwajia Wayahudi. Ona?

151 Sasa, ndiposa wakati huo. . .Ona, Bibi-arusi wa Mataifa yuko Mbinguni, na wale wanawali waliolala, mwanamwali Mtaifa, hawataokolewa katika wakati huo; yeye amekwisha okolewa, lakini amekataliwa katika yule Bibi-arusi. Naye apitia tu katika wakati wa ile dhiki kwa wakati wa utakaso, kwa sababu yeye amemkataa Kristo, yule Neno, kwa ajili ya utakaso Wake. Ndipo yeye apaswa kuteseka kwa ajili ya matendo yake, lakini yule Bibi-arusi ambaye ameshakuwa Neno, utakaso mkamilifu ulifanywa na Kristo, kwa sababu Yeye ni Neno. Mwili huo ulipasuliwa, na mwili huo ulipopasuliwa, Bibi-arusi alikuwa katika mwili huo, kwa sababu ni Neno lote! Amina! Mwalifahamu?

152 Yesu aliugua katika mwili huo, Yeye aliteseka. . .Kwa sababu mwanamume na mwanamke ni mtu mmoja. Hawa alitolewa toka kwa Adamu, na Kanisa. . .Ilitendekekaje? Mungu aliufungua ubavu wa—wa Adamu na kuondoa toka mle msaidizi, yule bibi-arusi. Na Mungu alifungua ubavu wa Yesu pale Kalvari na kutoa Bibi-arusi yule. Ona? Na Yesu alipokufa

pale Kalvari. . . Kumbuka, Bibi-arusi hakutolewa toka kwa mwili hata mwili ule ulipokuwa umekufa. Yeye alikuwa amekwisha kufa, nao walikuwa wakienda kuivunja miguu Yake. Na nabii yule alisema, “Hakutakuwa na mfupa hata mmoja utakaovunjwa.” Kwa hivyo waliinua nyundo juu kuvunja mguu, na mtu mwingine akaenda na mkuki na kuuingiza moyoni Mwake, na maji na damu vikatoka; Yeye alikuwa amekwisha kufa. Bibi-arusi alikuwa tayari amekombolewa katika mwili kwa kifo Chake, kwa hivyo hakuna tena kuteswa katika ule wakati wa dhiki kwa Bibi-arusi. Ona? Yeye ataingia. Lakini kanisa la mataifa linalomwamini Yeye tu, na kuchukua kanuni za imani za kidhehebu na kadhalika. . .

153 Na bado kama maskini mtu huyu alivyosema; “Mume wangu na mwanangu bado wanapenda vitu vya ulimwenguni na mambo kama hayo.” . . . Ona, bado hawajakubali huo ukombozi, kwa yale wafanyayo, hukuosha papo hapo. “Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi.” Hakuna tamaa, hakuna cho chote ndani yake kinachotamani mambo ya ulimwengu.

154 Yesu alisema, “Yeye aipendaye dunia (*Kosmos* sasa), wala mambo yaliyomo katika dunia, kupenda Mungu hata hakumo ndani yake.” Yeye hapendani na Bwana wake. Ona? Kwa hivyo, yeye apaswa kulipia adhabu hiyo, na si. . . Yeye hajaokoka katika wakati huo; yeye ameokoka sasa toka kwa mauti ya milele; lakini yeye atapaswa kupitia katika wakati wa ile dhiki kwa kutakaswa. Mwafahamu yale ninayokusudia? Naam, hilo—naamini hayo yametosha kwa swali hilo. Hebu tuone, kuna kitu kingine hapa.

155 “Tafadhali eleza, kwa sababu ulisema kuwa kungekuwa tu na wachache katika kunyakuliwa kule.” Hiyo ni hawa walio duniani watakaogeuzwa. Yesu alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, ila nao waionao ni wachache.”

156 “Itakuwaje kwa watu wanaomwamini Bwana sasa na hawa—na hawajui jinsi unavyohubiri?” Si lazima waamini hili. Si lazima waamini jinsi ninavyoyolihubiri. Ona? Si lazima waamini hayo. “ . . . Ujumbe wa siku za mwisho. Wataokoka?” Naam, wakimwamini Bwana. Ona? Na kama wao kama wanapinga na kusema, “Siamini Yeye ni Neno. Siamini kuwa hilo ni kweli. Siamini ubatizo wa Roho Mtakatifu,” hilo laonyesha ambapo wanaelekea, wakati wa ile dhiki. Lakini wale wawezao kukubali Neno katika utimilifu wake, si mimi nikilihubiri, kwa sababu ni Biblia inayosema hivyo. Wale wanaokubali hilo wako huru, kwa sababu wao—lile Neno limekwisha kuwahukumu.

157 Sasa, Hakimu wa haki aweza kumhukumu mtu mara mbili kwa jambo lo lote kama adhabu imelipwa? Kama nilikuwa katika duka la rehani, na uje na usema, “Nitamkomboa”; na uingie na kulipa dhamani kwa ajili ya ukombozi wangu (na hiyo ndiyo adhabu yangu ya kuwa katika duka lile la rehani), na

ulipie ukombozi wangu, basi dalali wa rehani awezaje kunidai mimi? Isipokuwa niujiuze tena. Naam. Nilipokataa Utimilifu wa Neno, ndipo narudi tena kwenye duka la rehani. Ona, ona? Ndipo nijitahidi kutoka, nikiweza. Lakini Yeye alinikomboa. Vema. Natumai kuwa hilo... Nina—nina mengi sana hapa nataka kupata haya ambayo... [Mwisho wa upande wa kwanza wa kanda. Sehemu ya pili yaanza bila sehemu ya swali—Mh]

248. ...huu ni mvuto wa tatu na ni kunena Neno. Yaonekana inawezekana kabisa kwako kunena Neno na mtu kurudishwa kabisa, awe amewekwa tayari kabisa kwa ajili ya kunyakuliwa katika ule ufufuo, yule Mwana wa Adamu. Ni kweli ama sivyo? Na ungefanya hili kama ungelishawishiwa vizuri. Je, haungeweza “kuokoka katika haya yote (lina n.k. pale)—kuokoka katika hayo yote na kusimama mbele za Mwana wa Adamu?” (Luka 21:36)

¹⁵⁸ Sasa, rafiki ya—yangu mpendwa. Ona? Sasa, nadhani hapa kuwa u—una—una—una matamshi mazuri. Naam, bwana! Naam, bwana! Sasa, hilo lingekuwa hivyo. Ulisema, “Ndugu Branham...” Katika Maneno mengine, haya ndiyo yale nina... Sidhani kuwa ni...naweza...naamini...Si kulainisha yale ulisema, lakini naamini naweza kuyaeleza dhahiri zaidi kidogo kwa watu. Ona? Mnaamini, kwa sababu ya Neno lililonenwa na mambo kama hayo ambayo Yeye alinena kuhusu. Na ninyi nyote mmeshuhudia wale kichakulo na mambo haya yote ambayo yamefanyika. Lakini mlitambua, hayo yalitolewa na Mwenyezi! Sikumwuliza, “Bwana, niruhusu nifanye hili, ninene mambo haya vile, nifanye mambo haya pale.” Sikumwuliza Yeye hayo kamwe. Yeye kwa mapenzi Yake Mwenyewe ya Kiungu alinjia na kusema, “Wewe nenda ukafanye *hivi*.” Ona? Sikuwa nikiomba cho chote. Musa hakupata kamwe kuomba aende Misri, lakini ilikuwa Mungu aliyemtuma kushuka kwenda Misri. Ona?

¹⁵⁹ Sasa, naamini kuwa Roho Mtakatifu angenjia mimi na kusema katika ono, “Nenda kamwambie fulani, mtu *fulani na fulani* hawako—wanajaribu kushinda jambo *fulani*, nao hawawezi kulishinda. (Na wanavuta sigara; wanakunywa pombe; wandanganya, wanaiba, au kufanya uzinzi, lo lote lile; au wana roho wa tamaa mbovu.) Na uende tu waliko na kusema, ‘Ewe roho, ondoka mle; namweka huru huyu aliyefungwa.’” Je, lingetendeka? Hakika! Naam, kabisa, hilo hakika lingetendeka; lingetendeka. Lakini sasa, juu ya kuthubutu kwangu...Sasa, *kuthubutu* ni—maana yake ni “kuenda bila ruhusa.” Ona? Naenda chini kule kumsaidia mtu huyu; nadhania tu itakuwa vema. Ona? Basi sijui; naweza kulitaja jina la Bwana juu yao; naweza kuwaombea, kufanya cho chote ninachotaka kufanya.

¹⁶⁰ Kama ningefanya nipendavyo asubuhi hii...Ni—nilikuwa na mahojiano na huyu mama anayeketi katika hiki kiti cha kusukumia wagonjwa. Kuja kwa mkutano huu leo, iliwapasa kuita idara ya wazima-moto kumwondoa ndani ya nyumba

yake kule Chicago; na watu wanaishi hapa upande wa pili wa barabara na hawahudurii mikutano. Ona?

¹⁶¹ Ningefanyaje? Kama ingekuwa ni nguvu zangu... Yako katika... Ninayo mamlaka kulifanya, lakini yanipasa ningoje amri ya kulitenda. Ona? Nina mamlaka toka kwa Mungu kulifanya; lakini sasa, Yeye atakapotoa amri, huyu atarudi nyumbani amepona. Ona? Najua hilo ni kweli. Ona? Ningalikuwa tayari kufia hayo asubuhi hii jinsi tu ningalikuwa tayari kwa cho chote kile. Ona? Hilo ni kweli.

¹⁶² Lakini kwanza mwaona, yote yako hivyo... Hakuna ye yote, hata Yesu Mwenyewe alisema, “Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndivyo atendavyo. Mwana vile vile.” Twajua hilo. Injili ya Yohana 5:19. Vema. “Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndiyo ayatendavyo Mwana vile vile.” Vema.

249. Je, ono lile ulilokuwa nalo miaka mingi iliyopita kuhusu muujiza mkuu ambao ungetendeka karibu Corydon, Indiana, je limetimia?

¹⁶³ Nilitazama katika kitabu changu nilipopata hili na kuweka alama ya kuuliza. Sasa, ilipasa kuwa na wakati ambao nilikuwa—nilipaswa kutazama ambapo hiyo miti ya mierezi... Mara tu uanzapo kushuka chini ya mlima ule pale, upande mwingine, kuelekea upande wa Corydon, baada ya kumaliza kile kilele cha mlima kule New Albany, ilinibidi kuitazama mierezi hiyo ajali mbaya sana ambayo ngingekuwamo. Na kwa neema ya Mungu, niliiepuka wakati msichana mdogo aliyekuwa akinywa chupa ya wiski, alipouawa—koo lake lilikatwa papo hapo na chupa aliyokuwa nayo kinywani mwake, msichana mwenye umri wa miaka kumi na sita, na ningalikuwa papo hapo kwa wakati huo. Ona? Sasa, huenda hilo ndilo ulilokuwa ukinena. Nilisoma hivyo.

¹⁶⁴ Kisha pia nilipokuwa na mkutano huu kwa Ndugu Beanblossom... Huenda ilikuwa hiyo. Huenda ilikuwa Georgie Carter. Ona? Nyingine ilitendeka kule. Halafu kuna manne au matano ndani mle... Sikuona lo lote ila lile lililokuwa limetimia. Kama—kama mtu yule aliyemandika hili angeandika tu tena na kuniambia yale niliyosema wakati huo, ndipo ningelitazama. Ona? Ukiniambia tu yale niliyosema, ono lile... Kwa sababu niliona katika ono lile pale mambo niliyoyaweka kitabuni mle, na hapa ndipo ilitendeka hivi. Sikuwa na lo lote lililoachwa, ambalo nilijua, jambo fulani lo lote nje ya hayo.

¹⁶⁵ Ndiposa kulikuwa na jambo lingine; hayo yalikuwa kuongoka kwa Omar Price chini kule wakati alipokuwa akinipinga vikali. Nanyi mwajua, yeye alikuja hapa maskanini na kubatizwa kwa Jina la Bwana Yesu. Ee, alinipinga vikali mno kuhusu hilo; nami nilikaa pamoja naye usiku. Niliendelea

tu kumpenda na kukaa pale tu haidhuru; lakini mwishowe yeye alikuja, kwa sababu Bwana aliniambia yeye atakuja, na kwa hivyo ni—nilikaa tu moja kwa moja nalo. Ona?

¹⁶⁶ Vivyo hivyo na mhubiri mnayemjua anayeketi nyuma yangu hapa. Nilienda chini kule Clarksville kuongea naye wakati mmoja, kumhubiria yeye katika hilo kanisa la Methodisti, naye alikuwa Mmethodisti kupindukia ninalomaanisha. Nilirudi tena juu hapa: Nilisema, “Wakati mmoja nitambatiza katika Jina la Bwana yesu Kristo.” Nami nilifanya hivyo; huyo ni Ndugu Neville!

250. Kama ni kosa kwangu ku—je, ni kosa kwangu kuendesha duka la urembo? Mimi ni mwuza vitu vya kujirembesha na siamini katika wanawake Wakristo kukata nywele zao, lakini nakata za wengine na (nadhani ni kutia r-a-n-g-i, rangi, hilo maana yake ni rangi, nadhani, sivyo?) kutia rangi pia.

¹⁶⁷ Dada mpendwa, ninge—singejua la kukwambia. Sikiza, siwezi kuwaambia wanawake kuhusu hilo, kuweka rangi katika nywele zao. Sina Andiko dhidi ya hilo; naweza tu kukaa na Maandiko. Ona? Andiko halisemi wao wasifanye hilo. Andiko lasema lazima wawe na nywele ndefu, na baada ya hilo, sijui nielekee wapi. Ona? Si—sijui lo lote kuhusu hilo.

¹⁶⁸ Sasa, mhudumu fulani aliyeko humu mahali fulani nimjuaye, rafiki msiri wangu, tulikuwa tukiongea pamoja majuzi kule Blue Boar tulipokuwa tunakula chakula cha kutwa Yeye alisema “Mke wangu huona haya kuja mbele ako.” Mwanamke mtakatifu mno, na mcha Mungu, nimjuaye, naye ni—ni mwanamke mzuri sana, nyanya, na . . . Lakini yeye ni mzuri, mwadilifu, mwanamke halisi . . . Mke wangu anampenda sana mwanamke huyu, na—nami nadhani yeye ni mwanamke halisi, kabisa. Yeye . . . Sijui kama yeye anaketi humu; nadhani yumo. Nadhani mume wake yuko hapa. Na yeye aliniambia; akasema, “Aliacha nywele zake ziote baada ya kukusikia ukihubiri naye anaona ni sahihi, lakini,” kasema, “yeye anatumia rangi fulani katika nywele zake; naye anajaribu kadiri awezavyo kufanya rangi hiyo ipungue kabla hajakugaribia.”

¹⁶⁹ Sasa tazama, Dada mpendwa, naheshimu hilo sana. Nina heshima kwa mwanamke ambaye atafanya hilo. Maana wanawake wengine huja na kufanya nywele zao vyo vyote, au kukutemea mate mguuni mwako na kutembea hapa na pale kwa kiburi na hawana heshima kamwe, kumbuka, Yesu alisema, “Yale uwatendeayo hawa umenitendea Mimi.” Ona? Nami naheshimu hilo ndani yako, na Mungu atakubariki kwake.

¹⁷⁰ Lakini, Dada, kuhusu rangi za nywele au kitu kama hicho, si—sijui. Si—siwezi kuliunga hilo mkono kwa Maandiko, kwa hivyo ni—hilo ni juu yako. Mwaona? Wewe, ukitaka kulifanya, hilo ni sawa kabisa kwangu. Nijuavyo mimi, kanisa halina

desturi kama hizo. Kama unataka . . . Lo lote ambalo haliko katika Biblia hii, vema, una . . . Hilo ni juu yako. Mwaona? Lakini nitawapa tu wosia wangu, basi nijuaavyo mimi . . . Mwajua, ni hali ya mwanamke kutaka kuonekana mrembo; yeye anapaswa kuwa hivyo.

¹⁷¹ Mwajua, katika kila nama ya kiumbe, wa kiume ndio wanaovutia mno, ila uzao wa mwanadamu. Chukua ndege ye yote, ng'ombe. Chukua kundi la ng'ombe wa kike. Gani malidadi mno, ng'ombe jike aliye na pembe zilizokunjamana au mdume mkubwa? Chukua paa; yupi, ni jike au ndume mkubwa? Chukua kundi la kulungu; gani malidadi mno, wa kiume au wa kike? Kongoni, ye yote utakaye kumchukua. Mchukue—chukua katika ndege; tazama katika kuku, jogoo au koo? Chukua katika ndege, yule—jimbi mkubwa malidadi au koo la ndege, anayeketi kwenye kiota na kuatimia mayai yake? Ona? Kila kitu katika viumbe vyote, kila mara cha ki—kiume ndicho malidadi zaidi, isipokuwa mwanadamu wa kike. Kwani? Yeye alisababisha ndiye kule kuanguka. Shetani alimchagua yeye papo hapo, na urembo ni wa Shetani. Ona?

¹⁷² Shetani alikuwa ndiye malaika wa kuvutia sana. Yeye alikuwa kerubi aliyefunika. Tazama jinsi wanawake wanavyokuwa tofauti sasa na vile walivyokuwa. Wangapi wanamkubuka Pearl—wamesoma habari za Pearl O'brien? Hebu tuone mikono yenu, baadhi yenu watu wa kale. Hakika. Ona? Ndiye aliyedhaniwa kuwa mwanamke mrembo sana katika Amerika. Msichana ye yote anayeyumbayumba barabarani angekuwa mrembo mara mbili zaidi yake sasa. Mbona? Hilo ndilo Biblia ililosema hasa; “Wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri . . .” Hilo lilikuwa kundi la walaghai waliosababisha gharika juu ya nchi, hata Mungu akaangamiza uzao wote wa mwanadamu. Ona? Ndivyo hasa. Na leo kila kitu kina msingi juu ya Hollywood na—na urembo na mambo kama hayo, wakati urembo hasa ni kitu cha siri kilichoko moyoni (ona?) na si cha kuonekana kwa nje. Na wajipambe wenyewe, si kwa nje, lakini kwa ndani, kwa roho ya upole, utulivu. Hao ni—hao ni Wakristo.

Kwa hivyo, kwa swali lako, Dada, sijui tu la kukwambia.

Sasa, naweza kukomea papa hapa sasa au nichukue dakika zingine thelathini basi, halafu . . . Je, dakika thelathini zinge- . . . ?

Wangapi wanaweza kukaa dakika zingine thelathini, na ndipo hilo litatupa wakati mwingine zaidi usiku huu. Vema, nitaharakisha basi.

251. Ndugu Branham, je hii I Timotheo 2:9 ina maana kwamba mwanamke awezi kusuka nywele zake? Je, “kusuka” nywele kunamaanisha maana “kusokota” nywele?

173 Sasa tazama, Dada, sasa hili... Nina—nina furaha hilo lilifuata hili. Sikulipanga pale, lakini tu—yalifuatana vizuri.

Tazama, nywele zilizosukwa siku hizo zilikuwa ishara ya mwanamke wa mitaani; hayo ndiyo yeye aliyofanya, kusuka nywele zake. Na Paulo aliwaambia Wakristo, “Sasa, huko kujipamba, kusiwe kwa kusuka...” (au ‘kusuka’ na ‘kusokota’ ni mamoya)—kusuka nywele zao, kwa sababu ilionekana kama walimwengu wengine.

174 Sasa, mnapaswa msionekane kama walimwengu au kutenda kama walimwengu! Ona? Wanawake wanapaswa kuwa tofauti pale. Ona? La, sasa, kusuka nywele... Sasa, leo nywele iliyosukwa ni malidadi, na ni mbali sana na mtindo wa ulimwengu. Sasa, mmeona wanawake, jinsi wafanyavyo nywele zao siku hizi... Tunzeni tu nywele zenu kwa njia yo yote; lakini msionekane kama walimwengu! Ona? Msionekane au kuvalia kama wao! Wakivaa suruali, ninyi vaeni nguo za wanawake. Waki—wakifanya nywele zao kama—wakizikata na kuzifupisha, na kuzifanya vyo vyote... Ni—ni—ninyi achilien zenu. Ona?

175 Na kusuka—lakini kusuka... Swali lilikuwa: Je, kusuka maana yake—“kusokota” maana yake ni “kusuka?” Naam, ndivyo. Na sasa, kule barabarani...

176 Sasa nililichunguza nipate kujua miaka mingi iliyopita maana ya “kusuka” nywele. Ona? Mwanamke, hakika, wanawake wa kale, walivuta tu nywele zao nyuma na kuzifunga, karibu kama kufunga kifundo kichwani siku hizi. Na walienda hapa na pale... Walikuwa wanavalia mavazi hivyo, lakini wanawake wa mitaani walishika nywele zao na kuzisuka mistari vichwani mwao, na kuisokotasokota kote hivyo, na kuzitia maua na vitu kama hivyo, na hiyo ilikuwa kama—kama kipusa wa mitaani; kama tu vile tungeona kipusa siku hizi, jinsi avaliavyo. Nasema, *kipusa* kwa sababu mwajua mimi ni mzee, hivyo ndivyo walivyowaita katika siku zangu. Wanaitwaje siku hizi? Ni... Lo, sijui. *Kisura* au cho chote kile. Kwa hivyo... Cho chote kile. Wape jina lo lote lile, wanapenda hayo.

252. Ndugu Branham, ulisema kwenye kanda moja kuwa Nuhu aliokoa nyumba yake. Je, hili lamaanisha mama aweza kuwa na imani ile ile kwa ajili ya nyumba yake? Na lamaanisha kila mmoja wa jamaa ataokoka akiamini?

177 Sasa, hilo ni—naam, hilo lina... Yakupasa uchunguze ninavyojibu swali hili sasa. Ona? Kwanza, “Ulisema... (Sasa, hebu nitazame vizuri...) Ulisema kwa mojawapo ya kanda zako kuwa Nuhu aliokoa nyumba yake.” Kwani? Kwa sababu wao waliamini. Naam, kwa sababu waliamini ujumbe wake.

178 “Je, hili lamaanisha mama aweza kuwa na imani ile ile kwa nyumba yake?” Naam, Dada! Naweza kuona moyo wa mama ukiwalilia watu wake. “Na hili lamaanisha kila mmoja wa jamaa ataokoka tukiamini?” Naam, kama watakubali. Hiyo ni kweli.

179 Kumbuka yule mlinzi wa jela kule Filipi. Amini kwa ajili ya wote. . . Kama una imani ya kutosha kwa wokovu wako, si unaweza kuwa na imani ile ile itakayofanya kazi kwa watu wako? Imani ni nini? Ni nguvu zisizoonekana. Ona? Roho ni—ni—ni nini? Roho Mtakatifu huleta imani. Ona? Ni nguvu zisizoonekana.

180 Mbona niweke mikono juu ya wagonjwa? Ona? Kama naweza kuwasiliana na roho aliye katika mtu yule pale, jambo fulani litatendeka. Ona? Hapa yuasimama Roho Mtakatifu; Yeye atafunua siri za moyo. Yeye atafanya barabara yale yote alisema angefanya katika siku za mwisho. Watu wanaamini hiyo; wanayatazama, “Naam, bwana, naamini hilo.”

181 Sasa, nisipokuwa tu wa kawaida sana kwenu (ona?)—linakuwa tu jambo la kawaida. Unajaribu tu siku moja na kujaribu tu siku nyingine. Ona? Huko ni kubahatisha tu. Ona? Kwanza huliadini (ona?), kwa sababu mara tu unapoliamini hakika. . . Mwanamke yule alisema, “Nikiweza tu kugusa vazi Lake, nitapona,” naye alifanya hivyo. Ona? Yeye hakusema, “Hebu nijaribu tena.” Ona? Yeye aliliadini. Ona? Hilo ni. . .

182 Sasa, ukiamini tu kwa vyote vilivyo ndani yako kwa ajili ya jamaa yako. . .

183 Sasa, kama hapa, nini hunichochea mimi? Nini—nini nguvu hii mkononi mwangu? Hakika si misuli yangu, ni roho yangu. Hakika, ondoa roho huyo, na misuli itafanyaje? Ni mifu kama iwezavyo kuwa, ona? Itaoza, lakini ni. . . Ona, ni roho anayetoa nguvu.

184 Mtazame maskini Samsoni. Wengine wao wameona milango na inaonekana kama ingekuwa kati ya hivi vizingiti hapa. Naam, mtu ukubwa huu angemwinua simba na kumraru vipande-vipande, Ndugu Jackson. Simba akimrukia mtu kama huyo na mlango—na mabega kama mlango wa ghala, naam hakika, hilo halingekuwa mwujiza; lakini mwujiza ulikuwa, yeye alikuwa mtu mdogo, mwenye nywele za kipilipili, mdogo, kijana wa kale, karibu—dada mdogo, mvulana mdogo wa mama, misokoto saba ya nywele za kike ikinig’inia mgongoni mwake. Lakini mnatambua, yeye alikuwa tu asiyeweza kama cho chote kile hata Roho wa Bwana alipomshukia. Na wakati Roho wa Bwana aliposhuka juu yake, simba huyo alimkimbilia na kumngurumia, yeye akamvunja-vunja vipande. Haikuwa Samsoni; Hiyo ilikuwa Roho wa Bwana.

185 Sasa, angechukua taya ya nyumbu, ambayo ilikuwa imekaa kwenye jangwa hilo na imekaushwa na jua hata ikawa nyeupe. . . Na hizo kofia za chuma za Wafilisti zilikuwa karibu unene wa inchi moja ya shaba nyekundu tupu. Vema, ukichukua hiyo taya na uigongeshe juu ya kofia moja ya chuma ingelivunjika vipande elfu. Mwajua hilo. Wangegonga hiyo taya ngumu, zee. . . Lakini tazama pale, yeye alisimama pale na taya

hii mkononi mwake na kuwaangusha Wafilisti elfu; wengi wao walikimbilia majabalini. Yeye alisema, “Njoooni, mnataka kuonja kidogo pia?” Angali—angali anaishikilia! Ilikuwa nini? Roho wa Bwana alikuja juu yake. Ona?

¹⁸⁶ Kwa hivyo, ni Roho wa Bwana. Na unapokuwa na Roho wa Bwana ndani yako kuamini kwa ajili ya wokovu wako mwenyewe, weka huko juu ya jamaa yako. Sema, “Nawadai katika Jina la Yesu Kristo: naudai! Mungu, sijui jinsi utakavyomfanya mwanamke alifanye, na jinsi utakavyomfanya mwanamume yule alifanye, lakini naamini. Naamini, Bwana! Saidia kutokuamini kwangu.” Iдай na ukatazame kile kitatendeka. Itatendeka.

253. Je, Bibi-arusi—je, Bibi-arusi kabla ya kuja kwa Yesu, je, atakuwa na nguvu zote za Roho Mtakatifu kutenda miujiza, kufufua wafu, na kadhalika kama katika ile mvua ya vuli—au je, hii mvua ya vuli ni kwa ajili ya wale Wayahudi 144,000? Je, wahudumu wote watakuwa nayo, tuna—au tunangoja tu kuja kule?

¹⁸⁷ Naam. Ona, rafiki, mi—mi—mimi si mwanatheologia. Mimi si mwanatheologia; kwa hivyo, yanipasa nifundishe yote nijuayo kuhusu Biblia kwa vivuli na mifano. Mnaniita mfundisha kwa mifano. Lakini kama naweza kutazama kwenye ukuta huo, nami sijawahi kujiona mwenyewe; nami nitazame, na naweza kuona nina kichwa, masikio, na mikono, na—nitajua jambo fulani kuhusu kile nitakachokuwa kama nikijiona mwenyewe. Ona? Nikiona sura yangu katika kioo, najua nilivyo kama ningesimama kando na nijitazame mwenyewe.

¹⁸⁸ Sasa, hivyo ndivyo ninavyowaza kuhusu Biblia. “Mambo haya yote,” Warumi 26 ilisema, “yalikuwa mifano kwetu.” Tunaweza kutazama nyuma na kuona jinsi yalivyokuwa, kama vile mwezi unavyorudisha nuru ya jua. Tunajua jua litakavyokuwa wakati—tusipoona jua; tunaweza kuona mwezi, na kuona kuwa litakuwa kubwa zaidi ya huo. Vema, mnapoona yale yanayotendeka katika Agano la Kale, ni mng’ao tu wa nuru uliorudishwa wa yale yaliyotendeka katika lile Jipya.

¹⁸⁹ Sasa, ndani humu, naamini kwa moyo wangu wote mimi—sisi tuna, au siku hizi. . . Kama hatuko hivyo, mtu fulani yuko hivyo; haina budi kuwa hivyo. Wakati umekwisha; tuko mwishoni!

¹⁹⁰ Kila. . . Ulimwengu. . . Mungu aliumba ulimwengu kwa miaka elfu sita, na katika miaka ya elfu saba akastarehe. Yeye alisema mwanadamu hataishi kamwe amalize wakati huo mwa—mwa—mwaka—au—au siku—“siku ulapo, ndiyo siku utakayokufa.” Adamu—au Methusela alikuwa ndiye mtu aliyeishi sana katika Biblia, naye alikuwa na umri wa miaka 969; naye hakuishi hiyo miaka elfu. Lakini mtu atakayeishi miaka hiyo yote elfu ya ule Utawala wa Miaka Elf, miaka elfu, kuonyesha kuwa—adhabu hiyo imekwisha lipwa. . .

Mwanadamu ataishi milele; siku imekwisha; wakati umekwisha; wako utukufuni.

¹⁹¹ Walakini, nimepata barua nyingi sana kuhusu ujumbe wangu Jumapili mbili au tatu zilizopita juu ya—*Yale Makao Yajayo ya Bibi-arusi na Bwana-arusi*. Hilo hakika liligusia ndani mahali fulani kwa wengi wao. Hilo. . . Lilifanya hivyo kwangu pia. Haijaniacha bado.

¹⁹² Sasa, tazama. Juu ya hili (ona?), Ibrahimu aliona. . . Sasa, kama Yeye alivyomshughulikia Ibrahimu, ndivyo atafanya na uzao wake Sasa, hivi karibuni nitakaporudi wakati fulani, nataka kuleta hilo karibu zaidi na kuwaonyesha ninyi hasa kituo cha maisha ya Ibrahimu. Ni vivyo hivyo na Luther, Wesley, na kuendelea hadi hapa, jinsi Yeye alivyoshughulikia makanisa ndivyo Yeye alivyomfanyia Ibrahimu; jinsi Yeye alivyomtokea; jinsi Yeye alivyoimarisha agano kwake chini ya damu iliyomwagwa, ndio uliokuwa wakati wa Filadelfia. Naam, bwana, huo ulikuwa wakati wa damu, Luther—ule wakati wa Wesley.

¹⁹³ Lakini sasa tazama ule wakati wa Pentekoste. Baada ya Yeye kufikia pale, Yeye alitoa ahadi ya *El Shaddai*, “Ninyonye mimi.” Swali ni: Waweza kunyonya? Lile lililoletwa mbele ya Wapentekoste. Ona? Waweza kunyonyeshwa? Lakini hawakufanya hivyo; walijinyakulia ti—titi la dhehebu walimotoka. Lakini yule Mzao, Mzao halisi, alikuja kunyonya titi hilo.

¹⁹⁴ Na ishara ya mwisho waliyokuwa nayo kabla huyo mwana aliyeahidiwa waliyemngoja miaka hii yote arudi ilikuwa nini? Ilikuwa Mungu akisimama katika mfano wa Mwanadamu na kupambanua mawazo yaliyokuwa moyoni mwa Sara (Sara akiwa Kanisa, akiwakilisha Kanisa)—kupambanua mawazo yaliyo katika Kanisa hata yale yaliyokuwa nyuma Yake. Sivyo? Na mara tu baada ya hayo, Sara aligeuka kuwa msichana na Ibrahimu mvulana; na Isaka akazaliwa, yule mwana aliyeahidiwa.

¹⁹⁵ Naamini mnaona jambo la mwisho litakalotendeka kwa Kanisa kabla ya kunyakuliwa. Naam. Naliamini. Mvua imekwisha. Soma tu sura za kwanza tatu za Ufunuo na mtaona yale yaliyoahidiwa kwa Kanisa. Hilo ndilo lililoahidiwa, kanisa, papo hapo—nyakati za kanisa.

¹⁹⁶ Mnatambua majuzi tulipoanza hizo baragumu, Roho Mtakatifu alisema, “Hizo si za hapa.” Ona, ona?

¹⁹⁷ Sasa, mvua ya vuli, Wayahudi 144,000, la, hilo si—hilo—hawawezi—hilo ni—hilo ni wakati Eliya na Musa. . . Hapo ndipo miujiza inatendeka. Mambo ambayo watu wanatarajia, Wapentekoste, kutarajia miujiza, hapo ndipo hayo yatatendeka katika hilo—chini yao. Ona, hiyo ni ya Eliya na Musa. Wanapiga dunia kwa laana kila watakapo; wanafunga mbingu

ili isinyeshe katika siku za unabii wao. Na Mungu, atasimama na kuwapigania wao kama vile Yeye alivyofanya, kisha atawaondoa kwa mkono wenye nguvu kama vile tu Yeye alivyofanya katika Misri (ona?), toka kwa haya “mafundisho” ya ulimwengu. Na yeye atafanya hilo, lakini hilo si . . .

¹⁹⁸ Sisi yatupasa tu kungoja kule kuja kwa Bwana. Kungoja tu; tengezeni taa zenu, huku zimejaa mafuta. Ombeni kila saa, si kila siku, kila saa. Iweni tu tayari; iweni tayari, iweni wazuri, na mkikeshana . . .

Ee, tunatazamia kuja kwa siku hiyo kuu yenye furaha tele ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja na kunyakua Bibi-arusi Wake anayemngoja. Ee, lo—ee, lo moyo umejazwa na kunyakuliwa ninapofanya kazi na kungoja, na kuomba, maana Bwana wetu yuaja tena duniani.

Naam; hilo ndilo tumaini la Kanisa saa hii.

254. Jina la “Yesu Kristo” ni sawa kwa ubatizo, au yapasa iwe kwa Jina la “Bwana Yesu Kristo?”

¹⁹⁹ Mojawapo. Nachukua *Bwana Yesu Kristo* (ona?), kwa sababu nadhani Yeye ni Bwana wetu. Sasa, kwa *Jina la Yesu* tu kama ndugu zetu wengine wabatizavyo, ni—ninatofautiana pale (ona?), kwa sababu najua nina marafiki wengi wanaoitwa Yesu, wengi sana—marafiki wengi wahubiri kule Mexico, na—na Italia, na kwingineko. Wao wanaitwa *Yesu*, na kwa hivyo *Yesu* pekee halitoshi. Yeye alizaliwa Kristo Mwokozi, kama Yeye alivyojaliwa Mwokozi, Kristo, yule mtiwa mafuta. Na siku nane baadaye akapewa jina la *Yesu*. Ona? Basi Yeye alikuwa Bwana Yesu Kristo. Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Vema.

255. Ndugu Branham, je, Bwana aweza kukuruhusu utufundishe kuhusu swali la ndoa na talaka wakati huu? Swali; Je, mwanamume aweza kumwoa mwanamke na akaachwa na mwanamke yule halafu akamwoa mwingine? Wote wawili wakioa au kuolewa na mwingine, je wote wanazini? Ulitaja lingeshikamana na uzao wa nyoka. Vipi hivyo?

²⁰⁰ Sasa, hapa—hapa kuna mojawapo wa swali la hadhari sana tulilo nalo katika mafurushi haya, na ndilo linaloswaliwa sana u—u—ulimwenguni siku hizi. Sasa, nisikizeni, nami nina sababu yake. Kama hakika nililileta humu kanisani na kwenye kanda hii asubuhi hii, jambo sahihi kuhusu ndoa na talaka, ingevunja kila kanisa nchini kama wangelisikia. Ona? Hiyo ni kweli.

²⁰¹ Sasa kwa hivyo anisaidie, hapa kuna Biblia mbele yangu, kwa swali hilo nina, BWANA ASEMA HIVI! Na pande zote mbili zinazobishana zimekosea. Wote wanaoaa tena waliiolewa na kadhalika, wote wamekosea kwa yale wanayofanya, lakini kati

yake kuna Ukweli, katikati ya njia. Sitaki ku . . . Nitanasa kanda ili kama jambo fulani likinipata, basi ndugu wanaweza kuicheza baada ya kuondoka kwangu (ona?) kwa makanisa. Lakini nininataka kufanya kanda kuhusu hayo na kuwaonyesha tu ilivyo; lakini hadi nijisikie nikiongozwa na Bwana, sitasema lo lote kulihusu. Lakini naona kuwa katika mambo haya yanipasa niongozwe na Bwana; nisipoongozwa, nitafanya madhara mengi kuliko nitakavyofanya mema. Ona?

²⁰² Sasa, nataka ninyi mtambue hili. Swali: “Je, mwanamume aweza kuoa mwanamke na aachwe na mwanamke huyo halafu aoe mwingine; na wote wawili wakioa au kuolewa na wengine, wote wanazini?” Sasa, rafiki yangu, sitaki kuumiza dhamira yako; lakini hilo ni Kweli. Yesu alisema, “Ye yote akioa mwanamke aliyeachwa azini.” Ona? Sasa, sitaki tu kusema, lakini ni Kweli.

²⁰³ “Ulitaja hili lingeshikamana na uzao wa nyoka.” Ona? Sikumbuki kutaja hilo, lakini labda nililitaja mahali fulani, nikasema jambo, fulani kulihusu.

²⁰⁴ Kama majuzi, nilifarakanisha jambo fulani, nililisia, na ni . . . Nililishika papo hapo; na liko kwenye kanda, nami labda ni—nitaisikiza. Nilipokuwa naongea kuhusu zile Baragumu Saba, nilisema zilikuwa baragumu saba. Nilikuwa nataja karamu ya Pentekoste. Toka sikukuu ya Pentekoste hata saba—hata zile—zile Baragumu, kulikuwa na Sabato saba. Sabato saba zilikuwa kati ya sikukuu ya Pasaka hadi Pentekoste (mwaona?), ambayo ilifanya siku hamsini. Ona? Lakini kile nilikuwa nataja, kuwa ndiyo, nilisema, Hilo lamaanisha Nyakati Saba za Kanisa.

²⁰⁵ Kwa kanda hiyo (ukiipata au lo lote)—kwenye kanda hiyo yapasa iwe hivyo, kwamba mwezi wa saba baada ya hiyo ilileta ile—ile siku Kuu ya Baragumu, ambayo inamaanisha Nyakati Saba za Kanisa—miezi saba, si sabato saba. Sabato saba zilienda kwa . . . Nilieleza hiyo kule. Nilisema Sabato saba, hivyo, lakini ndipo nilibeba wazo lile lile kuliendeleza, bali ni mwezi wa saba baada ya Siku Kuu ya Pasaka—au kwenye Karamu ya—ya Pentekoste, ndipo huja karamu ile, baada ya miganda kuletwa, kutikiswa. Mwaona basi—basi . . . Kumbuka pale, miganda inakuwa mkate baada ya wakati huo. Ona? Wakati ule—ule mganda wa—mganda mmoja, ndipo wote waenda katika mkate mmoja. Ee, ni mafundisho makuu pale; sikugusia ukingo wake. Lakini ukinyapata hayo kwenye kanda yako, kumbuka, tazama katika Biblia. Mwaona, ni miezi saba baada ya hilo. Hesabu miezi saba: Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, na Julai—ingekuwa Julai, miezi saba, ambayo yaainisha Nyakati zote Saba za Kanisa. Mhudumu fulani huenda akayachukua hayo, na ndipo ungefahamu. Mwafahamu pale? Vema.

²⁰⁶ Sasa, juu ya hili hapa, na—na—na tu . . . U . . . Hili ndilo nisemalo. Na niseme hili, si Bwana, hebu nisema. Kama umeoa

wakati huu, nanyi wawili mumeokoka, na mmejazwa na Roho Mtakatifu, na mnapendana, na mna watoto wadogo (sasa, kumbuka hili ni mimi, si Bwana. Ona?), endeleeni mkaishi pamoja, mwe na furaha; kwa sababu hungeishi na mke wako wa kwanza au kweli hungelioa. Ndipo ukimwacha huyu na kumrudia tena yule wako wa kwanza, unatenda vibaya kuliko ulivyofanya kwanza. Ona? Kwa hivyo ona, umefarakanika; hakuna njia ya kuondoka ndani ya hayo. Kungekuwa tu na njia moja hakika ambayo naweza kusema kwa Biblia; ninyi nyote wawili ishini bila kuoa wala kuolewa tena. Ona?

²⁰⁷ Sasa, lakini. . . Hiyo ndiyo njia ningesema hivi sasa, lakini kuna jambo moja ndani mle, ambalo si—siwezi kuwaambia ninyi sasa, na sababu nasema, “Si mimi, ila Bwana, endeleeni.” Kama mtaweza kuleta hilo kwenye kanda, na siku moja, kama nikilileta, kumbukeni jinsi nilivyosema hilo. Kama mna hekima, mngelielewa hayo (Ona?, jinsi nilivyosema hilo basi, basi mngejua.)

256. Ndugu Branham, yatupasa kuhudhuria makanisa mengine hata ikiwa wao hawakubaliani nawe?

²⁰⁸ Hakika naam! Yesu alienda ingawa hawakukubaliana naye. Endelea. Twaona hapa lasema, “Yatupasa kuhudhuria kanisa lingine lisilokubaliana nawe?” Hakika, si. . . Mimi siye changarawe pekee pwani, mwajua. Kuna—kuna watu wengine wacha Mungu kila mahali; natumai mimi ni mmojawao. Ona? Ona? Lakini usifike chini hapa. . .

²⁰⁹ Niliingia katika kitu fulani kama hiki majuzi. Ku—kundi moja katika Arizona liliniambia hayo. Ona? Kundi la wahudumu lilisema, “Jambo pekee tulilo nalo dhidi yako, Ndugu Branham, ni (mojawapo wa mambo haya) watu wanaokuja nje hapa pamoja nawe, hatuwezi kuwafanya wahudhurie kanisa mahali po pote.” Kasema, “Wana watoto na kila kitu; hawawezi kuenda kanisani.” Na Kasema, “Vema, tuliwaambia kitu; hawawezi kuenda kanisani.” Na kasema, “Vema, tuliwaambia wamealikwa kuja—kuja kanisani mwetu.”

²¹⁰ Sasa, najua wanaweka mkazo kwenu na kutaka ninyi kujiunga nao, lakini haimpasi mjiunge; lakini wapelekeni watoto kwenye shule ya Jumapili mahali fulani! Nanyi nendeni kanisani; msiketi nyumbani, kuenda kuvua samaki, na kuwinda, na mambo kama hayo mnamo Jumapili.

Mnasema, “Vema, mimi si mshikilia sheria.”

Vema, heri uwe katika hali hiyo kwa muda mchache, kutoheshimu ule ufufuo wa Kristo. Nyinyi endeni kanisani mahali fulani!

²¹¹ Kama ni—kama ningalienda. . . Kama singepata. . . Kama nilienda kwa kanisa *fulani* ambalo najua kuna jambo moja tu ninaloamini ambalo watu wale waliwahi kusema—walisema wao wanaamini Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Walisema

hivyo (nalitilia shaka), lakini ningependa kwenda kuwasikia wakisema hilo. Pengine wewe husema... Hilo ni kanisa hili, labda kanisa linalofuata litakuwa kitu kama Baptisti. Wao husema, "Naam, naamini yakupasa uwe na tukio fulani." Nita—nitaenda nao hapo. Ndipo naamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu; naamini yakupasa uwe na tukio fulani. Vema.

²¹² Kisha labda kuna Assemblies of God. Sasa, wao wanaamini... Ona, ni—sasa ninaweza kula vipande vitatu au vinne vya mkate pamoja nao (ona?), kwa sababu wanaweza kuamini...

²¹³ Kama hivi majuzi, mtu yule aliniita na kutaka kujua kuhusu hilo, na kusema, "Ulisema..." (Mhudumu huyu nje kule mtu huyu kule chini aliyetaka kujadili hilo. Maskini ndugu huyo, yeye amedanganyika jinsi gani.) Yeye alisema, "Vema, Ndugu Branham (ona?)," yeye kasema, "yeye anawapinga ninyi Assemblies of God." Na mhudumu wa Assembly akipata kanda hii, nataka wewe uniambie lini nilipinga mtu wa Assembly of God au mtu mwingine! Mbona hivyo, hali makao yenu makuu yanakubali kuwa nimewaletea robo tatu milioni ya watoto wangu niliomzalia Kristo? Naweza je kuwa dhidi ya Assemblies of God? Sababu gani nipingene oneness? Mimi sipingi oneness. Assemblies of God, Church of God, wala mtu ye yote! Mimi napinga kila utaratibu unaowatenganisha wanadamu.

²¹⁴ Tazama, nimepeleka kwa Assemblies, kwa hesabu yao wenyewe robo tatu milioni ya watoto wangu. Kama ni wabaya sana, mbona nafanya hivyo? Mbona? Nadhani ndilo bora sana lililomo nchini kuwapeleka kwake—mojawapo ya oneness au zile—baadhi ya zile zenye imani ya Kipentekoste, kwa sababu wanaamini uponyaji wa Kiungu; wanaamini matokeo ya kimbinguni; wanaamini ubatizo wa Roho Matakitu. Hilo ndilo bora sana... Siwezi kuwaleta wote papa hapa; wako ulimwenguni kote. Nina marafiki ulimwenguni kote, watoto niliomzalia Kristo. Nitawapeleka kwa lile bora... Je, mliwahi kunisikia nikitoe wito wa madhabahuni? Ninasema... Niwaletapo juu pale wapate kuokoka, nasema, "Sasa, ninyi endeni kwa kanisa fulani nzuri la Injili Nzima mpate kanisa la nyumbani." Wangapi wamewahi kunisikia nikisema hilo? Hakika, hakika. Vema, sababu gani niwapeleke kule basi? Je, si ningekuwa mnafiki kupeleka watoto wangu mautini? Na isiwe hivyo kwangu, La, bwana!

²¹⁵ Kama huwezi kwenda... Kama hamwezi kuja hapa maskanini, tafuteni kanisa fulani mahali fulani; enendeni kwalo. Haikupasi kuchukua yote wafanyayo. Hata washiriki sehemu gani ya mkate, wewe kula mkate. Wanapofikia kitunguu saumu, naam, kiache hicho pekee. Ona? Ndivyo. Siwezi kuwafanya wakalifanya, lakini hilo ni halisi... Hakika, nenda kanisani. Po pote mlango wa kanisa ufunguliwapo, nenda upesi uwezayo. Kama hawaamini, vema... Sasa, haikupasi kuwa mshirika.

Msijiunge nao, msijiunge na yo yote ya makanisa hayo; lakini endeni kwayo; shiriki nao. Mwajuaje si Bwana? Yeye alisema angefanya kila kitu kiendeleo vema? Na labda kuna watu ndani mle ambao wanapaswa kuokoka, na unaweza kuwaangazia Nuru. Ona? Enda kule. Usiende kwa kiburi, enda kwa unyenyekevu; na watu wote waanze kunena juu yako, “Huyo ni mwanamke mzuri Mkristo, na mume na mke Wakristo; huyo ni mvulana au msichana Mkristo. Lo, ningependa ku... Wee, hakika wanatenda kama walio na kitu fulani.” Ona? Na kusema, “Ni nini?”

“Jambo ni hili.” Ndipo waambie. Lakini iweni tu wanaokolea mno, nao wataona kiu.

257. Mpendwa Ndugu Branham: Je, unaamini kuwa yapasa ishara zifuatae hao walio na Roho Mtakatifu?

Yesu alisema hivyo Marko 16.

Kama ndivyo, vipi kwa watu wanaoamini Ujumbe kwa vyote vilivyo ndani yao, hali hawana ishara hizi? Je, wao ni wasioamini au wanahitaji Roho Mtakatifu? Kama ndivyo, tafadhali utufundishe leo, jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu. Tunaamini wewe u mnenaji wa Mungu kwetu siku hizi. Ndugu yako.

²¹⁶ Asante, ndungu yangu, kwa kunichukua mimi kama ndugu ya—yako, nami nadhani hilo ni swali nzuri mno. Marafiki, naam, ni legevu kidogo. Ningependa kushughulikia hilo kwa muda mwingi kidogo kama ningeweza. Ona? Ni legevu. Tazama! Baadhi yenu... Ona? Wakati—hamwezi kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu bila kuwa na tukio inapotendeka... Sasa, unaamini “kila chembe ya Neno,” unasema... Unasema unaamini kila chembe yake, basi Neno linakaa ndani mle likingoja Roho Mtakatifu kulifanyiza kazi, lakini kunahitajika kuwashwa mshumaa.

²¹⁷ Hapa kuna mshumaa na utambi ndani yake, na mafuta yote, na kila kitu kipaswacho kuwako ndani ya mshumaa huo; lakini hadi moto uje juu yake, hautaangaza nuru yo yote. Haijalishi mshumaa huo u mkamilifu jinsi gani, na utaungua kikamilifu jinsi gani na kadhalika, sharti uwashwe, kisha utaungua. Na unapoamini na umefundishwa Roho Mtakatifu ni nani, upendo, furaha, amani, saburi, wema—matunda anayozaa, hadi Roho Mtakatifu na tukio moto moto atakaposhuka kuwasha mshumaa huo, basi una—una—hujampokea Roho Mtakatifu. Ona? Yakupasa uwe na tukio upate kuwa na Roho Mtakatifu.

258. Niko kwa chama cha wafanyi kazi, hili ni kosa kwa Mkristo? Neno lasema, “Usiape—usiape.” Yatupasa kuapa kulinda katiba ya hicho chama cha wafanyi kazi. Sijakuwa mwenye juhudi sana tangu kuwa Mkristo, lakini bado nalipa ada yangu.

259. Je, jina la Yuda Iskariote lilifutwa toka kwa Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, au halikuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo?

218 Vema. Kuhusu chama cha wafanyi kazi: Najua unafanya kazi. . . Ninyi watu mna vyama vya wafanyi kazi na kadhalika ambavyo mna. . . Kama unataka kufanya kazi, yakupasa ujiunge navyo. Ndivyo hasa. Yakupasa ufanye hivyo. Lakini kitazame (ona?), kwa sababu kitageuka toka kwa chama cha wafanyi kazi hata kuwa dini hivi karibuni. Ona? Sasa, kumbukeni tu, ni utangulizi wa kuungana kwa kila kitu. Huwezi kufanya kazi; hawatakuruhusu ufanye kazi; wewe u—u “kigaga” isipokuwa u— isipokuwa uwe kwa muungano huu.

219 Sasa kumbuka, ninyi vijana, kumbuka yale Ndugu Branham anasema. Na maneno haya yaandikwe ndani na kalamu ya chuma katika m—m—mlima wa chuma cha pua! BWANA ASEMA HIVI, jambo lile lile litatendeka katika dini. Utakuwa kwa dhehebu la namna fulani, au huwezi kununua wala kuuza. Kwa hivyo jihadhari sana, Ndugu. Na acha tu kionekane kama chama cha wafanyi kazi pekee. Litazame; ni onyo!

220 “Jina la Yuda Iskariote lilifutwa toka kwa kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, au halikuwahi kuwa kule?” Naam, lilikuwa kwenye Kitabu kile na likafutwa. Ona? Kwa sababu katika Mathayo sura ya 10, Yesu alimwita Yuda na wengine wote, na kuwapa nguvu dhidi ya pepo wachafu. Walienda wakitoa pepo, na Yesu alisema, “Mimi hata nilimwona Shetani akianguka kutoka Mbinguni.” Sivyo? Nao walirudi, na wanafunzi hao wote pamoja, nao walikuwa na furaha; naye alisema, “Msifurahi kwa—Shetani anavyowatii ninyi, lakini furahini kuwa majina yenu yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima.” Ona? Naam. Na Yuda alikuwa papo hapo pamoja nao! Ona?

221 Kwa hivyo kumbuka, hukumuni, tazama, kwenye kiti cha hukumu, “Hukumu iliwekwa; vitabu vikafunguliwa, na Kitabu kingine kikafunguliwa ambacho kilikuwa kile Kitabu cha Uzima, na kila mtu akahukumikiwa kulingana nacho.”

222 Sasa, naam, kwa swali kitambo kidogo kilichopita. Ona. Kwenye kile kiti cha hukumu. Yesu, Kanisa, Bibi-arusi, walinyakuliwa, walienda Utukufuni, na walikuwa juu pale na wakaoana, wanarudi duniani, na kuishi maiaka elfu. Mwishoni mwa ile miaka elfu Shetani anafunguliwa toka kifungoni mwake, ambamo amefungwa na Malaika kwa pingu, si pingu za kawaida, lakini ni pingu za hali ilivyo; raia wake wote walikuwa kuzimuni. Wote waliofufuliwa duniani walikuwa wamekombolewa na Yesu yuko pamoja nao. Yeye hangalitendea kazi juu ya cho chote; lakini mwishoni mwa ile miaka elfu, ufufuo wa pili. . . “Heri na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu.”

²²³ Sasa tazama, katika huu ufufuo wa pili, wanapofufuka, ndipo Shetani anafunguliwa toka kifungoni kwa muda mchache; kisha hukumu inawekwa. Sasa, tazama, Yesu akiwa na Bibi-arusi, kama Mfalme na Malkia, wanaketi kwenye kiti cha enzi, kiti cha Cheupe cha Enzi, hukumu; na vitabu vikafunguliwa, vitabu vya wenye dhambi. Na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa Kitabu cha Uzima; na kila mtu alihukumiwa hivyo na Bibi-arusi, “Hamjui ya (kupeleka haya mambo madogo mbele ya sheria) hamjui kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu?” Ona, Ona? Vema.

260. Tafadhali, waweza kueleza hilo kundi la Ufunuo 20:4 ni akina nani? Je, wao ni sehemu ya Bibi-arusi wa kale au wa usoni?

²²⁴ Wao ni Bibi-arusi wote, wote wa kale na wa sasa. Wao ni Bibi-arusi wote, kwa sababu wanaishi katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Vema.

261. Tafadhali waweza (Vema, ni swali lile lile hasa) . . . Ufunuo 20:4, hizo ni roho za wale waliouawa kwa ushuhuda wa Kristo ambao hawangeabudu yule mnyama wala kupokea chapa yake juu (Ee, nafahamu lile wanaloendea sasa. Hili lililetwa tu kwangu, lililetwa kwangu kwa mkono) . . . kwa kuwa inasema waliishi na kutawala na Kristo miaka elfu? Kwa hivyo ni linatitiza, kwa sababu mateso ya Bibi-arusi, lakini ingekuwa kina nani na kutawala pamoja na Krisro miaka elfu? Je, wange—wa—wangukuwa wale 144,000?

La, la! Wao ni Bibi-arusi. Sasa, kumbuka, kumbuka, wao . . .

²²⁵ Ulisema, “Hali walikatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda . . .” Sasa, unasema, “Kwa yule—kutokumwabudu yule mnyama . . . Hakika! Unasema, “Mnyama yule angali atakuja.”

²²⁶ Mnyama yule amekuwako wakati wote; huyo mnyama ndiye aliyewalisha wao nyuma kule tunduni mwa simba, aliwalisha kule katika huo uwanja wa tamasha katika Roma. Huyo alikuwa mpinga Kristo, huyo alikuwa mnyama pale; alianzisha namna ya dini. Vivyo hivyo hasa—karibu kama mfululizo. Kanisa la Kirumi lilitolewa moja kwa moja toka kwa Biblia, ndiposa . . . Walipofanya hivyo, waliungana na kufanya dini na kuunda ka—kanisa la ulimwenguni kote kutoka kwalo na wote ambao hawangelisujudu waliangamizwa. Ona? Ndivyo.

²²⁷ Kisha hao waliokuwa katika sehemu hiyo ya Mwili ambayo ilikuwako wakati huo . . . Sasa, mwili umekua kama tu mti hata unafikia kichwani. Ona? Na wote, wafia imani wote, na walioteswa, na kadhalika . . .

²²⁸ Lakini Yesu ametupea amani ng’ambo hii ya mtoni, kama vile Yeye alivyowafanyia makabila ambayo . . . pale (ona?) hayakuvuka ng’ambo. Sasa.

262. Nimfanyieje? Yanipasa niendeleo ku-(Lo!) msaidia baba shambani? Nifanyaje...kupata ri—riziki kwa ajili ya...?... Naye ameweka sahihi la jina lake.

Naam, ndugu yangu...Ime—limeandikwa hapa. Sijui nani...Lasema, “Ndugu Branham...” Linaanza tu, “Nimfanyieje?”

²²⁹ Sasa, labda mvulana fulani kwa baba yake. Tazama, Ndugu yangu mpendwa, umebarikiwa ukimsaidia baba yako, kwa maana baba yako alikulea wewe ulipokuwa huwezi kujitunza mwenyewe. Na amri ya kwanza iliyo na ahadi, amri ya kwanza yenye ahadi; “Waheshimu baba na mama yako siku zako zipate kuwa nyingi duniani akupazo Bwana Mungu.” Ona? Naam, mtunze baba yako kwa njia yo yote uwezayo. Ona? Hakikisha ya kwamba yeye anapata kilicho bora zaidi.

263. Ulisema Kaini alikuwa mzao wa nyoka, bona Hawa kasema, “Nimempata mtoto mwanamume kwa Bwana?”

Naam. Heri ningoje hadi baada ya chakula cha kutwa kwa hili. Naam, nitangoja hadi baada ya chakula cha kutwa kwa hilo. Ee, hilo litachukua wakati mwingi kidogo kueleza hilo. Vema.

264. Mpendwa Ndugu Branham: Je, waweza kunieleza kifungu hiki, Isaya 2:2; “Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana—katika mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya mlima, nao utaninuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi.”

²³⁰ Naam; nilifanya hivyo, Jumapili mbili zilizopita. Ona? Nyu—nyumba ya Bwana itaimarishwa juu ya milima, na mataifa yote watauendea makundi makundi. Ule mkubwa...Kama huna... Kama una kanda juu ya *Yale Makao ya Bibi-arusi na Bwana arusi*, inaeleza hivyo hasa.

Jamani! Heri niache sasa hivi, kwa sababu.

Lo, jamani, ndugu, hatuwezi kuyamaliza haya yote hapa. Whiu!

265. Ndugu Branham, ime...(Hebu tuone hili lilivyo). Ndugu Branham, inaaminiwa mara kwa mara na wengi wanaofuata Ujumbe wako kuwa wewe u Masihi wa siku hizi. Je, ni kweli?

²³¹ La, bwana!

Twambie waziwazi, Ndugu Branham, inaonekana unasitasita kujitambulisha mwenyewe, nasi tunajua kwa huduma kama huu aliokupea Mungu, yapasa utambulikane atika Maandiko mahali fulani.

266. Nambari 2: Ulitwambia kusudi lako la kuenda Arizona mara ya kwanza. Ulitwambia sababu yake, na ikatimia, lakini hukutwambia sababu gani ulirudi kule tena.

232 Kwanza, mimi si Masihi! Ona? Masihi ni Yesu Kristo, lakini sisi tu “masihi wadogo,” kila mmoja wetu. *Masihi, Masihi* maana yake “mtiwa mafuta.” Na katika Yeye mnakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili; ndani yangu mna sehemu tu ya Roho Wake, yule yule aliye ndani yako. Nimepewa kipawa ku—ku—kujua mambo madogo madogo na kutabiri mambo. Hilo lanifanya mimi bado ndugu yenu. Ona? Mimi si—si Masihi; mimi ni ndugu yenu (ona?); mchungaji wa kundi. Na kama ningewaambia nilikuwa Masihi, ningekuwa mwongo. Ona? Nami sitaki kuwa mwongo.

233 “Sasa, sababu gani nilienda Arizona mara ya kwanza?” Mwfahamu hiyo. Nilienda kwa Jina la Bwana, kwa sababu nilitumwa kule na ono. Nilirudi mara ya pili kwa ajili ya kusudi fulani. Acheni hilo. Najua sababu ya kuenda huko; siwezi kusema kila kitu. Unapo—Shetani hajui—hawezi kulipata toka moyoni mwangu. Nikilinena, basi yeye aweza kupata hilo, lakini yeye—yeye hawezi kulipata linapokuwa moyoni mwangu. Nikisema, “Ngojea mpaka litakapotimia!” Kumbuka tu, shika kanda hii; nimeenda Arizona kwa ajili ya kusudi fulani. Tafadhali nivumilieni. Ona? Fanyeni tu yale ninayowaambia mfanye (ona?); fanyeni tu—tu nise mavyo mfanye. Ona?

267. Ndugu Branham, nina maswali kadha ambayo nitakuuliza—nitakayokuuliza. Nimesikia watu wakisema kuwa umewashauri watu kuuza vyao vyote... (Labda heri niache hilo pekee pia. Hebu tuone. Vema, umefika wakati wa kuondoka. Huenda sisi tutapata hili baada ya chakula cha kutwa, lakini ni—nitajibu hili au kujaribu niwezavyo. Sijui; nilikabidhiwa hili. Ona? Billy alileta tu kifurushi pale—pale mlangoni. Ona?) **Nimesikia watu wakisema kuwa umewashauri watu wauze manyumba yao na wakufuate kwenda Arizona au—au hawatakuwa katika kunyakuliwa kule. Je, hili ni kweli?**

234 Huo ni uongo. Ona? Enhee, enhee!

...au yatupasa kuuza manyumba yetu, au je, uliwahi kusema hivyo?

235 La, bwana! Sikusema hilo! Jambo ni kwamba, nimewashauri watu wasilifanye. Enhee, enhee! Kumbuka, mnakumbuka ndoto ya “Junie” Jackson wakati nilipoenda kule nje? “Junie” aliota kuwa huu... Wangapi wanakumbuka ndoto ile, na jinsi Bwana alivyotoa tafsiri: huo mlima mkuu, sisi tulikuwa tumesimama juu yake, na maandishi ya kale yaliyofutika pale; nami nilikuwa najaribu kuyafasiri, na singeweza. Nami—nilikuwa nawafasiria wao. Baada ya kufasiri hayo yote, kufasiri yote, ndipo nilinyosha mkono wangu pale na kupata (katika ndoto hii sasa) aina fulani ya—kama mtaimbo na kukata kilele cha mlima kisha nikaangalia mle ndani, na wote ulikuwa mweupe kama theluji, kama marmar. Lakini haukuwa umeandikwa juu yake, nami

nikasema, “Ninyi nyote kaeni hapa mkatazama humu ndani sasa, ninapoenda kule.”

236 Naye “Junie. . .” Hao wote wakaenda kule juu na ndugu wote na walikuwa wakitazama juu yake, lingine. . . Hawangeweza kufahamu; kasema, “Vema, wajua nini? Hata hayajaandikwa hapa, lakini hata hivyo yeye alikuwa akisoma upande wake wa nje. Mbona hayajaandikwa humu ndani? Hatuwezi kufahamu.”

237 Kisha akageuka akatazama, naye akaniona mimi nikielekea magharibi, kuelekea machweo ya jua, nikipanda juu ya mlima mmoja, mlima mwingine, upesi sana, nikipata tu. . . Kisha wao wakageuka na kutazama na kuona kwamba nimeenda; kundi kubwa mno lao waliondoka hivyo, nao walitaka kuenda *hivi* na kufanya *yale* baada ya mimi kuwaambia wakae pale. Kaeni pale, kaeni papa hapa; hapa ndipo mahali panapofaa.

238 Halafu nilipofanya hivyo, ndipo—nami nilienda vivyo hivyo; na kitambo kidogo baadaye, Malaika wa Bwana alinjia, kasema, “Nenda zako kule Arizona.” Nikasikia mlipuko huo ukilia na nikaenda kule, na ilikuwa nini? Mvulana yule aliota ndoto hiyo sahihi kabisa, na Bwana aliifasiri sahihi. . . Kumbuka, nilisema, “Naenda kule kwa ajili ya jambo fulani.” Na nilipoenda kule, ilikuwa zile siri za zile Muhuri Saba, ambayo ilikuwa imetiwa muhuri ndani ya mlima huo wa Bwana. Nikarudi moja kwa moja pamoja na kule kufunuliwa kwa zile Mihuri Saba. Ona?

239 La, haiwapasi kufanya hivyo. Ukitaka kwenda, hiyo ni juu yako. Hakika, si. . . Lo, sijali unaenda wapi, ila kufanya hivyo, ukidhani Bibi-arusi atanyakuliwa kutoka pale, umekosea.

240 “Pia nimesikia hili. . . Nime- (acha ni. . . nimekosea mahali fulani hapa. Hebu nione). . . kunyakuliwa kule. Je, hili ni kweli au yatupasa kuuza manyumba yetu, au uliwahi kusema hili?” La, sijapata kusema hayo. Sikuwahi. . . Mimi kila mara nimewapa watu shauri kukaa walipo na kuendelea kusonga mbele hata Yesu atakapokuja. Kama ninavyowaambia mara nyingi, hebu kanda hii iwe ukumbusho; na hili liwe ukumbusho siku hii; na neno langu liwe ukumbusho; sijawahi kamwe, wakati mmoja, kumwambia ye yote kamwe, kumfanya mwongofu wangu, sijajaribu kamwe kumfanya mtu fulani kuja kwa kanisa hili! Sijawahi kamwe. . . Kuhusu kuwaambia wao waache makanisa yao na kuuza vitu na mengineyo, Mungu ajua kuwa mimi kila mara nimewashauri watu kubaki Wakristo na kukaa walipo hata Mungu atakapowaita. Kila mtu ajua hayo. Kaa papo hapo! Lakini sasa, kuwaambia watu. . . Mtu fulani aseme, “Vema, nataka kwenda juu hapa. Nataka kuishi pale. . .” Enda ko kote unakotaka kwenda; hilo ni sawa. Sijali wapi unakotaka kwenda; sijali hayo.

241 Lakini sasa, kudhani kuwa. . . Ona, inafanya nini? Linaanzisha kundi la kidini lililojitenga (ona?), kisha naingia

mashakani. Kuna kundi nje kule sasa ambalo litaishi kwa misaada hivi punde. Na ndipo itakuwaje? “Tulikuja nje hapa kwa ajili ya kunyakuliwa kwa Bibi-arusi.” Hayo tu ndiyo magazeti yanangoja! Wanangoja kulipata watakapoanza kuishi kwa misaada na hawawezi kurudi manyumbani kwao. Ndipo watafanyaje?

²⁴² Vema, tulimfuata Ndugu Branham nje kule. Anadhaniwa kuwa... Nami sina hatia kabisa juu ya jambo hili. Hao ni watu wapendwa na wazuri, wao—wao wanajua nawapenda, na hata katika kosa lao. Nao... Vipi, wale... Wao... Nawapenda haidhuru. Ona? Nawapenda; wao ni watoto wangu; lakini wao hawatanisikiza, kile ninachojaribu kuwaambia. Ninajaribu kufanya jambo fulani katika Jina la Bwana, nao hawawezi kuniacha nifanye. Ona? Hakika waenenda dhidi yangu badala ya kuwa upande wangu. Wanafanya...

²⁴³ Si niliwaambia ujumbe ukiwahi kuhubiriwa, ningekuwa papa hapa maskanini humu; lo lote linipasalo kufanya, nitakuja humu na kulifanya, ningekuja hapa na kuwaambia kwanza, moja kwa moja toka humu maskanini? Hiyo ni ahadi yangu!

268. Pia, nimesikia kuna fundisho linaloendelea, kuwa kitabu ulichoandika miaka kadha iliyopita kuhusu ule mkate wa Uzima... Wanakifasiri kuwa yatupasa sote kuwa pamoja nawe, la siyo, hatutanyakuliwa.

²⁴⁴ Vema, kitabu kile kimekosea. Kitabu kile cha *Ule Mkate wa Uzima*, nakumbuka hilo sasa. Hilo lilikuwa kulisha kanisa ulimwenguni kote, kila mahali. Ona, shida yake ni... Naam, sasa, ninyi watu, ninyi wenyewe mu imara, lakini hamna budi kupata hilo. Hilo linafuata kila mkutano. Ile—ile...

Nilikuwa nasoma kuhusu Martin Luther hapa si muda mrefu uliopita, si kujilinganisha mwenyewe na hayo; lakini haya ni matengenezo tu vivyo hivyo kama hayo yalivyokuwa. Na—swali lilikuwa... Wale—wale—wale wanahistoria, wao walisema, “Ni jambo la ajabu kuwaza kuwa Martin Luther angeweza kubishana na kanisa Katoliki na kufaulu. Hilo lilikuwa jambo la kushangaza, lakini,” kasema, “jambo la kushangaza sana kuhusu Martin Luther halikuwa hilo. Ni jinsi yeye angeshikilia kichwa chake juu ya uzushi wote uliofuata mkutano wake na akadumu mwaminifu kwa Neno, wito wake-...” Ona?

²⁴⁵ La, bwana! Msiweke... Mwanamume au mwanamke anayeongeza lo lote kwa yale ninayosema, haamini yale nisemayo. Wao hawa... Wao husema... Wao...

269. Pia kuhusu jamaa hizi ambazo zimeuza na kuenda Sierra Vista, Arizona, ambapo wamefasiri toka kwa kanda yako inayoitwa (hebu kidogo) “Bethlehemu Ndogo”—“Bethlehemu Ndogo,” kunyakuliwa kutafanyika katika Arizona. Je, uliwashauri kwenda kule?

²⁴⁶ Hakika sikuwashauri. Walipoandika barua kuhusu hilo, mtu fulani juu hapa katika Connecticut au penginepo, nilijibu barua hiyo na kusema, “Mnachukua hatua mbaya mno mliyowahi kufanya maishani mwenu. Msifanye jambo kama hilo.” Ona, huwezi. . . Vema, kumbukeni tu, ninyi watu. . . Sasa, ninyi nyote mwajua kwamba siwaambii watu hawa kufanya hayo; ninawaambia wasifanye hayo. Lakini mwaona, hilo halina budi kufuata mkutano. Kwa nini watu wananiita mimi *Masihi*? Kwa nini watu. . . ? Inawapasa kubeba. . . Vema, mtu mmoja nje pale hivi majuzi alinionyeshwa, yeye alikuwa na kitu kidogo alichokuwa ana—anakiendeleza, alitaka watu wote wabatizwe katika jina langu. Hilo lingenifanya mimi mpinga Kristo! Lakini siyaungi mkono mambo hayo, na ninyi watu mwajua hilo. Lakini mwaona, hili lapasa ku. . . Hilo linatambulisha Ujumbe kuwa kweli.

²⁴⁷ Je, si wao walikuja na kujaribu kumwambia Yohana, yule—huyo aliyetangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, “Si wewe ni Masihi?”

Yeye alisema, “Mimi siye! Mimi hata sistahili kufungua viatu Vyake. Mimi hata sistahili kumtazama Yeye.” Ona? Lakini yeye alisema, “Yeye ajaye nyuma yangu. . .”

270. Sasa, Ndugu Branham, tunaacha nje jambo fulani? Watu hawa wanadai kuamini kila neno unalosema kuwa ni kweli. (Lakini hawaamini! Hawaliamini. Matendo yao yenyewe yathibitisha hawaamini). **Tafadhali hebu nijue jibu lako la moja kwa moja; ndiyo au la** (umelipata! Vema) **kuhusu mambo haya na kama ni kweli, tunataka kujitayarisha kwenda kujiunga na wengine wao kule—hao wengine. Nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali haya, kwa kuwa natarajia kuyasikia Jumapili hili, Bwana akikawia kuja.**

²⁴⁸ Lo, Jamani! Vema, Ndugu, Dada, na—natumai limefahamika (ona?) ya kwamba mimi, mimi si. . . Sasa, kama watu. . . Ee, hakika, mkitaka kuja Arizona kuishi. . . Na sasa, nitakuwa kule Arizona labda hii nusu ya kwanza ya mwaka. Itanipasa kurudi tena hapa. Itanipasa. . . ni—ninataka kukaa kule; watoto wana afya njema zaidi na kadhalika. Ni—ninataka kukaa kule kwa muda mchache, na nina kusudi. Kumbuka sasa, kwenye kanda, BWANA ASEMA HIVI, nina kusudi katika kufanya lile ninalofanya; mnajua ninalo; lakini siwezi kuwaambia ninyi hilo.

²⁴⁹ Sababu gani nawaambia ninyi msiuze nyumba zenu, mtakosekana, na mtajiangamiza. Msifanye hivyo. Sitakaa Arizona ila kidogo tu. Kwani? Siwezi kufanya hivyo sasa.

²⁵⁰ Nikiacha watu wakae kule na wategemee msaada, kipi kitatendeka? Basi hivyo ndivyo hasa madhehebu na hao wote wanatarajia. “Ahaa, niliwaambieni kilichowaongoza, shule nyingine ya manabii au kitu fulani!” Ona? Naam, hilo tu ndilo

wanalotarajia! Hata hivyo, watu hao, ninahusika nao; ijapokuwa hawajafanya yale niliyowaambia wafanye, nao wamefanya hasa. . . Mnasema, “Waache waende; wao—wao walifanya yale uliwaambia wasifanye!” Hilo haliko moyoni mwangu. Bado nataka kuwaendea. Wao ni watoto wangu. Huenda nikawapiga kidogo ninapowarudisha, lakini ni—lakini ni—nina hakika nitawatafuta. Na nitafanyaje nje kule?

²⁵¹ Walisema, “Tulikuja kufuata Neno.” Hata sina kanisa kule la kuwapeleka. Namna ya maskani watakayohudhuria kule ni ile ile mnayoiacha mahali pengine, labda mabaya zaidi. Ona? Na hawataenda kanisani haidhuru, nami sina kanisa la kuwahubiria. Ndipo nina wajibu kuwaondoa watoto wangu Arizona, ambapo. . .

²⁵² Nawauliza ninyi jambo fulani. Nimehubiri zaidi ya jumbe thelathini katika kanisa hili mwaka uliopita. Na kwa miaka mitano, nje, tangu nimekuwa Arizona, nimehubiri zaidi katika kanisa hili katika mwaka mmoja kuliko nilivyofanya katika miaka mitano wakati mwingine wo wote (hakika!), humu kanisani. Hiki ndicho kituo changu cha nyumbani; haya ndiyo kanisani. Hiki ndicho kituo changu cha nyumbani; haya ndiyo makao yangu makuu; hapa ndipo tumeimarika. Sasa, shikilia hilo mawazoni haijalishi itakuwaje. Sasa, kama mna busara, mtashika jambo fulani. Haijalishi itakuwaje, haya ndiyo makao yetu makuu, papa hapa! Na wekeni hilo mawazoni na mrejee kwenye kanda hii siku fulani, ambamo mlinisikia nikifanya unabii. Vema, kumbukeni hayo.

²⁵³ Kama mnataka—kama yawapasa kuondoka na kuja kanisani, msiende nje kule kulitafuta, kwa sababu mimi hata siko kule. Sina mahali pa kwenda; sina mahali pa kuhubiria. Hawawezi kunikubalia nihubiri katika makanisa yao. Mimi hata sina mahali, nami niliahidi watu wale nilipokuja kule. . . Wote walifadhaika nilikuwa naenda kule kujenga jengo kubwa—kunyonya makanisa yale. Lakini hilo silo kusudi la maisha yangu. Ona? Ni—ninawafanya watu waoko. Ni juu yao. Kama Msamaria yule alivyoshuka chini kule na kumpeleka mtu yule mkahawani, ndipo akawaacha wao wamshughulikie tangu hapo na kuendelea. Mimi siko hapa kuvunja makanisa, mimi niko hapa kuwapeleka waongofu kwa Kristo! Ona? Na linanifanya nikose kufahamika kati ya watu (ona?) wanapo—wanapofasiri kwa njia yao wenyewe na si—na—hawasemi ninayosema. Ona?

²⁵⁴ Je, hamkumbuki ono lile? Wangapi wanakumbuka ndoto ya Junior Jackson? Na hayo yote yalifuatana tu vivyo hivyo. Ilikuwa nini? Kaeni hapa hadi niende kule! Ona? Na kupata tafsiri na kurudi.

²⁵⁵ Sasa, nina jambo lingine moyoni mwangu ambalo nimeonywa na Bwana kufanya, mwenendo fulani kuhusu maskani haya, na kanisa hili; ambapo yanipasa kwenda kule

au mahali fulani kwa muda mfupi. Ni kwa kusudi fulani, kusudi kuu, kusudi ambalo ninyi nyote hamnjui lo lote kulihusu. Lakini kumbukeni, mimi siko “kuzurura” hapa na pale, kwa sababu ninafanya kama ninavyofanya. Ninafanya kazi katika mapenzi ya Bwana, kwa kadiri nijuavyo jinsi ya kufanya katika hayo. Ona? Hiyo ndiyo sababu kama mnaamini yale ninayosema, basi fanyeni yale ninayosema mfanye (ona?), ndipo nisikizeni na niaminini kama ndugu yenu. Kama mnaniamini mimi kuwa nabii, msifasiri kwa kosa maneno yangu!

²⁵⁶ Kama kuna lo lote, ole wangu, kama kuna cho chote Mungu ameniambia na mwapaswa kujua, Mungu ajua ningekwambieni vivyo hivyo! Na usiongeze kwalo wala kuondoa kwalo; lifanye tu jinsi nilisemavyo (ona?), kwa sababu ninawaambia toka kwa moyo wangu bora zaidi nijuavyo. Ona? Aminini tu hayo. Chu—chukueni tu—yale ninayosema juu yake, na myaache tu hivyo. Vema.

²⁵⁷ Kwa hivyo sasa, yanipasa kuwarudisha hao watoto hapa wapate kula. Wako chini kule jangwani wakiunia kwa njaa.

²⁵⁸ Mhudumu fulani alinjia hivi majuzi, kasema, “Ndugu Branham, wanaunda dhehebu baya mno kule chini niliyowahi kuona.” Kasema, “Kila mmoja wao, kila asubuhi, wanaondoka, nao walisema hawatafanya kazi, kunyakuliwa kumekaribia sana.” Hawatafanya kazi. Vema, hilo laonyesha tu hata hamwelewi. Ona? Vema. (Kanda hii inaenda chini kule!) Kwa hivyo, naam, bwana! Yawapasa mpate funzo toka kwa chungu, Biblia ilisema, mwajua. Wasipofanya kazi basi na wasile. Kwa hivyo hilo ndivyo lilivyo hasa.

Hapa—kuna—hapa, nilichukua tu mojawapo wa hili.

271. Je, (Sijui. Ona, ni—ni tofauti—ni mwandiko tofauti na huu mwingine. Inawaonyesha tu, nadhani kuna karibu manane au kumi ya ndani mle. (Ona?) Je, kanisa bora—je, lile kanisa kamilifu sana litakuwepo katika Tucson, Arizona? Nataka kuwa katika mapenzi makamilifu ya Mungu. Je, tuhamie Tucson?

²⁵⁹ Huu haufanani kamwe na mwandiko ule mwi—mwingine. Ni...ni...Tazameni tu hapa; nitawaonyesha mangapi yaliyoko kwa hilo swali moja. Si...Si singeyapata, nadhani. Hapa kuna—hapa kuna...Ninayo mengine yametiwa alama juu hapa, “Nitawajulisha.”

272. Ndugu Branham: Tafadhali... (Hebu tuone). Kwa kuwa tunajua kuwa wewe u nabii, na kwa wakati tunaishi, uta—na nabii wa wakati tunaishi (Hivyo ndivyo lilivyo.), utakuja wakati ambapo watu wa Mungu watapaswa kukimbilia Arizona pamoja nawe? Kama ndivyo, utatwambia ni lini wakati huo ufikapo?

²⁶⁰ Hakika nitafanya hivyo. Nitawaambia. Nitawaambia. Sasa ona, kuna miandiko tofauti miwili, watu wawili mbalimbali.

Ona? Kuna moja limeandikwa kwa mkono, na kuna lingine. Ona? Haina budi hilo ndilo, lililo kwenye nia ya kanisa. Ona? Vema, hebu na tutatue hili. Hebu na tuone kama ningepata . . . Hebu tuone.

273. Ndugu Branham . . .(Lingine ndilo hilo, tofauti kabisa.) **Ndugu Branham, wengine walikufahamu wewe kusema katika ujumbe wako wa “Makao Yajayo ya Bibi-arusi na Bwana arusi” yangukuwa** (La, hili ni tofauti)—**kuwa maili elfu moja na mia tano toka kwa maskani—mraba—mia saba kila upande** (Yaani, maskani yakiwa papo hapo katikati ingekuwa mia saba kila upande—ingekuwa maili elfu moja na mia tano. Enhee?)—**kila upande. Je, hii ni kweli? Naishi nje ya eneo hili; je nihamie ndani yake?**

²⁶¹ La, mpendwa, usifanye hivyo. Tazama! Sasa, mwaona ni rahisi vipi kwa watu? Wangapi walikuwa hapa nilipohubiri ujumbe huo? Nilisema hayo nilipokuwa napima Yerusalemu Mpya, kuwa ingekuwa maili elfu moja na mia tano mraba. Nilisema ingekuwa kama toka Maine hadi Florida, na maili mia sita magharibi ya Mississipi; hiyo ingekuwa maili elfu moja na mia tano mraba. Nilisema Mji ule, kwa maoni yangu, utakuwa papo hapo kwenye ardhi ambapo nabii Ibrahimu alitafuta Mji huo, wakati hakutakuwepo bahari tena. Biblia ilisema kuwa hakutakuwepo bahari tena ambapo robo tatu ya nchi imo majini. Na hakutakuwa na bahari tena; kwa hivyo basi, hautakuwa Mji mkubwa sana umekaa mahali kama hapo. Naamini utakuwa katika mahali pale padogo ambapo wanazozania sana, na alikozaliwa Mungu, kule Bethlehemu. Naamini itakuwa pale pale katika Palestina kule, ambapo patainuka toka ardhini papo hapo na kuwa mlima huo.

²⁶² Lakini, rafiki mpendwa, haina uhusiano wo wote na maskani haya. Ona? Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Paulo, watakatifu wote, waliokufia kote ulimwenguni, waliteketezwa, walizamishwa, waliliwa na simba, na mengineyo; nao watatoka katika kila ufa, mwanya, na pembe ya ulimwengu. Natumai niko kule. Sijui nitakuwa wapi, lakini ko kote kule, kama niko kwa kundi hilo, hakuna lo lote liwezalo kunizuia kuwa kule! Ona? Nami si lazima niwe mahali po pote maalum. Mahali pekee nipaswapo kuwa ni kuwa katika Kristo, kwa maana wale walio katika Kristo ndio Mungu atakaokuja pamoja nao. Sijui ni wapi, Yeye atawaleta . . . Nizike katika Yesu.

²⁶³ Tazama manabii hao nyuma kule. Walijua katika hisi zao, sasa, kuwa ufufuo wa kwanza, yale malimbuko, yangukuwa katika Palestina. Ibrahimu alinunua mahali fulani, naye—si—naye akamzika Sara. Naye akamzaa Isaka. Isaka alizikwa kando ya baba yake katika Israeli—katika Misri, akarudishwa Palestina. Na ndipo, Yusufu pia alikufia chini kule. Nao walirudisha mifupa ya Yusufu, kwa sababu yeye alisema, “Fanya . . .” ilimpasa Yusufu amwapie—Yakobo, kuwa yeye

hangemzika chini kule, lakini amrudishe tena katika ile nchi ya ahadi. Yusufu alisema, “Wakati mmoja Bwana Mungu wenu atawazuru. Hebu ni—mifupa yangu itwaliwe ikazikwe pamoja na baba yangu.” Nao walifanya hivyo, kwa sababu, wakiwa manabii, wao walifahamu kuwa malimbuko ya ufufuo yangukuwa katika Palestina.

²⁶⁴ Sasa, Biblia ilisema . . . Na kama mnaniita nabii, sisemi mimi ni nabii; lakini mkiniita mimi hivyo, mkiniita mimi hivyo, kumbukeni, nawaambia katika jina la nabii (ona?)—katika Jina la nabii, ufufuo ule na kunyakuliwa vitakuwa ulimwenguni kote! Haijalishi uko wapi, saa hiyo ifikapo, utanyakuliwa kumlaki! Hivyo tu! Hakuna lo lote litakalokuzuia, haidhuru uko wapi. Nami natumai tu kuwa nitakuwa kule, mmoja wao. Nasadiki na kutumai katika Mungu kuwa nitakuwa mmoja wao na kila mmoja wenu atakuwa katika—atakuwa pale pale.

Sasa, tuna wakati kwa lingine? Ndipo itakuwa tu (ona?)—karibu tu saa saba.

274. Ndugu Branham: Mimi na mke wangu tulitengana. Yeye ananishitaki apate talaka. Yeye si Mkristo, nami naamini Ujumbe na nataka yeye aokoke (Si hilo ni nzuri? Huyo hakika ni roho wa Kikristo. Ona?) na naamini. Yanipasa nifanyeje? Sisi pia tuna wavulana wawili. (Ameandika majina yao.)

²⁶⁵ Ndugu, tazama, hebu nikwambie, yeye anaenda kukushitaki apate talaka; huyo ni Shetani. Ona? Hapaswi kufanya hivyo, lakini kama wewe u Mkristo na hujafanya lo lote ulimwenguni kumzuia mwanamke huyo, basi ni Shetani anayefanya hilo. Yeye anajaribu tu kukuvunja moyo.

²⁶⁶ Sasa, kama mwanamke huyo ni mmojawapo wa wateule wa Mungu, atamjia Yeye. Kama siye, yeye hastahili kuhuzunikiwa. Halafu kama linafanya . . . Kama ukiwa na huzuni mwingi utadhoofisha afya yako, na hilo ndilo Shetani analotaka kufanya. Yeye anafanya kazi, kwako. Kwa hivyo weka tu jambo lote kwa Mungu na endelea kumtumikia Mungu kwa furaha uwezavyo kuwa. Mungu atayashughulikia mengineyo. “Wote anipao Baba watakuja kwangu.” Piga magoti; nitaomba pamoja nawe au lo lote. Nitaomba kuhusu jambo hilo. Sema tu, “Bwana Mungu, nampenda mke wangu, yeye ni mama ya watoto wangu,” (kama ndivyo alivyo) na useme, “Ni—ni—ninaweka tu jambo lote Kwako, Bwana. Nawataka waoko, Wewe wajua nataka hivyo; lakini siwezi kwenda mbali zaidi. Yeye ataniacha haidhuru. Sijafanya lo lote; kama nimefanya, nifunulie; nitaenda nilirekebishe. Nitafanya cho chote.” Ndipo liweke kwa Bwana na liache basi, liache tu. Endelea kuishi vivyo hivyo kama—kama kwamba hamna cho chote kilichofanyika. Na Mungu atayashughulikia hayo mengine.

275. Sasa: Ndugu Branham, mambo gani haya kuhusu watu (Ee, tena!) kuenda Arizona? Lieleze. Ndio huo mwandiko mwingine. Ona, Ona?

Vema, tumekwisha eleza hayo (ona?), jinsi hilo lilivyo.

276. Ndugu Branham, je, Bibi-arusi atapatia kwa mateso kama vile lile kanisa la kwanza la mitume lilivyopitia?

²⁶⁷ La, nilieleza tu hayo dakika chache zilizopita. La, jambo linalofuata ni kunyakuliwa sasa. Kumbuka, sisi tuko kwenye nchi ya ahadi; tuko mpakani. Mwafahamu ile safari ya Israeli?

277. Je, ni halali kwa—kutumia namna yo yote ya kupanga uzazi?

²⁶⁸ Heri niache hilo hadi jioni hii (ona?), kwa sababu ni... ninataka ku—ninataka kunena jambo fulani kuhusu hilo.

278. Ndugu Branham, ni... (ninaangoja tu dakika zingine 3 zaidi nikiweza. Hebu nipate kitu fulani kifupi hapa labda.) Siwezi kujitolea kabisa kwa Yesu. Je, nina pepo?

²⁶⁹ Hebu tu nitumie wakati wote uliobaki kwa hilo pale. Huwezi kujitolea kwa Yesu? Hawa... Ona, sijui ni mwanamume au mwanamuke; siwezi kutambua ni nani. Mungu ajua hilo.

²⁷⁰ Huwezi kujitolea kwa Yesu. Mbona? Kuna shida gani? Kama wewe u mwanamke, si inakupasa kujitolea kwa mumeo kuwa mke, kujitolea kwa cho chote ulicho? Mwanamke mdogo ulipoolewa, mwadilifu, ulipigana maishani mwako mwote kubakia mwadilifu, lakini siku moja ulipata mwanamume uliyempenda. Ulikuwa wake kabisa. Mambo ambayo ungepigana nayo maishani mwako na kujaribu kuishi msafi, na dhahiri, na mwadilifu; sasa, unatoa kila chembe yake kwa mwanamume mmoja. Sivyo? Unajiweka mwenyewe kabisa mikononi mwake; wewe u wake. Yote uliyoshikilia kwa ustahifu, na uadilifu, na kila kitu vivyo hivyo, sasa unayakabidhi mwanamume fulani, kwa sababu unajitolea mwenyewe kwa mwanamume huyo. Huwezi kufanya vivyo hivyo kwa Yesu Kristo? Jitolee tu hivyo—vyote nilivyo, nia yangu yote, mawazo yangu yote. Bila shaka.

²⁷¹ Sidhani una pepo; nadhani pepo ndiye amekujaza mawazo hayo, akijaribu kukufanya wewe udhani huwezi kujitolea kwa Mungu. Wakati... Hebu nikuonyeshe kitu fulani. Mbona utake kujitolea Kwake? Kwa sababu kuna kitu fulani nje kule kinachokuita ujitolee. Ni ishara nzuri sana kuwa yakupasa ujitolee mwenyewe.

²⁷² Sasa, yote ufanyayo, Ndugu au Dada (huenda ni kijana au mzee, ye yote yule), ulisema... Hawawezi kujitambua wenyewe ili waweze kujitolea kabisa. Jitolee mwenyewe tu. "Bwana, kuwaza kwangu, yote niliyo, ni—ninataka kukupa Wewe. Maisha yangu, nayatoa kama maisha ya huduma. Nichukue, Bwana, na unitumie jinsi nilivyo." Na ni jambo rahisi sana; natumai

kanisa hakika linge. . . Naamini kama—kama—kama maskani hayo sasa yakifaidika kwa maswali haya. . . Je, mnayapenda? Vema. Yatasaidia kidogo.

273 Sasa tazama, juu ya hili, kama kanisa lingeliza tu mambo haya (mwaona?), wangeuliza mambo haya: iwapo wanapaswa kufanya *hili* au kufanya *hilo*, na kila kitu, nitajaribu kufanya vema niwezavyo. Kama nimewashauri vibaya, sikutaka moyoni mwangu kufanya hivyo. Kama nilisema lo lote baya ili kushikilia tu mawazo yangu mwenyewe na kadhalika, bila—kujua—kujua ni kosa kufanya hilo au kuwaambia ninyi hilo, ningekuwa mnafiki mchafu. Naam. Lakini toka moyoni mwangu, kama nimekosea, Mungu ajua (ona?) nimefanya yote yaliyo ndani yangu kujibu maswali yenu.

274 Na kwenu wahudumu katika nchi ambamo kanda hii itaenda, sikusema haya kuwaudhi ninyi. Nilisema kwa sababu nawapenda. Ona? Nami hakika, kwa moyo wangu wote. . . ni. . . Sasa, mimi sijaribu kufanya kazi kuwaonyesha ninyi kuwa—kuwa ni—ninajua kitu fulani ambacho hamjui. Hilo silo, ndugu yangu. Mimi ninafanya tu hilo kwa sababu nawapenda ninyi, nami—ni—mnanipenda mimi, naamini.

275 Vipi kama uliniona mimi kule mtoni katika mtumbwi mkuukuu, nje hapa kwenye mto huu, karibu ambapo tuliko sasa, hapa maskanini, Mto Ohio; na mto ule ungejaa na kufurika; na maporomoko ya maji yalikuwa tu chini yangu. Na unajua kuwa mtumbwi huo hautavuka maporomoko hayo ya maji; hauwezi kuvuka. Na mimi hapa nimeketi nje pale kichwa nyuma, huku nikiimba, na kustarehe, na kuzidi kuteremka chini—nikielea kuelekea huko chini—kwa taratibu chini ya mto ule; na unajua chini pale naenda kuvunjikavunjika. Kama unanipenda mimi, ungalipaza sauti, au ungeruka mtumbwini, na kukimbia nje pale, na kunigonga mimi kichwani na kitu fulani, uniingize. “Ndugu Branham, umerukwa na akili? Umerukwa na akili, maporomoko ya maji yako papa hapa!”

276 Nami nilisema, “Ee, nyamaza! Niache!” Na ungali unanipenda haidhuru. Ungefanya cho chote ulimwenguni; ungenishika. Kama ingekupasa ku—kama ingekulazimu kulipua mtumbwi wangu, ungeniondoa nje kule, kwa sababu unanipenda; unajua litakalotendeka.

277 Na ndugu, najua hilo ndilo litakalotendeka kwa dhehebu hilo. Halitastahimili mkondo. Ona? Mnaenda moja kwa moja hadi kwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni; na sasa, yakupasa ulichukue au kutoka jinsi tulivyo sasa. Kwa hivyo, vivyo hivyo hasa, yakupasa ufanye chaguo lako. Na si—sikusudii kuwa. . . Ningependa kulipua mtumbwi hao, vema, ningependa kufanya lo lote ambalo ningeweza, si kuwadhuru, ndugu, lakini kuwaamsha kuwa mumekosea. Msifanye hivyo!

278 Na huu ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, hakuna mtu kwenye uso wa dunia ambaye angelaumu huo kwa Maandiko. Hakuna mtu awezaye kuulaumu huo. Hakuna hata Andiko moja. . . Ninyi watu, ninyi ndugu—ninyi ndugu, kumbukeni, kumbukeni tu, tafuteni katika Biblia; pateni mahali pamoja ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa katika Agano Jipya (hawakubatizwa katika la Kale, lakini katika Agano Jipya)—ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa vingenevyo isipokuwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo; ndipo njooni mnyonyeshe mimi. Au nendeni mkachukue kitabu cha historia ambapo waliwahi kubatiza kwa mamia ya miaka ya kifo cha mtume wa mwisho. . . Kanisa Katoliki ndilo lililoanzisha ubatizo huo. Katekisimu yao yasema vivyo hivyo, wakitumia Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

279 Kwa mahojiano na kasisi, papa hapa kwenye kanisa liitwalo Sacred Heart, aliniambia vivyo hivyo. Kasema kanisa Katoliki lilikuwa likibatiza hivyo, nilipomwambia nilibatiza huyu msichana Frazier, wakati askofu alitaka kujua. Yeye alisema, “Waweza kuapa kwa matamshi haya?”

Nilisema, “Siapi kwa vyo vyote vile.”

Yeye alisema, “Askofu anakutaka ufanye hivyo!”

280 Nilisema, “Askofu apaswa kuchukua neno langu au asiliamini, cho chote atakacho.” Ona? Nilisema, “Biblia ilisema usiape kwa vyo vyote vile.”

Naye alisema, “Vema, ee. . .” Yeye alisema, “Ile. . .”

281 Nilisema “Nilimbatiza kwa ubatizo wa Kikristo katika maji mengi, nilimzika majini mwanzoni mwa Barabara ya Spring kwa Jina la Bwana Yesu Kristo.”

Na kasisi yule alipoliandika, yeye alisema, “Hivyo ndivyo kanisa Katoliki lilikuwa likibatiza.”

Nikauliza, “Lini?”

Yeye akasema, “Katika siku za mitume.” Nilisema, “Unawaita wao Wakatoliki?”

Yeye akasema, “Hakika, wao walikuwa vile.”

282 Nikasema, “Basi mimi ni Mkatoliki bora kuliko mlivyo ninyi. Nafuata mafundisho yao.” Naam. Ona, ona? Wanadai hilo, lakini sivyo.

283 Kanisa Katoliki liliimarishwa kule Nikae, Rumi, chini ya Konstantini, wakati kanisa na taifa na—viliungana pamoja, na—na taifa lilipewa mali, na mambo kama hayo; hakika wao walidhani walikuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Wao walidhani wameingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Huo ulikuwa utawala wa Shetani wa miaka elfu. Ndipo hasa. Msiamini upuzi huo. Naam, bwana!

²⁸⁴ Sasa, lakini...Ndipo walipounda—au badala ya kuwa na sa—sanamu, wao walishusha—wao walimshusha Venus wakamweka Mariamu; wakamshusha Jupiter, wakamweka Paulo au Petro. Papo hapo kule—kule Vatikani, papo hapo kule—kule Rumi sasa, katika Jiji la Vatikani, sanamu ya futi kumi na tisa ya Petro, wanadai wamebusu vidole hivyo vitatu vya mguu au miguu ya sanamu hiyo hata vikamalizika. Ona? Na kila kitu ni...

²⁸⁵ Kote chini...Tulienda kanisani, mimi pamoja na Billy, asubuhi moja kule, tulienda kupitia kwa orofa ya chini kule ambapo wanazika watawa wote na watu kama hao na kuacha mifupa yao ioze katika vumbi hili—mfupa mmoja unaoza toka kwa mwingine juu pale—na ndipo wanaitwaa hiyo mifupa wakatengenezea vyombo vya kutoa nuru vya mifupa ya mikono ikijitokeza nje *hivi*, na fuvu; na hao watu wanaoingia mle wamesugua fuvu zile zikawa nyeupe, wakijaribu kupata baraka toka kwa fuvu za hao watu wafu. Ni namna ya kuabudu mizimu. Ona?

²⁸⁶ Basi hapo ndipo inaanzia papo hapo, katika Rumi, na hapo ndipo yalipo yale makao ya mnyama, na toka humo anajitokeza yule mama kahaba wa kale. Na binti zake ni makahaba vivyo hivyo kama yeye alivyo, kwa sababu yeye aliupea ulimwengu wote kikombe cha ghadhabu yake—kikombe cha ushuhuda wake, ambacho kilikuwa kimechanganywa ndani mle na nyongo ya ndunia. Naye alikuwa na ushuhuda wake. Yeye alisema, “Naketi kama bikira, nami—naketi kama mjane (nakusudia hivyo), na sina haja ya kitu;” naye hajui yeye ni mwenye mashaka, mchafu, kipofu, maskini, na hajui. Naam. Na hilo laenda kwa kanisa Katoliki pamoja na kila dhehebu la Kiprotestanti! Lakini katika mchafuko huo wote nje kule, kuna watu wapendwa wanaompenda Bwana kwa moyo wao na nafsi na nia. Nao wanadhani wako sahihi. Wao wanadhani wanatenda mema. Mungu ndiye atakuwa Hakimu Mkuu.

²⁸⁷ Kwangu mimi, kama Mungu atahukumumu kanisa kwa ulimwengu—kanisa Katoliki linasema hivyo—ndipo nilimwuliza mtu huyo aliyekuwa akinihoji...Yeye alisema, “Mungu atauhukumumu ulimwengu kwa kanisa.”

Nilisema, “Lipi?”

Yeye alisema, “Kanisa Katoliki.”

²⁸⁸ Nilisema, Kanisa Katoliki gani? Yanatofautiana na mengine. Kanisa gani? La Kiyunani au la Kirumi? Au atahukumumu kwa lipi? Kama Yeye atahukumumu kulingana na kanisa Protestanti, gani? Methodisti, Batisti, Lutheri, Pentekoste; atauhukumumu kwa lipi? Biblia ilisema Yeye atauhukumumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, na Yesu Kristo ni Neno. Kwa hivyo kwangu, ni Neno la Mungu atakalotumia kuuhukumia Ulimwengu. Naam, naamini hukumu zimo duniani sasa, nami naamini...Hebu tujitahidi kwa mioyo

yetu yote kuepuka ghadhabu ya hukumu ya hasira ya Mungu itakayomiminiwa juu ya ulimwengu huu usioamini; na hakuna njia yo yote kwao ku—kuepuka.

289 Wokovu hautakuja kamwe, kamwe, kamwe ulimwenguni tena. Wamevuka mpaka wao kati ya neema na hukumu. Kuna . . . Huenda mkamweka Abraham Lincoln katika kila jimbo Marekani, na haitageuza hili kundi la akina “Ricky” na “Elvis” wamrudie Mungu.

290 Unapooona katika gazeti hili (Ninalo. Nitawaletea jioni hii mkitaka kuliona usiku huu), ambapo kanisa la Presbiteria (huenda wengi wenu mmeliona)—kanisa Presbiteria likishiriki misa au kushiriki kwa—kwa—kushirikisha sakramenti na dansi ya rumba. Mchungaji akisimama pale akipiga makofi hivyo; nao walikuwa wakipiga zile hatua za kule kusulubishwa kwa “makelele na ghasia” kama dansi ya rumba katika kanisa Presbiteria.

291 Na wakati hili kundi linalojiita Beatles, lenye utovu wa uadili, likipiga mayowe, chafu, ambalo limekuwa duni kuliko mwanadamu hata wakataka kuwa mdudu . . . Walikataa mapatano ya dolla elfu mia katika St. Louis majuma machache yaliyopita; hawangecheza kwa hizo. Wanakuja hapa, kundi ndogo la Waingereza wafidhuli pale na nywele zikipepea machoni mwao. Na sasa, wana dini yao wenyewe wanayoanzisha. Utayaona katika gazeti liitwalo *Look*. Ona?

292 Ee jinsi ulimwengu huu unavunda. Hakuna tumaini kwake kwa vyo vyote vile; wameruka mpaka kati ya—kati ya kuwaza na busara, tusiponena kati ya wokovu.

293 Mwanadamu hata hawezi kuhukumu. Hatuna tena watu kama wale tuliokuwa nao. Yuko wapi Patrick Henry? Yuko wapi Abraham Lincoln? watu wanaoweza kusimamia dhana thabiti.

294 Yuko wapi mtu anayeweza kusimama na kuwafanya hawa wanawake wenda wazimu nje hapa, wanaojivua nguo wenyewe—na kule nje mbele ya wanaume hawa; kisha—kisha wanakimbia kule nje kama kundi la wanawake watembea uchi, halafu kuwapeleka wavulana ambao wanawatusi korokoni . . . Fikira zenu ziko wapi? Busara ni nini? Yeye akijiweka mwenyewe nje kule, kujiachilia aende kama mbwa. Naam, bwana! Kama mwanamke huyo hata . . . hana adabu bora kuliko huyo . . . Iko wapi sheria ambayo ingezuia hilo?

295 Papa hapa Louisville, Kentucky, majuma mawili yaliyopita mwanamke yule alipo—akijaribu kufanya ku—kufanya jina lake liandikwe gazetini, alivaa bikini ya plastiki, akatembea nje pale toka Hoteli iitwayo Brown; na polisi alijaribu kumsimamisha, naye hangesimama; alimchekelea polisi huyo. Na polisi yule alimfyatulia risasi asimame; naye alimwingiza katika motokaa na kumfanya amkute katika kituo cha polisi kwa ajili ya mavazi

mazinifu na mambo kama hayo, naye alienda akamwona... Wajua lile walilofanya? Walimfukuza kazi yule polisi.

²⁹⁶ Mungu asaidie taifa lililooza hivyo! Huwezi kuendelea usipofanya mabaya. Huenda tusiendele mbebe, bali tunaweza kwenda juu; na huko ndiko tunakotarajia. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁹⁷ Bwana Yesu, hebu na Mchungaji mkuu aje na atuondoe kwa haya, Bwana. Tunamngoja Yeye. Tunangoja saa hiyo. Tunapooona ulimwengu umechafuka hivyo, Wewe ulisema ingekuwa hi—hivi. Manabii Wako wakuu walitabiri kuwa wakati huu ungekuja. Tunaamini manabii, Bwana; tunaliamini.

²⁹⁸ Na sasa, twaomba, Mungu, kuwa wewe utatupea manabii kutufasiria Neno hili, kusudi tupate kujua kama sisi tu sahihi au tumekosea. Twaona manabii wa uongo wakizuka; wako nyikani, Salt Lake City, sehemu zote za taifa, aina yote ya majangwa, na vyumba vyote vya siri vya kila aina, kila aina ya Baba Miungu, na kadhalika, kila mahali.

²⁹⁹ Kuona hao maskini ndugu weusi, na kina dada nje kule sasa; walitaka kuchanganyikana. Mara tu walipolipata... Naam; wapaswa kuwa nalo; wao ni ndugu na dada. Sasa, walipolipata, wako vibaya zaidi kuliko walivyokuwa. Yaonyesha ukomunisti unalichochea. Ee, Mungu, maskini watu hao waweza kuona hilo? Hilo limefanywa tu... Vema, halina budi kufanywa, Bwana.

³⁰⁰ Njoo, hilo ndilo tunalotaka. Njoo tu, Baba. Sisi tunangoja. Njoo, Bwana, tuchukue chini ya mikono Yako. Tusamehe dhambi zetu. Hakuna—hakuna haki tena katika ulimwengu huu. Kitu kimoja kinapinga kingine, na huku umeliwa sana na wadudu hata una—hakuna uhai ndani yake. Wewe ulisema mwili wote tayari umekuwa kama vidonda vilivyooza. Kweli, kila meza imejaa matapiko. Ulisema, “Nitamfahamisha nani habari hii? Ni nani nitakayemfanya afahamu siku hiyo?” Meza yote ya Bwana imejaa matapiko. Tunaiona, Bwana. Wakati huo umeefika. Tusaidie, tafadhali.

³⁰¹ Mungu mpendwa, mengi ya maswali haya hapa kuhusu kuja kwa watu Arizona. Ee, Mungu mpendwa, hebu hao watu wapendwa na wa dhamani... Wao wataisikiza kanda hii huko. Hebu wao wajue ya kwamba mimi si mtawala wa mabavu kuwaambia watakoishi, ama watakofanya. Hebu wao na wafahamu hayo dhahiri. Iwapo wanaipenda nchi hiyo, vivyo hivyo nami pia, hebu wawe huko, Baba. Bali wanapofundisha ya kwamba kunyakuliwa hakuna budi kutokea kule, na kule pekee, ama hawana budi kuwa pamoja nami, maskini mtu mwenye dhambi, mchafu na asiyestahili, aliyeokolewa kwa neena ya Mungu—hawana budi kuwa karibu nami... Bwana, nataka kuwa karibu—nataka kuwa karibu na Paulo; najua ya kwamba yeye anaenda. Na Petro, na Yakobo, na Yohana, wao wako kule Palestina wamezikwa mahali fulani pale. Najua

nitaenda pamoja nao iwapo uliliandika jina langu katika kile Kitabu tangu kuwekwa misingi ya dunia. Nitakuwa kule. Nami naomba, Mungu, ya kwamba kila mmoja wao atakuwa kule. Nisaidie, Bwana, kuwakusanya wote warudi mahali fulani, ambapo wanaweza. . . Wao wanataka kusikia ujumbe kutoka kwa waalimu hawa mashuhuri kama Ndugu Neville, na Ndugu Capps, na—na ndugu hawa wengine wote hapa: “Junie,” na Ndugu Ruddel, na lo, J.T., na hao wote: Ndugu Collins, na Ndugu Beeler, na Ndugu Palmer, na. . . Mungu, naomba ya kwamba utawajalia hili. . .

Hebu—hebu—hebu wao waje hapa ambapo watausikia kweli, iwapo wanataka kuusikia, si kukimbia kule katika lile jangwa. Wao wanajaribu kufanya yale hasa Maandiko haya yaliwaambia wasifanye. “Lo, ako jangwani; msiamini! Lo, ako nyumbani; msiamini!” Bwana, ninajaribu niwezavyo kuwaonya, bali yote inaonyesha ya kwamba ile saa imekaribia sasa. Mawingu ya jioni yanashuka.

³⁰² Naomba kwa ajili ya neema, Bwana. Nirehemu; nisaidie mimi. Inanifanya kuwa na wasiwasi, Baba. Naomba ya kwamba utanisaidia. Si—sitaki kutia muhuri maisha yangu. . . Kazi yangu yote hapa ingekuwa huku nje kama mshupavu wa dini fulani kwongoza kundi fulani ama dhehebu kule jangwani mahali fulani. Usiache jina langu liishie hivyo, Bwana. Nilipigana vikali kwa sababu hii. Mimi ni mwaminifu kwake niwezavyo kuwa. Mungu, usiache hayo yatendeke. Nisaidie kwa njia fulani. Sijui la kufanya; ninakutegemea Wewe, bali unisaidie. Nitafanya cho chote uniambiacho nifanye. Mimi ni mtumishi Wako; hawa ni watoto Wako. Bwana, hawa. . . Wengi wa watu hawa, tisini kwa kila mia, Bwana, ni imara sana. Wao wanaamini; wao wanajua; wanafahamu. Wanajua si mimi; bali najua mambo haya hayana budi kufuata kila ufufuo, na huu si huru kwake. Kwa hivyo naomba ya kwamba utatusaidia sasa.

³⁰³ Tusaidie tunapoenda kupata chakula kidogo cha kutwa leo, Bwana. Bariki ushirika wetu pamoja. Tukasanye hapa pamoja mapema adhuhuri ya leo. Wengi wao itawabidi kwenda nyumbani sasa, Bwana. Hawana budi kwenda ma—makwao, nami naomba ya kwanba utawasaidia. Hebu waweze kwa njia fulani, Bwana, kupata ukanda huu na kusikia maswali yao yaliyosalia. Huenda ikawa yao hayakujibiwa. Naomba ya kwamba utawasaidia, Bwana.

³⁰⁴ Nisaidie upesi sana usiku wa leo kuyajibu maswali haya na kupata kila moja yayo niwezayo. Hata tutakapokutanika hapa tena adhuhuri ya leo, wabariki. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,

Na kununua wokovu wangu
Mtini Calvari.

³⁰⁵ Imeandikwa pale, niliyaandika kusudi yapate kuwa mbele yangu daima: “Kristo mbele yangu, minapoyajibu maswali haya.” Mnaamini nilisema hayo kutoka moyoni mwangu? Kila kitu kinatoka moyoni mwangu kuwasaidieni.

Wengine wao huenda wakaja kuchukua vifurushi vyao hapa.

³⁰⁶ Mungu mpendwa, hapa mna lesu, vifurushi vilivyoo hapa. Vinaenda kwa wagojwa na wanaoteseka. Hebu na yule Mfasiri mkuu wa Neno, Roho Mtakatifu aliyeliandika, na aje karibu sasa katika sehemu hii ya ibada apate kubariki vitambaa hivi. Bwana, nikiwaza habari zangu mwenyewe, mimi ni nani kuweka mwili wangu mchafu na wenye taka juu ya hizi lesu ambazo zinasimama kati ya mauti na uzima kwa watu wengi. Ee Mungu, mimi natetemeka. Bali ninapowazia ya kwamba. . . Wewe hunioni, unasikia tu sauti yangu. Inapitia katika Damu ya Yesu Kristo kule. Sasa, ninaamini ya kwamba utanjibu tu kama ulivyomjibu Yeye, kwa maana Yeye alienda kwa ajili yangu kuketi kwenye mkono wa kulia, kule juu, wa Ukuu kule juu. Na Damu Yake iko kule kama upatanisho, nami nimefunikwa chini ya Damu hiyo.

³⁰⁷ Naamini, Bwana, kuwa Wewe utawaponya, kwa maana wana mahitaji. Hawangaliziweka hizi hapa. Naomba kuwa utamponya kila mmoja. Kama ninavyojiweka mwenyewe kati yao, kama. . . Wao walivyosema walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo. . . Yeye alikuwa tu pia mwenyewe dhambi, Bwana, aliyeokolewa kwa neema Yako. Watu walimwamini, ijapokuwa yeye aliwakemea na kila kitu, lakini walijua yeye alikuwa mchungaji. Wao walijua yeye—alitungwa toka Kwako, kwa sababu Wewe ulijidhihirisha Mwenyewe kwa huduma Yake. Mungu, watu hawa wanaamini vivyo hivyo leo. Nakuomba Wewe uwasaidie sasa na kumponya kila mmoja wao katika Jina la Yesu Kristo, Amina.

³⁰⁸ Je, mnasikia njaa? Vema. Nina njaa kwa ajili ya maswali zaidi. “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Sasa, huenda nikawa. . . Baadhi ya maswali haya, huenda nisyajibu sawa sawa; nimefanya tu kadiri niwezavyo. Usiku huu, nitajaribu tu saa moja usiku. Vema, kanisa litafunguliwa saa kumi na mbili na nusu. Nanyi mnaoweza kukaa. . . Ninyi ambao hamwezi, tunafhamu; hilo ni sawa. Lakini nitajaribu kupata kila moja ya haya niwezavyo usiku huu. Mungu awabariki hata tutakapoonana.

Sasa, hebu na tusimame kwa miguu yetu na tuimbe huu wimbo mzuri wa kale, wimbo wetu wa kumalizia, *Peleka Jina la Yesu*.

Peleka jina la Yesu
 Ko kote uendako;
 Litafurahisha moyo,
 Peleka uendako.

Thamani, na tamu
 Ni jina lake Yesu;
 Thamani na tamu
 Ni jina lake Yesu.

³⁰⁹ Nataka kutoa tangazo hili. Billy alisema walichukua sadaka ya upendo asubuhi hii (ona?), na kusema walikuwa na sadaka nzuri ya upendo. Nimemwambia aende upande wa nyuma wa jengo hili na asimame nyuma kule. Kwa watu hapa ambao hawakuja wakiwa tayari, hawana pesa za chakula chenu cha kutwa, Billy atawapa pesa kwa chakula chenu cha kutwa na kwa ajili—kulipia malipo yenu ya hoteli au malipo ya mikahawa ya barabarani, cho chote kile. Zichukueni mkalipie hivyo sasa. Kama una . . . Kama unaweza kukaa . . . Billy atakukuta nyuma kule na aandike jina lako na unakoishi, na tutakulipia chakula chako cha kutwa na gharama zako za mkahawa wa barabarani kwa matoleo ya hiari ambayo yamechukuliwa kwa ajili yangu asubuhi hii.

Hata twonane!
 Hata twonane kwake kwema;



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org